

NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU: UTANGULIZI: Kanisa na Changamoto ya Ombwe la Viongozi Waadilifu katika Karne ya ishirini na moja

“Nioneshe kiongozi mwadilifu”. Hiki ndicho kichwa cha somo letu, katika semina yetu mwaka huu. Na katika siku tatu zijazo, tutakuwa tukiangalia nini maana ya kuwa kiongozi mwadilifu. Nini maana ya uadilifu? Je, kama wachungaji na wainjili, mnaongoza makanisa yenu kwa uadilifu? Je, nini hutokea kiongozi anapokosa uadilifu? “Nioneshe kiongozi mwadilifu”. Ili kutusaidia katika masomo yetu wiki hii, nitakuwa ninatumia vitabu viwili. Moja ya vitabu hivi ni Biblia. Tutakuwa tukitumia muda mwinge kuangalia Neno la Mungu. Tutakuwa tukiangalia baadhi ya watu katika Biblia, amba walikuwa viongozi waadilifu. Na kitabu kingine, ambacho nitakuwa nikitumia, ni hiki hapa: “*Nioneshe Kiongozi Mwadilifu: Kanisa na Changamoto ya Ombwe la Viongozi Waadilifu, katika Karne ya ishirini na moja*”.

Mafundisho mengi wiki hii yanatoka katika kitabu hiki, kilichoandikwa na mtu anayeitwa Donald Leo Mtetemela. Yeye siyo mchungaji wa AIC. Yeye ni mchungaji mstaafu wa Anglikana, ambaye kwa sasa anaishi Iringa na mke wake. Yeye alizaliwa mwaka **1947** – hii inamaana kwamba kwa sasa ana umri wa miaka **70**. Lakini, kwa miaka **35** alikuwa mchungaji, askofu, na pia askofu mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania. Na hii inamaana kwamba, nusu ya maisha yake, amekuwa kiongozi katika kanisa.

Alisoma theologia katika mkoa wa Dodoma, na pia Uingereza, na huduma yake ilianza mwaka **1971**. Kwa kazi yake ya kwanza katika kanisa, alitumwa katika kijiji, ambako hapa kuwa na Kanisa la Anglikana. Na kwa hiyo, kazi yake iliwa ni kupanda na kuanzisha kanisa jipya. Alikuwa mtu mwenye wito wa uinjili, na kupanda makanisa. Na ndio maana, kanisa hilo jipya lilikua. Alitambulika kama kiongozi mzuri katika kanisa, na mwaka **1990**, alikuwa Askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Ruaha. Alikaa katika wadhifa huo kwa miaka **20**. Katika kipindi hicho, pia alichaguliwa kuwa Askofu Mkuu wa kanisa la Anglikana Tanzania; wadhifa aliokaa nao kwa miaka **10**. Huyu ni mtu mwenye uzoefu mwinge, katika huduma za kichungaji, na ninatumaini kwamba tutaweza kujifunza mambo mengi, kutoka kwake ndani ya siku hizi **3**. Alipostaafu miaka michache iliyopita, aliamua kuandika kitabu hiki – kwa sababu alihisi kwamba jambo hili, lilikuwa muhimu sana katika kanisa leo.

“Huenda hakuna jambo lingine kubwa linalowasumbua watu katika nyakati hizi, hapa Tanzania na katika Afrika kwa jumla, kama uhaba wa viongozi wenyewe uadilifu na wacha Mungu. Naamini kitakuwa faraja kwa wale amba wamekatishwa tamaa na maisha ya ubiniasi na tabia mbaya za viongozi wao Kanisani, na katika jamii na taifa. Kitawasaidia kuwa waangalifu wanapofikia hatua ya kuchagua viongozi. Kitabu hiki kitakuwa msaada kwa wale walio katika nafasi za uongozi. Kitakuwa kama mzani amba kila mtu anastahili kusimama juu yake kujipima, na kuchukua hatua”.

Je, ni jinsi gani kitabu kinaweza kuwa kama mzani? Labda una mzani wowote nyumbani. Labda unapokwenda kwa daktari, utapimwa. Unaposimama juu ya mzani, utaona una uzito gani. Labda, kilo **70**? Labda kilo **60**, au **80**, au hata **90**?! Na kama daktari anafikiri kwamba una uzito mwinge – unaweza kuambiwa kwamba unapaswa kudhibiti kula chakula kingi, na kupunguza kiasi fulani cha uzito ili uwe na afya bora. Mzani utakuambia kama unapaswa kuchukua hatua. Kwa jinsi hiyo hiyo, tutakavyo tumia muda kuangalia katika kitabu hiki, na kuangalia umuhimu wa jambo hili, utaweza kuona una uzito kiasi gani – siyo katika kilo; siyo kimwili - lakini kiroho, kama kiongozi. Utaweza kuona kama wewe ni mchungaji au mwinjili mwidilifu. Labda, baada ya kuangalia katika somo hili, utataka kusoma zaidi, na siku ya alhamisi asubuhi, nitakupa kitabu kimoja, ili uweze kusoma kwa undani kuhusu jambo hili.

Ngoja niwape muhitasari mfupi wa kitabu hiki, ili mweze kujua kitu ambacho tutakuwa tunajifunza, katika siku hizi **3** zilazo. Sitakuwa ninaangalia kila sura kwa undani, kwa sababu hatuna muda wa kutosha, lakini nitakuwa ninachagua mambo machache kutoka kila sura. Nitatumia baadhi ya nukuu, na hadithi kutoka kwenye kitabu hiki, lakini pia, nitakuwa ninaongeza mawazo, na hadithi, kama tunavyo tumia Neno la Mungu kuleta ujumbe wa kitabu. Katika **sura ya kwanzu**, Askofu Mtetemela ameanza kwa kuangalia changamoto za uongozi, katika karne ya ishirini na moja. Je, hali iko vipi katika ulemwengu kuhusu viongozi? Je, hali iko vipi katika kanisa kuhusu uongozi leo?

Katika **sura ya pili** anaangalia sababu zinazowafanya watu waamue kuwa viongozi; anaangalia sababu zote mbaya, na nzuri. Katika **sura ya tatu**, anaangalia somo la uadilifu. Kwa huzuni, anasema kwamba katika kanisa leo, kuna ombwe la viongozi waadilifu. Na anasema kwamba, jambo hili linaumiza kanisa. Na kwa hiyo, swali lake ni hili: wako wapi viongozi waliojaa uadilifu? Anasema hivi: “*Nioneshe Viongozi Waadilifu*”. Katika **sura ya nne**, analenga juu ya sifa za kiongozi wa kiroho, na tutakuwa tunatumia muda mwinge, katika sura hii, tukiangalia baadhi ya sifa anazopaswa kuwa nazo kiongozi wa kiroho. Je, mchungaji

anapaswa kuwa na tabia gani? Tutaona. Nadhani ni katika sura hii, kuna sehemu ambayo inatuwezesha kujipima wenyewe, na hili linaweza kuwa jambo lenye changamoto. Ujumbe wa **sura ya tano** unahusu ‘majaribu’. Na tutaangalia baadhi ya majaribu, ambayo viongozi wa kanisa wanakutana nayo leo. Mara kwa mara, tunasoma kuhusu wachungaji, ambao wanaanguka katika majaribu, na kuharibu huduma zao. Wakati mwingine wanajiharibu wenyewe, familia zao, na hata makanisa yao, kwa sababu hawakupinga majaribu. Na kwa hiyo, tutaangalia baadhi ya majaribu, ambayo kiongozi wa kanisa anakutana nayo.

Sura ya sita inahusu migogoro katika kanisa. Je, ni maeneo gani ya migogoro ambayo kiongozi atakutana nayo? Je, tunaweza kufanya nini, kuzuia migogoro katika huduma zetu, na je, tunakabilianaje na migogoro inapokuja? Kwa sababu kuna wakati itakuja. Na kisha, sura ya mwisho: **sura ya saba** inahusu kustaafu. Kwa baadhi yenu, kustaafu ni jambo ambalo liko mbali sana, na pengine hujawahi hata kufikiri juu ya hilo. Lakini kwa wengine, linaweza kuwa jambo lisilo mbali. Je, tunajiandaaje kwa ajili ya siku yetu ya kustaafu? Hatutakuwa na muda wa kuangalia jambo hili, katika sura hii, kwa sababu kuna mambo mengi sana ya kujifunza katika sura zingine, lakini utaweza kusoma kuhusu jambo hili mwenyewe, tutakapo kupa kitabu siku ya Alhamisi.

Hapa ni nukuu kutoka kwa Askofu Mtetemela, ambalo linaweka mhitasari wa kitabu kizima: “*Kuna msingi mmoja tu wa uongozi, iwe katika uongozi wa kiroho, au wa kidunia. Kiongozi anapaswa kuwa mfano mzuri, kwa wale anao waongoza! Kama kiongozi siyo mfano mzuri, itakuwa rahisi kukataliwa na watu anao waongoza, aidha ana kwa ana, au ndani ya mioyo ya watu hao. Huu ni ujumbe wa kitabu hiki*”. Tunapoanza masomo yetu wiki hii, ni vizuri kutulia na kutafakari swalii hili: Je, sisi ni viongozi wanao onesha mfano mzuri, katika makanisa yetu? Watu katika makanisa yetu wanapotuangalia, je, wanatuona kama viongozi waadilifu? Wanapokuangalia wewe, je wanaona mchungaji ambaye ni mfano mzuri, au watu katika kanisa lako, wanamatamani kupata mchungaji mwingine?! Kiongozi anapaswa kuwa mfano mzuri kwa wale anao waongoza – na anaweza kufanya hivyo, kama yeze ni kiongozi mwadilifu. Ninatumaini hii inakupa picha kamili ya kitabu hiki, na tutakachokuwa tukiangalia wiki hii.

NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU: KIPINDI 1: **Kenya na Changamoto ya Ombwe la Viongozi Waadilifu** **katika Karne ya ishirini na moja.**

Kwa muda wote wa kipindi hiki, nataka kuangalia kuhusu anachosema Askofu Mtetemela, katika sura ya kwanza na ya pili ya kitabu hiki. Kuna mambo ambayo nataka tuangalia. **1:** Changamoto kuhusu uongozi tunazo kutana nazo, katika ulimwengu huu, na kanisa. **2:** Je, ni namna gani viongozi walichaguliwa katika Biblia? Na sifa gani zili angaliwa kwa wale walio chaguliwa. **3:** Kwa nini kanisa linachangamoto katika kuchagua viongozi leo? Na kwa kweli, haya yote yapo katika kichwa cha somo: “*Nioneshe kiongozi mwadilifu*”.

Ninajua kwamba katika Tanzania, na sehemu zote ulimwenguni, kuna watu wengi ambao ni viongozi wazuri. Lakini, ninajua kwamba kuna viongozi wengi sana ambao si mfano mzuri. Wakati mwingine tunaposililikiza redio, au tunapoangalia TV, au tunaposoma magazeti, tunaona kwamba kuna habari nyingi za huzuni za viongozi, ambao wamehusika katika tuhuma nyingi za rushwa. Tunasikia kuhusu kiongozi fulani, na tunajuliza wenyewe, walipataje uongozi wakati wanatabia mbaya? Na kutohana na uongozi mbaya, nchi zinaweza kuititia vita vya wenyewe kwa wenyewe, mtikisiko, na umaskini. Hatuwezi kutaja nchi hizo zote, kwa sababu ni nyingi sana! Hebu fikiri kuhusu **Zimbabwe** leo, na mgogoro ambao nchi hiyo inapitia, kwa sababu ya uongozi mbaya wa mtu mmoja.

Hebu fikiri kuhusu nchi kama **Ethiopia** na **Uganda**, katika siku za nyuma ambazo ziliwuwa na viongozi kama, Mengistu, na Idi Amin. Hebu fikiri kuhusu nchi kama **Jamhuri ya Afrika ya Kati**, na **Congo**, ambazo zinaendelea kuwa na matatizo hadi leo, kwa sababu ya uongozi mbaya. Wiki chache zilizopita, nilisoma makala kwenye mtandao juu ya Jamhuri ya Afrika ya Kati. Nilikuwa nikisoma kuhusu mtu mmoja, ambaye alikuwa Rais wa nchi hiyo, miaka **50** iliyopita. Jina lake alikuwa Bokassa. Hapakuwa na uchaguzi. Alichukua madaraka kwa mapinduzi ya kijeshi, na kujitangaza mwenyewe kuwa Rais, siyo kwa muhula mmoja, au miwili, lakini kwa maisha yake yote! Kulikuwa na sherehe kubwa ya kumchagua yeze kama Rais, na alitumia mamiliioni ya dola kwa ajili ya tukio hilo, ingawa nchi hiyo ilikuwa maskini sana.

Mwaka **1979** alitengeneza sheria – kwamba shule zote za watoto zilipaswa kununua sare. Lakini walipaswa kununua kutoka duka moja. Lakini duka hilo liliimiliwa na mmoja wa wake zake! Matokeo ya sheria hiyo yalisababisha migomo katika mitaa – na wanajeshi wa serikali waliambiwa kuzuia kwa nguvu. Zaidi ya watoto **100** waliuawa katika mitaa siku hiyo! Taarifa ilisema kwamba, Bokassa mwenyewe, yawezakana aliwaua badhi ya watoto hao. Na huyu ni kiongozi wa nchi! Huu ni mifano mdogo tu, wa kiongozi asiye mwadilifu. Kuna mifano mingi sana mibaya, ambayo tungeweza kutaja.

Viongozi wengi wamezungukwa na tuhuma za rushwa, hongo, dhuruma, matumizi ya nguvu, na maisha ya siyo na uadilifu. Wengine wamepuuza haki. Hawasimami kwa ajili ya wale wanao wawakilisha. Baadhi ya viongozi wamesahau wajibu wao, na badala ya kutumikia nchi zao, wanajifaidisha wenyewe! Na ni huzuni kuona jinsi baadhi yao wametumia uongozi kujipatia utajiri wenyewe, wakati huo huo kuna watu wengi katika nchi zao wenye uhitaji mkubwa. Aina hii ya uongozi ina patikana katika ngazi zote za jamii. Inatokea katika ulimwengu wa biashara. Inatokea katika serikali za mitaa. Inatokea katika jeshi la polisi. Inatokea katika kila ofisi!

Watu wengi sana hawaoni viongozi waadilifu. Wanaona mifano ya viongozi wabaya tu. Na kwa sababu hiyo, wamepoteza imani na tumaini katika viongozi wao. Lakini kwa huzuni, kama tunavyo juu sote, hii haitokei kwa viongozi wa kisiasa tu, au wale ambao si Wakristo katika jamii. Inatokea katika kanisa. Wachungaji, viongozi wa kanisa, wainjilisti, viongozi wa kwaya, maskofu – baadhi yao pia wameshindwa kuonesha uadilifu katika huduma zao. Wengi wao wameanguka katika rushwa, uzinzi, na mambo ya aibu. Na ndiyo, hata katika kanisa, wakati mwingine watu hutumia hongo ili kupata nafasi za uongozi! Tuhuma kubwa zimekuwa zikisemwa zidi ya viongozi wa kanisa. Haijalishi unazumgumzia dhehebu gani: Baptisti, Anglicana, Roman Katholiki, Pentekoste, AIC, na kadhalika. Inasikitisha kwamba, hii inatokea katika madhehebu yote.

Badala ya kuwa viongozi waadilifu, na wenye utakatifu, baadhi ya viongozi wamekuwa kama viongozi wabaya, ambao wapo kwenye jamii ya kawaida. Matokeo ya jambo hili ni kwamba, watu hawawezi kuona tofauti iliyopo kati ya tabia za wachungaji, na viongozi wengine katika jamii ambao hawamjui Mungu! Hawawezi kuona tofauti yoyote! Wanaweza kumuona Rais mwenye tabia mbaya, na Mchungaji mwenye tabia mbaya, na wanaweza kusema, “*Sijui ni yupi aliye mtu wa Mungu*”! Hili ni jambo kubwa, na lina kumkufuru Mungu. Ni huzuni kwamba, huu ndio uhalisia katika baadhi ya makanisa leo. Lakini, siyo tatizo jipya. Ni tatizo la siku nyingi, ambalo limekuwa likitokea katika historia.

Unaposoma Agano la Kale, utaona limejaa watu, viongozi, makuhani, na wafalme – ambao hawakuwa na uadilifu wowote. Na ilimfanya Mungu ahuzunike na kuchukia sana. Ngoja nitaje mifano michache: Kulikuwa na tatizo hapo mwanzo, katika Kitabu cha **Mwanzo**, miaka **4000** iliyopita. Je, unaikumbuka hadithi ya Sodoma na Gomora, katika **Mwanzo 18**? Mungu alimwambia Ibrahimu kwamba angeharibu miji. Kwa nini? Kwa sababu watu waliyoishi katika miji hiyo walikuwa waovu sana. Hawakuwa na uadilifu wowote. Ibrahimu alifanya nini? Alimsihi Mungu asiharibu miji. Kwa kweli, alijaribu kupatana na Mungu. Alimwambia Mungu: “*Vipi kama kutakuwa na watu wenye haki hamsini katika mji, je, utauharibu?*” Kwa maneno mengine, “*kama utakuta watu hamsini waadilifu katika mji, je, utaiharibu Sodoma*”? Na Mungu akasema: “*Kama nitakuta watu wenye haki hamsini sitauharibu mji*”. Tunajua hadithi yote, siyo? Ibrahimu anaendelea kumuliza Mungu kwa idadi ya ndogo. Alianza na 50, na kisha 45, na kisha 40, 30, 20, na hatimaye 10!

Mungu akasema: “*Sawa, kama nitakuta watu kumi waadilifu, sitauharibu Sodoma*”. Lakini kwa huzuni, hata idadi hii ndogo ya watu haikuwepo. Ingawa yapata watu maelfu wali-ishi humo, Mungu hakukuta hata watu **10** waadilifu! Mungu anasema: “*Nioneshe watu waadilifu, na sitawaharibu*”! Lakini hakuweza kupata hata watu **10!** Katika **Mwanzo 19:28** kuna picha ya huzuni sana. Siku iliyofuata, Ibrahimu anaangalia miji, lakini aliona moshi tu, kwa sababu Mungu alikuwa ameharibu miji yote. Hali ilikuwa hivyo katika kitabu cha kwanza cha Biblia! Hapa kuwa na watu wengi waadilifu.

Miaka **600** kabla ya Yesu Kristo – hali ilikuwa hivyo hivyo pia, hata mionganini mwa Waisraeli. Na kumbuka, Waisraeli walikuwa watoto wa Mungu; walikuwa watu wa Mungu, na Mungu alikuwa amewaleta katika nchi ya ahadi – na bado hawakuwa na uadilifu. Katika mji wa Yerusalem, hali ilikuwa mbaya sana. Mungu anatoa agizo kwa nabii Yeremia. **Yeremia 5:1***. Lakini, hebu hisi nini kilitokea? Hakupatikana mtu mwadilifu hata mmoja!

Mifano hii miwili, inauhalisia kwa watu – lakini unaweza kuwa na uhakika wa hili, kama watu hawana uadilifu, kwa sehemu fulani hali hii inachangiwa na viongozi kukosa uadilifu. Watu hawajaoneshwa mifano mzuri. Kuna mifano mingi sana, katika Agano la Kale, ambapo Mungu aliwakemea viongozi wa Israeli, pamoa na makuhani, kwa kuongoza bila uadilifu. Kwa jinsi hiyo kama ilivyo kwa Yeremia, kulikuwa na nabii mwingine jina lake Ezekiel. Watu hawa wote, walikuwa wenye haki, na waadilifu; walikuwa watu walio

mwabudu Mungu. Walikuwa na wajibu wa kusema ujumbe huu huu kwa watu wa wakati huo. **Ezekieli 11:12** na pia **Ezekieli 34:2-4***: Mungu anahasira sana na viongozi hapa, kwa sababu wanaenda kinyume na jinsi kiongozi wa kiroho anavyopaswa kuwa.

Ngoja nisome kutoka kitabu cha **Malaki**, kwa sababu hapa, hakuna mashaka kuhusu Mungu anamwambia nani. Anawaambia makuhani wa Israeli. Analalamika kuhusu viongozi wa kiroho, ambao siyo waadilifu. Na ninaposoma hii, sikiliza kwa makini, kwa sababu ninafikiri kwamba, hii pia inaeleza kuhusu baadhi ya wachungaji leo. **Malaki 2:7-8***: Mungu anahasira sana na viongozi hapa.

Kama tungekuwa tuna-itikia mistari hii leo - ingemainisha hivi: “*Mdomo wa mchungaji unapaswa kutangaza kweli kuhusu Mungu. Watu katika kanisa, wanapaswa kuwa na uwezo wa kwenda kwa mchungaji, na kuomba ushauri wa kibiblia kutoka kwake. Lakini, wachungaji wengi wameacha njia – na mafundisho ya kupotosha wanayofundisha yanasaababisha watu wengi wapotee. Wachungaji wengi, wahubiri, wainjiliisti, na viongozi wa kanisa, inasikitisha kwamba, hawaongozi kwa uadilifu*”. Na kama tulivyoona, hivi ndivyo ilivyokuwa katika Agano la Kale. Yeremia alikuwa anawaambia watu wa Yerusalem: “*Nioneshe mtu mwadilifu*” – na hakuna hata mmoja aliyepatikana. Ezekieli na Malaki, walikuwa wakisema: “*wako wapi viongozi waadilifu?*” Mungu alikuwa akiwaambia wale makuhani: “*Ninataka kuona kiongozi mwadilifu. Nioneshe kiongozi wa jinsi hiyo*”. Je, Mungu angesema nini leo?

Askofu Mtetemela anasema katika utangulizi wa kitabu hiki. “*Kuna mambo mengi ya kuzungumza kuhusu ukosefu wa viongozi waadilifu leo. Hii imekuwa changamoto kwa vizazi vingi. Watu wanatafuta viongozi wenyewe maadili mazuri kwa ajili ya kuwaongoza. Wanataka mtu ambaye watamfuata kwa uhakika, wakijua kwamba atawaongoza vizuri. Hawataki kumfuata mtu ambaye si mwenye haki – lakini mtu mwadilifu na anayemwabudu Mungu. Jamii ya kanisa inasema: tafadhalii tuoneshe viongozi waadilifu. Hili ni jambo kubwa ninaloleta katika kitabu hiki: uadilifu wa viongozi! Je, tunaweza kuwapata wapi?*” Je, tunaweza kumpata ye yote hapa? Natumaini sana hivyo. Na ninatumaini kwamba kufikia mwisho wa wiki hii, tutakuwa tumepata picha kamili kuhusu nini maana ya kuwa kiongozi mwadilifu, na kwamba tutatoka hapa tukiwa na shauku, na makusudi ya kuwa kiongozi wa jinsi hiyo.

Tumeona kwamba, moja ya changamoto kubwa kwa kanisa leo, ni kuchagua viongozi wake. Ni jukumu kubwa, na wale wanaofanya maamuzi haya, wanahitaji kufanya kwa uangalifu mkubwa. Na kwa muda mfupi, nataka tuangalie sababu chache, kwa nini kanisa wakati mwagine, hufanya makosa katika kuteua viongozi. Lakini, kabla ya hapo, ngoja tuangalie kwenye Biblia jinsi viongozi wa kiroho walivyo-chaguliwa, na kwa nini walichaguliwa.

Jambo la kwanza la kuzungumza ni kwamba, katika Agano la Kale, ni Mungu ambaye alichagua viongozi wake. Mungu alimwita **Nuhu** kujenga safina. Unaweza kuhoji kwamba hiyo haikuwa nafasi ya uongozi, lakini alichaguliwa kwa ajili ya kazi maalumu. Lakini, nataka tuone sababu ya Mungu kumchagua Nuhu kwa ajili ya kazi hiyo. Nafikiri kwamba **Mwanzo 6:9** inatupa jibu: “*Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu*”. Hii ndiyo sababu kwa nini alichaguliwa. Katika **Mwanzo 12** tunaona kwamba, Mungu alimchagua **Ibrahimu** kuwa baba wa taifa la Wayahudi: Mungu alimwambia: “*toka katika nchi yako, na watu wako, na nyumba ya baba yako, na uende katika nchi nitakayo kuonesha*”. Hatujaambiwa sana kuhusu sifa za Ibrahimu, katika **Mwanzo 12**. Hatusomi kuhusu sifa za uongozi wake, lakini tunajua kwamba alikuwa mtu wa imani, na mtu mtii. Mungu alisema ‘*nenda*’ - na alikwenda, ingawa hakujua alikuwa anakwenda wapi! Huu ni utii kamili kwa Mungu.

Alikuwa ni Mungu aliyemwita na kumchagua Musa, kuwatoa watu wake kutoka Misri. Alikuwa ni Mungu aliyemwambia Musa kumteua Yoshua kama mrithi wake. Yoshua ndiye angewaongoza Waisraeli kuvuka Yorodani, na kuingia katika Nchi ya Ahadi. Yeye alikuwa ni mtu aliyemtumikia Mungu vizuri.

Katika **1 Samweli 16** - ni Mungu aliyemchagua Daudi kuwa mfalme wa Israeli. Na ninafikiri kwamba hapa kuna kitu fulani, ambacho tunaweza kujifunza kuhusu hadithi hii, juu ya kuchagua viongozi.

Je, unakumbuka Mungu alipomtuma Samweli kwenda kumpaka mafuta mfalme? Samweli alijua kwamba alikuwa ni mmoja kutoka watoto **8** wa Yese, lakini hakujua ni yupi. Mungu alikuwa amesema tu: “*utampaka mafuta nitakaye kuonesha*”. Mnapochagua watu kuwa viongozi katika kanisa lenu, kabla ya kuanza mchakato, je, huwa mnaomba Mungu awaoneshe nani anamtaka? Au huwa mnachagua mnayemptaka tu? Mungu alimwambia Samweli: “*Nitakuonesha nani wa kumchagua*”. Lakini, kuna mambo mengi katika hadithi hii, ambayo yanaweza kutufundisha somo kuhusu kuchagua viongozi.

1 Samweli 16: Mtoto wa kwanza wa Yeso alilingia chumbani (jina lake lilikuwa Eliabu), na Samweli alivutiwa na mwonekano wake. Alifikiri mwenyewe: “*hakika, huyu ni mpakwa mafuta wa Bwana*”; huyu ndiye atakuwa kiongozi ajaye wa Israeli. Je, unakumbuka Mungu alimwambia nini Samweli? Mstari wa saba: “*Usitazame uso wake, wala urefu wake – kwa maana mimi nimemkataa*”. Lakini, sikiliza maneno yanoyofuata ambayo Mungu alimwambia Samweli: “*Binadamu huangalia uzuri wa nje, lakini mimi ninaangalia moyoni*”. Kwa maneno mengine, haijalishi anaonekanaje kwa nje, cha muhimu ni sifa yake ya ndani. Wakati mwininge, tunapochagua viongozi, watu wanafikiri kuhusu mwonekano wa nje, na wanasahau kwamba kitu cha thamani ni utu wa ndani.

Mungu anamwambia Samweli, na sisi: sahau kuhusu mwonekano wa nje, na badala yake, nioneshe kiongozi mwadilifu! Kwa sababu hicho ndicho kinachotakiwa. Sifa ndiyo jambo la muhimu. Na tunajua kwamba hatimaye, Daudi ndiye alipakwa mafuta na kuwa mfalme. Pia tumeambiwa katika ujumbe, kwamba wakati huo, “*Roho wa Bwana akaja juu ya Daudi kwa nguvu*”. Na akawa mfalme mwenye mafanikio kuliko wote katika Israeli. Biblia inatuambia kwamba, ingawa Daudi alifanya makosa machache, alikuwa ni mtu aliyemuata Mungu, na alikuwa mtii kwake.

NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU: KIPINDI 2: Changamoto za uongozi na viongozi katika Biblia.

Na kwa hiyo, katika mifano hiyo yote, alikuwa ni Mungu ambaye alichagua kiongozi. Nuhu alikuwa mtu mwenye haki na asiye na lawama. Ibrahimu alikuwa ni mtu wa imani na utii. Musa, kama kiongozi, alivumilia katika matatizo mengi. Yoshua alikuwa ni mtu mwenye utii na mkweli. Na Daudi alikuwa ni mtu mwenye moyo wa hofu ya Mungu; mtu ambaye Mungu alijua atamtegemea katika kufanya kazi yake. Kuna mambo mengi sana ambayo tungejifunza kutoka kwa watu hawa, amba Mungu alikwachagua kama viongozi, ingawa wakati mwininge walifanya makosa.

Pia kuna matukio mengi katika Agano la Kale, tunapoona viongozi wakichaguliwa na watu, na si moja kwa moja na Mungu. Katika kitabu cha **Kutoka 18** unaweza kumkumbuka baba mkwe wa Musa, mtu aliyeitwa Yethro, alimpa Musa ushauri kuhusu namna ya kuchagua wasaidizi. Na ulikuwa ushauri mzuri. Alimwambia Musa, kama hauta chagua viongozi wakukusaidia, utashindwa. Kazi unayoifanya, ni kubwa sana kufanya na mtu mmoja. Hivi ndivyo alisema: “*Chagua mionganini mwa watu wote, watu wanaostahili, watu wanaomcha Mungu, waaminifu na wanaochukia kuhongwa*”.

Na tumeambiwa kwamba Musa alikubali ushauri, na alichagua viongozi wa kumsaidia. Lakini, hebu ona nini kilihitajika kwa viongozi hawa. Lazima wawe na hofu ya Mungu; heshima kwa Mungu, na lazima wawe wakweli, na waminifu. Hapa kuna swali kwako. Je, hii inakuelezea wewe kama kiongozi? Kama watu wa kanisa lako wangeulizwa: ‘*je, hii inaeleza kuhusu mchungaji wako?*’ Je, unafikiri wangesema nini? Je, unahofu takatifu ya Mungu? Je, ni mwa-minifu? Je, watu wanawenza kukuamini? Je, unaweza kukataa rushwa? Natumaini kwamba jibu la maswali haya ni ‘*ndiyo*’. Ngoja tuangalie katika Agano Jipy, kwa sababu katika Injili, tunamwona Yesu akichagua mitume **12**. Hao ndio wangekuja kuwa viongozi, katika kanisa la mwanzo. Fungua **Luka 6:12-13**: Hatujaambiwa chochote kuhusu sifa zao. Lakini, nataka tuone kitu fulani ambacho tunaweza kujifunza, hasa kwenu ninyi amba Mungu huchagua viongozi wengine. Angalia mstari **12**: Tumeambiwa kwamba, usiku mzima Yesu alikuwa nje, juu ya mlima, katika maombi. Kwa nini? Kwa sababu, ilipofika asubuhi, alikuwa na kazi muhimu ya kuchagua wanafunzi wake, na kuchagua watu amba Mungu, na kuhusu viongozi wa kanisa la mwanzo. Hii ilikuwa ni muhimu kwake.

Ilikuwa muhimu sana, kwamba Yesu aliamua kukaa macho usiku mzima, ili kwamba aweze kuomba kwa Baba yake wa mbinguni, ili ajue ni wanafunzi gani atawachagua siku iliyofoata. Hii ilikuwa kazi kubwa. Mara kwa mara, tunafikiri tu kwamba Yesu alikuwa na wanafunzi **Kumi na wawili**, lakini ukialangalia kwa makini mstari **13**, inaonekana kwamba alikuwa na kundi kubwa la watu walio mfuata. “*ilipokuwa asubuhi, aliwaita wanafunzi wake, halafu akachagua kumi na wawili kutoka mionganini mwao*”. Hatujui kwa undani kwamba kulikuwa na wafuasi wangapi – lakini tunajua kwamba, kulikuwa na kundi dogo la wanawake waliokuwa wakimfuata, na katika **Luka 10**, tumeambiwa kwamba, Yesu alichagua wanafunzi **72** na akawatuma kwenda kum-tayarishia njia. Lazima walikuwa wanafunzi wake. Yesu anapoamua kuchagua wanafunzi kumi na wawili tu, anachagua kutoka kundi kubwa la watu. Lakini, jambo muhimu la kuangalia hapa, ni kwamba, kabla ya kufanya uamuzi wa kuchagua, Yesu alifikiri kwamba, ilikuwa muhimu kwake kutumia muda mwingu katika maombi.

Kama Yesu alihitaji kutumia muda katika maombi, kabla ya kufanya uamuzi, je, sisi tunahitaji kufanya maombi kwa kiasi gani, kabla ya kufanya maamuzi? Sijawahi kuwa katika kikao cha sinodi ya AIC, kwa hiyo sijui ni jinsi gani mambo hufanyika. Natumaini kwamba, wanapofanya maamuzi juu ya nafasi za uongozi katika kanisa, kwamba huwa wanatumia muda mwingu katika maombi. Kwenu ninyi ambao hufanya uteuzi katika kanisa lenu: ya uhasibu, na katibu, na kadhalika – na tumaini kwamba, huwa mnatumia muda katika maombi, kabla ya kufanya uamuzi huo. Kumbuka, hii ni kazi ya Mungu, kwamba tunahusika ndani yake. Ni kanisa lake, siyo letu – na kwa hiyo, ni sahihi tu kwamba, tumwombe yeye atusaidie katika kufanya maamuzi haya muhimu. “*Baba, tuoneshe kiongozi mwadilifu*”. Tunahitaji kumualika Mungu, katika mchakato tunapochagua viongozi.

Je, ni kwa namna gani kanisa la kwanza lilichagua viongozi? Unaposoma kitabu cha Matendo, tunaweza kuona kwamba, walifanya kwa makini sana. Fungua **Matendo 1**, kwa sababu hapa, tunaona uteuzi wa kiongozi katika kanisa la mwanzo. Katika mstari **15**, Petro anasimama na kusema kwa kanisa. Tumeambiwa kwamba, walikuwepo waumini wapatao **120**, katika mkutano huo. Je, Petro anataka kuwaambia nini? Anataka kusema kuhusu Yuda Iscarioti, ambaye alimsaliti Yesu, na kujiuwa mwenyewe. Petro hata anatumia mstari kutoka Zaburi, kuelezea hali yao ya wakati huo. Angalia mwisho wa mstari **20**: “*Mtu mwengine achukue nafasi yake ya uongozi*”. Petro anajisikia kwamba, mstari huu, katika Zaburi, unahu hali yao. Anatumia Agano la Kale kuongoza matendo yao. Na kwa hiyo, wanakutana kujadili nani achukue nafasi ya Yuda. Ngoja tusome **Matendo 1: 21***.

Inaonekana kwamba kundi zima walikuwa na majadilano: Wanafunzi **120**, kujumlisha mitume **11**, na walikubaliana kupendekeza majina mawili ya kupigwa kura; Yusufu na Mathia. Hatujaambiwa kuhusu sifa za hawa watu wawili, lakini sifa zilizotakiwa, zimetajwa katika mstari **21** na **22**, nazo ni hizi: mtu wa kuchaguliwa alipaswa kuwa mfuasi wa Yesu, tangu mwanzo wa huduma yake, na aliyeshuhudia kufufuka kwa Yesu.

Hatuwezi kutumia vigezo hivi leo kwa viongozi wetu, lakini mifano ya kibiblia tunayo weza kufuata ipo, katikia mstari **24**: “*Bwana, wewe unajua mioyo ya watu wote. Hivyo utuoneshe ni yupi kati ya hawa wawili uliyemchagua ili achukue nafasi hii ya huduma ya kitume*”. Tambua tena umuhimu wa maombi. Wanataka kuongozwa na Mungu katika maamuzi yao. Hawaharakishi mbele na kuchagua tu mtu wanayemtaka. Wanaweka tumaini lao kwa Mungu – na kisha wanatumia utaratibu wa desturi wa kupiga kura. Hakuna kitu kama hicho kisicho na mpangalio, ambacho Mungu anajihuisha. Kama wanavyopiga hizo kura, waliamini kwamba, Mungu angetumia njia hiyo kuwaonesha kiongozi sahihi – na Mungu aliwaonesha. Waliamua pamoja kama kundi nani angechaguliwa. Halafu waliomba kuhusu hilo. Walimwomba Mungu kuwaongoza, na kisha waliacha uamuzi wamwisho kwa Mungu.

Kuna mfano mwengine katika kitabu cha Matendo, ambao nataka tuone kwa ufupi. **Matendo 6:2-6***. Katika Biblia yangu, kichwa cha somo ni “*kuchaguliwa kwa watu saba*”. Idadi ya wanafunzi ilikuwa ikiongezeki, na kulikuwa na migogoro, kati ya baadhi ya Wakristo wa Kiyahudi. Kundi moja lilisema kwamba, chakula kilipo kuwa kikitolewa kwa wajane kanisani, wajane wao hawakupewa. Lalamiko limesikika kwa mitume. Hawajalipuuza – wanalfanya kazi. Lakini tambua kwamba, hawafanyi uamuzi wenyewe. Mitume wanawaambia waumini, chagua watu **7**, na tutawapa wajibu wa kuhakikisha kwamba, wajane katika kanisa wanapata chakula cha kutosha. Nataka tuone mambo mawili hapa, kuhushu watu waliochaguliwa. Majina ya watu **7**, katika mstari **5**, yote ni majina ya Kigriki. Je, kwa nini jambo hili ni muhimu? Angalia mstari **1**: Je, mwanzo wa lalamiko hili unatoka wapi?

Tumeambiwa kwamba, walikuwa ni Wakristo wa Kigriki, ambao walilalamika kuhusu Wakristo wa Kiyahudi. Na kwa hiyo, kwa kujua kwamba hili lilikuwa ni tatizo, kwa Wakristo wa Kigriki, inaonekana kwamba, kanisa kwa makasudi walichagua watu **7** ambao walikuwa, na asili ya Kigriki, ambao yaweza kuwa waliongea Kigriki.

Hii inamaanisha kwamba, wangeweza kuwashudumia Wakristo wa Kigriki kwa ubora zaidi. Wangeweza kuhudumia vizuri, kwa sababu wao wenyewe walitoka katika kundi hilo. Huu ulikuwa uamuzi wa busara uliyofanyawa na kanisa. Hebu fikiri kuhusu hili – kama kungekuwa na tatizo katika kanisa hapa Tanzania, lakini kwa sababu fulani fulani, ikawa nitatizo kwa kabilia moja. Ngoja tuseme tatizo ni watu wanaotoka katika kabilia la Wamasai. Na kanisa limesikia lalamiko kutoka kwa Wamasai, na kuamua kuchagua viongozi kwa ajili ya kutatua tatizo hilo. Si fikiri kwamba, ingekuwa ni jambo la hekima, kama kanisa lingechagua watu **7** kutoka kabilia la Wasukuma, kwa ajili ya kutatua tatizo. Hii ingeleta tatizo kubwa zaidi. Kanisa katika Yerusalem walitambua jambo hili, na ndiyo maana walifanya jambo hili kwa umakini sana. Kwa hiyo, tunahitaji kukumbuka kwamba, kuna mambo mengine ambayo tunapaswa kufikiri tunapochagua viongozi.

Kuna jambo lingine ambalo nataka tuangalie, kuhusu watu waliochaguliwa katika mstari 3: Je, sifa kwa ajili ya kazi ni nini? "Kwamba wawe wamejaa Roho Mtakatifu na hekima". Kwa maneno mengine, tuoneshe watu 7 waadilifu! Kumbuka, huu sio mwongozo wa mafundisho. Hii ilikuwa ni kazi ya Mitume – na tunaona katika mstari 2. Watu hawa 7, walichaguliwa kama watumishi katika kanisa. Walipaswa kuwa wanagawa chakula, na kuhudumia miradi! Na bado – sifa zilizotakiwa ni kwamba lazima wawe wamejaa Roho Mtakatifu. Na kwa hakika, hizi sifa ndizo zinazotakiwa, kwa kila mmoja mwenye nafasi ya uongozi wowote katika kanisa.

Je, hii inamaana gani? Katika **Waefeso 5:18**, Paulo anasema: "Mjazwe na Roho Mtakatifu". Anatushi tuendelee kutembea na Roho Mtakatifu. Hasemi kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na hapa, katika **Matendo 6** – pia mwandishi hasemi kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sifa za hawa watu 7, ni kwamba ni watu, wanao mruhusu Roho Mtakatifu kutembea katika maisha yao. Wanapaswa kuwa watu, wanao ongozwa na Roho Mtakatifu, siyo watu wanao ongozwa na mawazo yao. Kisha kanisa liliwachagua – halafu mitume wakawasimika kama viongozi. Tuangalie mstari 6: Watu wale 7 waliletwa kwa mitume wakawaombea, na kuweka mikono juu yao. Tambua tena, umuhimu wa maombi katika mchakato huu.

Tumechukua muda kidogo tukiangalia namna viongozi walivyochaguliwa, katika Agano la Kale, na Agano Jipy. Ninatumaini kwamba, katika kuangalia aya hizi asubuhi hii, tutaona kwamba mchakato wa kuchagua viongozi, ulifanya kwa makini sana. Namna walivyo chagua viongozi ilikuwa pamoja na maombi mengi. Walikuwa makini kuhusu kuchagua mtu aliyejikuwa mwadilifu. "Nioneshe kiongozi mwadilifu". Lakini, swali lina paswa kuulizwa. Je, kanisa la leo, liko makini inapofika hatua ya kuchagua viongozi? Tunapochagua viongozi, je, kanisa huwa linamkaribisha Mungu katika mchakato? Je, huwa tunaomba kwa bidii kuhusu nani tumchague? Je, huwa tunachagua watu walio jawa na Roho Mtakatifu? Je, huwa tunaangalia sifa zao badala ya mwonekano wa nje. Na mara kwa mara, kwa sababu ya matatizo tunayo yaona na kuyasikia, tunapaswa kusema: 'hapana – hatufanyi hivyo kila mara'. Askofu Mtetemela anasema hivi: "Leo, kuna usemi mwingi kuhusu kukosekana kwa viongozi waadilifu katika kanisa". Kwa hiyo, kwa nini iko hivyo? Kwa nini baadhi ya makanisa huchagua viongozi wabaya? Kwa nini tupo katika hali hii? Kwa ufupi sana, ngoja-ni-washirikishe baadhi ya sababu kutoka kwenye kitabu:

Wakati mwingine, watu katika kanisa, huongozwa na mawazo yao, na hawa mtafuti Mungu kwa ajili ya ushauri. Wameacha msingi wa imani. Baadhi ya makanisa hawafundishi Biblia. Hawaishi kwa kufuata mafundisho ya Biblia katika maisha yao. Na kama hawaishi kwa kufuata mafundisho ya Biblia katika maisha yao, je, kwa nini huwa wanatumia mafundisho hayo, wakati wa kuchagua viongozi? Baadhi ya makanisa, yameufuata ulimwengu sana, kwamba kinachoendelea katika chaguzi za kisiasa, kinaendelea pia katika chaguzi za kanisa. Wakati mwingine, kuna matumizi mabaya ya fedha, kampeni chafu, kujaribu kushawishi, na kuhonga watu ili wampigie kura mtu mmoja! Wazo la kumwomba Mungu, halipo.

Kuna watu wengine pia, katika kamati na sinodi, ambao siyo hata Wakristo! Hawana uhusiano binafsi na Mungu. Wanapotaka kuchagua viongozi wengine, haishangazi wanapochagua viongozi, ambao siyo Wakristo wa kweli. Hii inaweza kukushangaza – lakini katika Uingereza, kuna baadhi ya wachungaji, na maaskofu, katika kanisa la Anglikana, ambao hawaamini hata kwamba, Yesu alikufa na kufufuka tena! Je, hii inatokeaje? Kwa sababu wakati mwingine, watu walio wachagua kama viongozi, hawa ulizi maswali ya msingi, na wao wenyewe hawa amini injili kwa ukamilifu. Baadhi ya wachungaji hutaka kuwa viongozi kwa nia mbaya – na watu walio wachagua, hawa kuuliza maswali ya msingi.

Wakati mwingine, baraza au kamati, hutaka tu kuziba nafasi ya uongozi katika kanisa, na kwa hiyo wao hupokea na kushukuru tu kwa yelete, anayekuja na kusema anataku kuwa mchungaji. Wanashindwa kuangalia sifa za ndani, na wanawachagua kwa vyovoyete. Na kisha, kuna matatizo mengi. Baadhi ya wachungaji, wanafikiri: "Je, nitapata nini katika nafasi hii ya uongozi?", badala ya "jinsi gani nitawahudumia watu katika kanisa langu, na kuwaonesha Yesu"?

Wakati mwingine, kamati na mabaraza, yanajali zaidi kueneza nguvu ya dhehebu lao, badala ya kueneza habari njema ya Injili. Sababu nyingine kwamba kuna weza kuwa na ombwe la viongozi waadilifu, ni kwamba, kiongozi mpya anahitaji mfano mzuri wa kufuata. Wanahitaji kuona namna uongozi mzuri ukoje. Lakini, kama hawamjui kiongozi yelete mwadilifu – ni vigumu kwao kujifunza. Labda wale viongozi wachanga wanasesma: "Tuoneshe viongozi waadilifu" ili kwamba tujifunze kutoka kwao. Inasikitisha kanisa linaposhindwa kutoa mifano ya kufuata.

Haya yote yanaweza kusikika vibaya kwako. Unaweza hata kuniambia, ni kweli hali iko hivyo? Baadhi yenu mnawenza kukubali. Baadhi yenu mnawenza kukataa. Baadhi yenu mnawenza kuwa na uzoefu binafsi, kuhusu mambo haya, ambapo mmekutana nayo uso kwa uso. Labda, unaweza kuwa umesikia hadithi za wachungaji na viongozi, ambao hawa kuongoza kwa uadilifu. Sitashangaa kama mmesikia. Kumbuka, kitabu

hiki kiliandikwa na mtu, ambaye alikuwa katika uongozi wa kanisa kwa miaka **35!** Askofu Mtetemela, alichaguliwa kuwa Askofu kwa miaka **20**, na alikuwa Askofu mkuu kwa miaka **10**.

Je, hii inakuambia nini? Hapa ni mtu mwenye uzoefu mwingu! Amekuwa katika ngazi ya juu, na ameona matatizo haya mwenyewe. Hii ndiyo maana ni muhimu kusikiliza anachosema. Na ndiyo maana aliandika kitabu hiki. Aliguswa sana kuhusu ubora wa viongozi katika kanisa, kwamba alitaka kujaribu kusaidia kubadilisha hali hii. Kwa kweli, anasema katika utangulizi wake, kwamba moja ya malengo ya kitabu hiki, ni kuliamsha kanisa! Kwa hiyo, baada ya kipindi hiki cha pili, ni vizuri kutulia, na kutafakari, swali hili: je, sisi ni viongozi wanao toa mfano mzuri, katika makanisa yetu? Je, sisi ni viongozi waadilifu? Kama matokeo ya tulichosikia asubuhi hii, je, kuna kitu chochote unachohitaji kuchagua kwa ajili ya maisha yako? Je, kuna dhambi maalumu ambayo unahitaji kuitubu? Je, kuna eneo lolote katika huduma yako, ambalo unajua kwamba unahitaji uamusho na kufanya mambo sahihi? Ninatumaini kwamba, kufikia mwisho wa wiki hii, utakuwa na picha kamili, kuhusu nini maana ya kuwa kiongozi mwadilifu, na kwamba utavutiwa, na kuamua kuwa kiongozi wa namna hiyo. Mungu atupe nguvu ya kuwa kiongozi wa namna hiyo.

“NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU”. KIPINDI 3: Maadili ya Uadilifu ni nini?

Asubuhi ya leo, tulitambulisha kitabu hiki kwako: “*Nioneshe kiongozi mwadilifu*”. Tulijifunza machache kusushu mwandishi wa kitabu, na tulijifunza kwa nini, anafikiri kwamba somo hili ni muhimu sana, kwa kanisa leo. Tuliangalia changamoto, ambazo tunazo katika ulimwengu huu, na pia katika kanisa, katika maswala ya uongozi. Tuliona kwamba, kulikuwa na baadhi ya mifano mizuri ya uongozi, lakini pia, tuliona kwamba, kulikuwa na mifano mingi ya uongozi mbaya. Tuliona jinsi baadhi ya viongozi walivyochaguliwa, katika Biblia. Na tulimaliza kipindi, kwa kujaribu kuelewa, kwa nini leo kanisa, wakati mwagine, hufanya makossa, katika kuchagua viongozi. Na Askofu Mtetemela alisema kwamba, baadhi ya makanisa, na madhehebu, hupuuza ushauri wa kibiblia, kusuhu jinsi ya kuchagua viongozi.

Basi, katika kipindi hiki, ninataka tuelewe maana ya ‘*uadilifu*’ ni nini, ili kwamba tuwe na hakika kuhusu maana ya jambo hili. Na kisha, ninataka tuangalie aya chache, katika Agano Jipy, zinazotunesha kiongozi mwadilifu yukoje. Kwa kweli, aya ambazo tutaangalia zinaonesha sifa za viongozi, ambazo kanisa la mwanzo, walitumia katika kuchagua viongozi wao. Kwa hiyo – baadhi ya mambo tunayojifunza mchana huu, yapo katika sura **3** na **4**, katika kitabu hiki.

Ngoja tuangalie maneno haya mawili ‘*maadili*’ na ‘*uadilifu*’. Neno ‘*maadili*’ linahusu mkusanyiko wa kanuni, ambazo zinaweza kuwa nzuri, au mbaya; sahihi au siyo sahihi. Sana sana inahusu tabia, na imani. Kwa hiyo, ninaweza kusema kwamba, mtu ana maadili mazuri. Ana imani nzuri, na tabia nzuri pia. Kwa upande mwagine, ninaweza kumwelezea mtu fulani, kama mtu mwenye maadili mabaya. Hafanyi kinacho-kubaliwa kuwa kizuri, au sahihi. Anaenda katika tabia, ambayo siyo nzuri. Na kwa hiyo, katika jambo hili, ningesema anamaadili mabaya. Kama mtu fulani anasema: “*Askofu Mtetemela ni mtu wa maadili*”, inamaana kwamba, ni mtu mzuri – na siyo mtu mbaya.

Ni mtu anayeongozwa na kanuni nzuri, katika maisha yake, na kwa sababu ninajua kwamba ni Mkristo, ninajua kwamba kanuni zake zinatoka katika Biblia. Watu katika nchi wanaposema: “*tunataka Rais mwenye maadili*”, inamaana kwamba, wanataka mtu ambaye anatabia nzuri, na ana imani nzuri, na matendo mazuri. Mtu huyu anawenza kuwa hata siyo Mkristo, lakini bado anawenza kuwa na maadili mazuri. Kwa hiyo, neno ‘*maadili*’, linamaana ya wema, au uaminifu, na kinyume cha neno hili ‘*maadili*’ ni kukosa maadili.

Je, vipi kuhusu neno hili ‘*uadilifu*’? Lina maana gani? Nimewahi kusikia viongozi wengi, wakitumia ufanuzi huu: “*Uadilifu ni kufanya jambo linalo-takiwa, bila kuangaliwa na mtu mwagine*”. Inahusu kuwa mkweli kwako mwenyewe. Inahusu mtu yule yule, unapokuwa peke yako, na mbele za watu. Kwa hiyo, kama mchungaji anasema kwa watu, katika kanisa lake siku ya Jumapili: “*Mimi siku zote nimwaminifu kwa mke wangu*”, lakini, baadaye siku ya Jumatatu, anaonekana kwenye hoteli, akiwa na mwanamke mwagine, unawenza kusema kwamba, mtu huyu hana uadilifu.

Maneno yake haya fanani na matendo yake. Maneno yake yanasesma kitu fulani, lakini matendo yake, yanasesma kitu kingine. Hicho ni kinyume cha uadilifu. Mtu mwenye uadilifu hutenda vile vile, hata unapokuwa anaangaliwa na watu **100** katika kanisa, au anapokuwa peke yake, katika nyumba yake.

Hapatakuwa na tofauti katika tabia yake. Hapa kuna nukuu nyingine maarufu: “*Viongozi wenyе uadilifu, hutembea katika kauli zao*”. Je, hii inamaana gani? Inamaanisha kile kile, ambacho nimikuwa nikisema. Mtu huyu hufanya alichosema atafanya. Matendo yake haya pingani na maneno yake.

Kwa kweli, Biblia ina neno kwa mtu, anaye sema jambo moja, lakini akafanya jambo jingine. Ni neno ‘unafiki’. Yesu alitumia sana neno hili, alipokuwa akizungumza kuhusu viongozi wa dini. Katika **Mathayo 23** anawaambia neno hili mara **6**. “*Ole wenu, walimu wa sheria, na mafarisayo, ninyi wanafiki!*”! Anatumia lugha kali sana! Anahasira sana na viongozi hawa, kwa kuwa wamekosa uadilifu. Katika **Mathayo 23:3** Yesu anawaonya watu, na wanafunzi wake, kuhusu mafarisayo. Anasema hivi: “*Msifanye wanachofanya, kwa kuwa hawafanyi wanacho hubiri*”. Walisema kitu fulani, kisha wakafanya kinyume chake. Walihubiri mahubiri wakiwaambia watu jinsi ya kuishi na kutenda, lakini wao wenye hawakufanya hivyo katika maisha yao.

Walikuwa wanafiki. Walikuwa watu wasio na uadilifu. Watu walio jaa uadilifu, na tabia nzuri, wanaaminika. Ni waminifu, na wamejaa kweli. Matendo yao yanafanana na maneno yao. Wakisema watafanya kitu fulani, kisha watafanya hivyo kweli. Na kiongozi aliye-jaa uadilifu, anaweza kuaminiwa kwamba atatunza ahadi, na hatakuangusha. Kwa upande mwingine, mtu asiye na uadilifu, hawezi kuaminiwa, na mara kwa mara, huwaangusha watu, kwa sababu anaweza kusema kitu fulani kwako, na kisha, ukiondoka anaweza kufanya kinyume chake kabisa. Na kuwa na kiongozi, asiye na uadilifu mara zote husababisha matatizo. Hauwezi kumwamini. Kwa hiyo, neno ‘uadilifu’ na ‘kuaminiwa’ yanaenda pamoja.

Hebu sikiliza nukuu hii: “*Mtu mwenye akili nyingi, husifiwa. Watu wenyе utajiri mwingi, huonewa vivu. Watu wenyе mamlaka, huogopwa, lakini watu wenyе uadilifu pekee, wanaamininiwa*”. Nina maswali machache kwako: Je, wewe ni mtu mwenye maadili, au ni mtu asiye na maadili? Je, huwa unatabia hiyo hiyo popote ulipo? Ukiwa nyumbani, mtaani, au katika mimbari – je, huwa unabaki na maadili yale yale? Je, huwa unatenda yale unayohubiri? Je, unaaminika katika tabia yako? Je, ni mwaminifu na mkweli? Maswali haya yote, yanaweza kuwekwa katika swali moja: “*Je, wewe ni kiongozi mwadilifu?*”

Asubuhi ya leo, tuliangalia mifano michache katika Biblia. Tuliona kwamba, hapakuwa na watu wengi, waliokuwa na uadilifu. Kwa kweli, tuliona viongozi, makuhani, na wafalme, ambao hawakuwa na uadilifu wowote. Na ilimfanya Mungu ahuzunike, na kukasirika sana. Kumbuka, alikuwa amewaleta watu Waisraeli, katika Nchi ya Ahadi. Aliwapenda, na aliwajali, na aliwapa mahitaji yao. Lakini bado, walichagua kuacha kumtii, na walimuasi kwa kufuata njia zao wenye. Walichagua kumpuuza Mungu. Lakini ukiwaangalia baadhi ya viongozi walio kuwa nao, haishangazi kuona kwamba, watu pia walimuasi Mungu. Inakufanya utambue, jinsi kiongozi alivyo muhimu katikati ya watu wake. Nilikuwa ninasoma Kitabu cha Wafalme, katika Agano la Kale. Nilitaka kuhesabu na kuona ni viongozi wangapi mionganoni mwao walikuwa waadilifu.

Tunajua kwamba, Ufalme wa Israeli, ulikuwa umeungana chini ya watu **3**, kwa kipindi cha miaka **120**: Sauli, Daudi na Solomoni – na kila mmoja wa hawa wafalme, alitawala kwa miaka **40**. Tunajua kwamba, Daudi alikuwa mfalme mzuri. Alimfuata Mungu na alitawala kwa uadilifu, ingawa alifanya makosa machache. Wote Sauli na Solomoni, walianza vizuri – lakini wakamaliza vibaya. Lakini Solomoni alipokufa, nini kilitokea? Ufalme wa Israeli, uligawanyika sehemu mbili, na kulikuwa na vita vya wenye hivyo wenye. Kulikuwa na Ufalme wa Wayuda, katika upande wa kusini, na Ufalme wa Israeli, katika upande wa kaskazini, na kila ufalme ulikuwa na mfalme wake. Kwa zaidi ya miaka **350** – kulikuwa na wafalme **40** tofauti, ambao walitawala falme hizi mbili. Wafalme ishirini katika Yuda, na Wafalme ishirini katika Israeli.

Unaposoma aya hizi katika Wafalme wa kwanza, na wapili, zinakuambia ni muda gani kila mfalme alitawala, na lini walianza kutawala. Mmoja wa wafalme hao, alitawala kwa miaka **55**; huyu ni mtu mbaya aliyeitwa Manase. Mmoja wa wafalme hao, alitawala kwa siku **7** tu! Huyu ni mtu aliyeitwa Zimri. Lakini pia – utaona wangapi katii yao, walikuwa viongozi waadilifu. Neno ambalo limetumika kuelezea tabia za kila mmoja wafalme hawa, ni ‘mema’ au ‘mabaya’; ‘sahih’ au ‘siyo sahih’. Kwa mfano: Kulikuwa na mfalme aliyeitwa Yosia, na kwa kweli, alikuwa mfalme akiwa katika umri wa miaka **8** tu! **Wafalme wa pili: sura 22**, inasema hivi: “*Alifanya yaliyo mema mbele za macho ya Bwana*”. Lakini inasikitisha kwamba, hatuoni maneno haya, mara kwa mara, katika vitabu hivi viwili.

Tumeambiwa katika **Wafalme wa kwanza 26:25** kwamba: “*Omri alifanya maovu mbele za macho ya Bwana, na alifanya dhambi kuliko watu wote waliomtangulia*”. Hakuwa mtu mwadilifu. Na inasikitisha kwamba, kadri unaposoma aya hizi, utaona kwamba mfalme aliyeitwa, alifanya maovu zaidi kuliko mfalme aliyeitwa. Na kwa hiyo, mara nyingi utasoma maneno haya: “*mfalme huyu akafanya maovu*”; “*mfalme huyu akafanya maovu*”; “*mfalme huyu akafanya maovu*”. Inakatisha tamaa! Na kwa matokea ya viongozi wengi wabaya, watu pia waliongozwa katika uovu, na kuwa watu wasio waadilifu.

Tumeambiwa hii, katika **Wafalme wa kwanza 15:26**: Nadabu, mfalme wa Israeli, “*akafanya maovu mbele ya macho ya Bwana, na kwa sababu na dhambi yake, akasababisha Israeli watende dhambi*”. Mara kwa mara tena, Israeli na Yuda, walikuwa na wafalme ambao hawakuwa waadilfu. Na ndio maana Ufalme wa Israeli, uliharibiwa na majeshi ya Ashuru. Na Ufalme wa Yuda, uliharibiwa na majeshi ya Babeli. Hapa ni swali: Je, unafikiri ni wangapi kati ya wafalme hawa **40**, walikuwa viongozi waadilifu? **8** tu!

Wengine **32** wote, wameelezwa kama waovu, na inavutia kuona kwamba, wale wafalme **8** waadilifu wote, walitoka katika Ufalme wa Yuda. Kati ya wafalme **20** wa Israeli, hakuwepo hata mmoja aliyekuwa mwadilfu! “*Nioneshe kiongozi mwadilifu!*” Na katika Israeli, kwa zaidi ya miaka **350**, usingeona kiongozi mwadilifu hata mmoja! Hii ndio hali katika vipindi vingi, ndani ya Agano la Kale. Kulikuwa na viongozi wengi, ambao hawakuwa waadilifu; watu wasiyo mfuata Mungu.

Katika kitabu chake, Askofu Mtetemela anataja mambo **6**, ambayo anafikiri kwamba yanasaidia kueleza kuhusu uadilifu. Lakini, nitataja mambo **2** tu kati ya hayo, kwa sababu nafikiri kwamba, tayari tumekwisha taja yale ma-nne. **Namba 1:** Tambua kwamba Mungu ni mwanzo wa maadili. Mungi ni mtakatifu, na hakuna uovu ndani yake. Yeye ni mwanzo wa kweli yote. Sikiliza maneno ya **Kumbukumbu la Torati 32:4**: “*Yeye ni mwamba. Njia zake ni takatifu, na njia zake zote ni za haki . Yeye ni Mungu mwaminifu, ambaye hafanyi maovu, mkamilifu na mwenye haki ni yeye*”. Hii inaelezea maadili. Utakatifu, haki, waminifu, ukamilifu, mtu asiye fanya maovu. Ahadi zake zote, ni za kuaminika na kuaminipa – ni mfano kamili wa uadilifu. Na hii ndio maana, mwanamume au mwanamke, ambaye anamwabudu Mungu, atakuwa kiongozi anayetenda kama yeye. Hii ndio maana watu, wanataka kuona viongozi wanao mwabudu Mungu.

Namba 2: Mtu mwadilifu pia, anauwezo wa kuona tofauti kati ya wema, na uovu. Kuna maombi ya ajabu, katika **Wafalme wa kwanza, sura 3**. Solomoni tayari ni mfalme, na anakwenda sehemu inayoitwa Gibeon, kutoa sadaka kwa Mungu. Wakati wa usiku, Mungu anamtokea Solomoni katika ndoto, na Mungu akamwambia: “*Omba chochote unachotaka na nitakupa*”. Wow! Ni ukaribisho ulioje huu! Hebu piga picha, kama Mungu angekutokea katika ndoto, na kukwambia ujumbe huu huu: “*Omba chochote unachotaka na nitakupa*”. Je, ungeomba nini? Ninafikiri kwamba jibu lako lingeonesha kama wewe ni kiongozi mwadilifu, au hapana! Je, Solomoni anasema nini katika jibu lake? Kwanza kabisa, katika **Wafalme wa kwanza 3:6** anasema kuhusu baba yake, Daudi. Alisema hivi: “*Umeonesha ukarim mwingi kwa mtumishi wako Daudi kwa sababu alikuwa mwaminifu kwako, na mtakatifu na mkamilifu katika moyo wake*”.

Haya ni maelezo yanayohusu mtu mwadilifu. Lakini, hebu sikiliza maneno ya Solomoni katika mstari **9**: “*Nipe moyo wa hekima, ili niweze kuwaongoza watu wako, na niweze kuona tofauti kati ya wema na uovu*”. Huu ni uadilifu! Solomoni, anatambua kwamba, kazi ya kuwa mfalme ni kubwa sana, na anajua kwamba anahitaji msaada. Hafikiri kuhusu mwenyewe, anafikiri kuhusu watu anao-waongoza. Angeweza kusema: ‘*nipe pesa nydingi*’. Angeweza kusema: ‘*nipe maisha marefu*’. Angeweza kusema: ‘*unaweza kupanga adui zanagu wafe*’. Lakini hakufanya hivyo. Aliomba hekima na moyo wa utambuzi, ili kwamba awaongoze watu vizuri. Alimwomba Mungu amsaidie kuona tofauti kati ya wema na uovu, ili kwamba aongoze kwa haki na usawa. Hii ni alama ya mtu mwadilifu. Na tumeambiwa kwamba Mungu alipendezwa na Solomoni, na akajibu ombi lake.

Nina swali: Je, kama kiongozi huwa - ninaomba sala ya Solomoni? “*Baba Mungu, nipe moyo wa hekima, ili niweze kuwaongoza watu wako, na niweze kuona tofauti kati ya wema na uovu*”. Ninafikiri kwamba, kila mchungaji na mwinjilisti, anapaswa kuomba sala hii kila siku!

Tunahitaji kutambua kwamba, kama viongozi, tunahitaji msaada kutoka kwa Mungu – kwa sababu hatuwezi kufanya kazi wenyewe. Kama tunataka kuwa viongozi waadilifu, tunahitaji kategemea msaada wa Bwana, na tunapaswa kufuata mfano wa Mungu Baba, na Mungu Mwana. Kadri tunavyojifunza Biblia, tunajifunza kuhusu tabia ya Mungu. Kadri tunavyojifunza zaidi kuhusu Yesu, tunajifunza kwamba, yeye ni mfano kamili wa uongozi wa maadili. Hatupaswi kuondoa macho yetu kwake – kwa sababu, tunapomtazama yeye, tunaanza kuelewa nini, maana ya uongozi wenye maadili ya kweli. Hatupaswi kuondoa macho yetu kwake.

Nimekumbushwa juu ya mistari **4** katika Agano Jipy: **Waefeso 5:1**: “*Muwe wenyewe kumwiga Mungu*”. Kama tunavyosoma Neno la Mungu, na kujifunza kuhusu yeye, tunatiwa moyo kufuata tabia yake. **Wafilipi 2:5**: “*Nia yenu iwe kama ile ile ya Yesu Kristo*”. Tunapoishi maisha yetu; tunapofanya majikumu yetu, je, tunapaswa kumuata nani? Tunapaswa kuwa kama Yesu. **Waebriania 12:2**: “*Tuelekeze macho yetu kwa Yesu, mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu*”. Tunahitaji kuendelea kumwangalia Yesu. Kutakuwa na uharibifu, na majoribu ya mara kwa mara, kama tutaacha kumwangalia Kristo, na kutazama mambo mengine - lakini ni pale tu tunapomwangalia Yesu, na kufuata mfano wake, ndipo tutaweza kusonga mbele kama viongozi.

Je, unakumbuka nini kilimtokea Petro, alipotembea juu ya maji ya ziwa Galilaya? **Mathayo 28**. Yesu alimwita Petro atembee juu ya maji – na alifanya hivyo! Ulikuwa muujiza. Tumeambiwa kwamba: “*Petro alishuka kwenye mtumbwi, akatembea juu ya maji, na kwenda mbele kwa Yesu*”. Kumbe! Je, watu wangapi wamewahi kufanya hivyo?! Ni Yesu na Petro tu. Lakini nini kilitokea baadaye? Alianza kuondoa macho yake kwa Yesu, na badala yake, akaangalia kwingine katika mawimbi, na upepo. Alichanganywa na macho yake yakaacha kumtazama Yesu, na akaanza kuzama.

Kwa jinsi hii hii, kama viongozi katika kanisa, unapoacha kutazama mfano wa Yesu, utaanza kuzama. Na unapoanza kuzama, na kanisa lako pia, linaanza kuzama. Hebu tuelekeze macho yetu kwa Yesu. Hebu tumtazame yeze kama mfano wetu, kwa sababu kadri tunavyo mtazama yeze, ndivyo tunavyokuwa kama yeze.

Wakati mwingine, ninaposoma Biblia yangu, ninaona kwamba, ninawivu zidi ya wanafunzi wa Yesu! Unaweza kupata picha, ilikuwa jambo namna gani kuwa kama watu hao? Kila siku, kwa miaka 3, walikuwa pamoja na Yesu. Walitumia muda kwa kuwa pamoja naye. Walimsikiliza akifundisha. Walimsikia akiomba. Walimtzama akiponya watu wengi. Walimuona jinsi alivyo itikia zidi ya adui zake. Waliona jinsi alivyoishi maisha yake. Walijifunza mambo mengi sana kutoka kwake. Alikuwa mfano waajabu sana kwao. Kuna wakati ambapo hawakuelewa alichokuwa anawafundisha, lakini baadaye, Roho Mtakatifu alipokuja juu yao, walikumbuka maneno yake, na matendo yake, na wakaelewa.

Katika **Yohana 13**, Yesu alipoosha miguu ya wanafunzi wake, aliwaambia hivi: “*Nimewapa mfano – mnapaswa kufanya kama nilivyofanya kwa ajili yenu*”. Alitaka waone mfumo wa maisha yake; alitaka wajifunze kutoka kwake. Hakuwa na maana kwamba, waoshane miguu siku zote, lakini mfano aliotaka kuwapa, ulikuwa na maana kwamba, walipaswa kuwatumikia wengine. Huu ndiyo mfano aliowapa. Je, Yesu alisema nini? “*Nimekuja kutumika, na siyo kutumikiwa*”. Hili ni somo kubwa kwetu, siyo? Na kesho, tutakuwa tunaangalia aya hii kwa undani. Yesu ni mfano wetu; yeze ndiye mtu tunayepaswa kujifunza kwake, na yeze ndiye tunayepaswa kumwiga, kama tunataka kuwa viongozi waadilifu.

Basi, tumeangalia maana ya kuwa na maadili. Tumeangalia maana ya kuwa viongozi waadilfu. Tuliona kwamba, katika Agano la Kale, viongozi waadilifu, walikuwa wachache sana - kulikuwa na wafalme **8** tu, katy ya **40**, ambao waliongoza kwa uadilifu. Pia tuliona kwamba, katika Agano Jipy, wengi wa viongozi wadini hawakuwa waadilifu. Yesu aliwarejea kama wanafiki. Na tayari tumeona kwamba, mfano tunaopaswa kufuata ni Kristo Yesu. Kama tunataka kuwa viongozi waadilifu, lazima tuelekeze macho yetu kwa Yesu, na kufuata mfano wake – na hivi ndivyo inavyosema sura **3**, katika kitabu hiki.

“NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU”: KIPINDI 4: **Sifa za kiongozi mwadilifu na sifa za kiongozi katika kanisa la mwanzo.**

Katika kipindi hiki, na katika vipindi vyetu vyote vya kesho, ninataka tuangalie juu ya sifa za kiongozi mzuri wa kanisa. Kama tunataka kujua ikiwa mtu fulani ni mwadilifu, je, ni sifa gani tunapaswa kuangalia katika tabia yake? Je, ni kwa namna gani kiongozi anaweza kuthibitisha kwamba ni mwadilifu? Je, tunawezaje kutambua yupi ni mchungaji mzuri, au mwinjilisti mzuri? Je, wanapaswa kuwa watu wa aina gani? Hili ni somo, ambalo Askofu Mtetemela anafundisha katika sura **4**, ya kitabu hiki.

Katika kanisa la Agano Jipy, wakati walipozingatia nani angeongoza kanisa, ninahakika wangeuliza swali hili: je, wanazaa tunda la Roho katika maisha yao? Je, tunda lao likoje? Na shangaa kama swali hili huwa linalizwa leo, wakati wa kuchagua viongozi? Lakini tunajua kutoka kwa barua za Paulo kwamba, sifa zingine zilihitajika pia. Kulikuwa na miongozo na kanuni kwa ajili ya kuteuwa viongozi, katika kanisa la mwanzo. Mitume walipokutana kufanya usaili wa viongozi, walijotarajiwu kuchaguliwa, walitumia sifa hii, kupima kama mtu fulani alikuwa anafaa, kwa ajili ya kazi ya kuwa kiongozi katika kanisa.

Unaweza kukumbuka – Paulo aliandika barua kwa Tito. Walikuwa wamepanda makanisa kadha, katika kisiwa cha Crete, huko Ulaya. Paulo ameondoka kisiwani – lakini alimtaka Tito acae huko, na kusaidia kusimamia makanisa mapya. Alimtaka achague viongozi katika makanisa hayo – na kisha, alimpa orodha. Alisema, watu unao wachagua lazima wawe na sifa hizi, na kisha anataja sifa **17**, ambazo kiongozi

anapaswa kuwa nazo. Kwa hiyo, ngoja tufungue barua hii, na tusome kuhusu sifa hizi. **Tito 1:6-9***. Na unaposikiliza ujumbe wa mistari hii, nataka ujiulize mwenye swalii hili: je, hii inani-zungumzia mimi?

Hii ni orodha ndefu! Na hizi ni sifa za juu! Tunaweza hata kufikiri kwamba, ni sifa za kiwango cha juu mno. Tunaweza hata kujuliza, je, kuna mtu ye yote anaye weza kuwa kiongozi, kama ni lazima kuwa na sifa hizi zote! Kwa nini Paulo anaweka sifa za kiwango cha juu hivyo? Angalia mstari **7**, kwa sababu ninafikiri kwamba, tunaweza kupata jibu hapo. Kwa nini sifa ziko juu sana? Ni kwa sababu “*kiongozi wa kanisa ni mwangalizi wa kazi ya Mungu*”. Unapofikiri kuhusu jambo hili – kwamba ni wajibu mkubwa. Kama wewe ni kiongozi katika kanisa – unafanya kazi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu! Unamwakilisha Mungu kwa watu wengine. Na kwa hiyo, inahitaji uwe kiongozi, mwenye sifa za kiwango cha juu.

Unapaswa kuwa kiongozi mwadilifu. Unapaswa kuwa mtu anayetafuta kuishi kwa ajili ya Mungu, na mtu ambaye kila siku, anatafuta kumwiga Yesu. Na kama kiongozi wa kanisa, unatarajiwa kuwa-shawishi wengine. Unatarajiwa kuweka mfano bora – ili kwamba wengine waweze kukufuata. Tabia yako, na mwenendo wako, unapaswa kuwaelekeza watu wengine kwa Mungu. Watu katika kanisa lako, wanapaswa kuwa na uwezo wa kumwona Yesu Kristo ndani yako. Kiwango ambacho Paulo anaweka ni cha juu – lakini kumbuka, kazi yako ni kwa Bwana Mungu, na yeye ni mtu, ambaye viwango vyake ni vya juu sana.

Katika mistari hii **4**, katika **Tito 1**, ninafikiri kwamba, kuna vigezo **17**, ingawa baadhi ya vigezo vinafanana. Baadhi ya vigezo havihitaji ufanuzi wowote, kwa sababu maana yake iko wazi. Lakini baadhi ya vigezo vinahitaji ufanuzi, na kwa hiyo, kwa dakika chache, tutaangalia sifa hizo pamoja. Lakini, kabla ya kufanya hivyo, nataka pia tusome aya nyininge, kuhusu sifa anazopaswa kuwa nazo kiongozi wa kanisa. Fungua katika **1 Timotheo 3**, na tutasoma mstari **1-13***. Na tena, tunaposoma mistari hii, nataka ujiulize mwenyewe swalii lile lile: Je, mistari hii inani-elezea mimi? Labda tungweza pia kujuliza wenyewe swalii jingine. Kama ungefanyiwa usaili na mitume, kwa ajili ya kuwa kiongozi wa kanisa - na kama wangekuwa wanatumia vigezo hivi, je, unafikiri kwamba wangekupa kazi? Kwa maneno mengine, ungeweza kufauru mtihani huu?

Labda, umegundua kwamba baadhi ya sifa zilizotajwa katika Timotheo ya kwanza, ni zile zile ambazo zimetajwa, katika **Tito 1**. Kwa mfano: Kiongozi lazima awe asiye na lawama, mkaribi-shaji, siyo mgomvi, siyo mlevi. Lazima awe na kiasi, na awe na mke mmoja tu. Sifa hizi zimetajwa katika aya zote. Lakini, kuna sifa **3** zaidi, ambazo zimetajwa katika **1 Timotheo** na hazipo katika Tito. **Namba 1**: Kiongozi anapaswa kuwa na ushuhuda mzuri kwa watu wasio Wakristo. **Namba 2**: Kiongozi lazima awe na uwezo wa kufundisha Neno la Mungu. **Namba 3**: Kiongozi lazima awe amekomaa katika imani. Kwa maneno mengine, asiwe Mkristo aliyeamini karibuni. Kwa hiyo, baada ya kusoma aya hizi mbili, kuna angalua sifa **20** tofauti, ambazo kiongozi wa Kikristo anapaswa kuwa nazo. Na sasa ninataka tuangalie kwa undani baadhi ya sifa hizo.

Nimegundua katika Biblia ya Kiswahili ya toleo la Union, na Kiswahili cha Biblia ya Habari Njema, maneno ‘askofu’ na ‘mzee’ yanetumika katika aya hizi. Lakini, tafadhalii usifikiri kwamba, aya hizi zinawahusu viongozi, ambao ni wazee tu, au viongozi ambao ni maaskofu tu. Aya hizi hazi-mhusu Askofu Mtetemela au Askofu Salala tu! Neno ambalo limetumika katika lugha ya Kigiriki, linahusu pia wazee, maaskofu, viongozi wa kanisa, na wachungaji. Na watu hawa wajibu wao, ni kuangalia afya ya kiroho ya kanisa – na ndiyo maana, Paulo anasema kwamba, lazima wawe na uwezo wa kufundisha Neno la Mungu.

Katika **1 Timotheo 3:8-13** Paulo pia anarejea aina nyininge ya kiongozi katika kanisa; kiongozi ambaye siyo mzee au mchungaji. Katika toleo la Biblia ya Union, wameitwa ‘*mashemasi*’, na katika toleo la Habari Njema, wameitwa ‘*wasaidizi*’ wa kanisa, au watumishi. Hawa ni watu, ambao wajibu wao hauhusu huduma za kiroho katika kanisa. Watu kama – wahasibu, na katibu, wanaweza kuitwa wasaidizi wa kanisa. Lakini tambua – wanahitaji sifa zile zile, kama za mzee wa kanisa, isopokuwa wao, hawahitaji kuwa na karama ya kufundisha Neno la Mungu katika kanisa. Kwa hiyo, ngoja niweke wazi hapa. Mchungaji ,na Askofu, anapaswa kuwa na uwezo wa kufundisha Neno la Mungu. Hivi ndivyo unavyosema mstari **2**, katika **1 Timotheo 3**.

Je, hii inamaana gani? Inamaana kwamba, mchungaji lazima aamini Biblia. Inamaana kwamba, mchungaji lazima ajue Biblia. Anapaswa kuwa mwanafunzi wa Neno la Mungu. Na lazima aweze kufundisha ukweli wa Biblia kwa wengine. Je, unaijua Biblia yako? Je, huwa unatumia muda kusoma na kujifunza Biblia? Je, huwa unaitumia katika kazi yako? Hili linaweza kusikika kama swali la kipuuzi kuulizwa katika kundi la wachungaji! Lakini, kuna baadhi ya wachungaji, ambao huwa hawatumii muda mwingu katika Biblia. Katika sura **3**, ya kitabu hiki, Askofu Mtetemela anasema hivi: “*hatari moja iliyopo leo ni kwamba, baadhi ya wachungaji hawahubiri neno la Mungu kwa uaminifu*”. Kumbuka, huyu anayeongea hapa ni Askofu Mkuu. Ni mtu mwenye usoefu mwingu, katika kazi za kichungaji, na jambo hili ndilo ameliona kwa miaka **35**, katika uchungaji wake. Anasema: “*baadhi ya wachungaji hawahubiri Neno la Mungu kwa uaminifu*”. Hili ni tatizo

kubwa katika kanisa leo. Wachungaji lazima wawe na uwezo wa kufundisha kweli kutoka katika Neno la Mungu – la sivyo afya ya kanisa itaanguka.

Tambua pia, kwamba katika aya hizo zote, zinasema mchungaji lazima ‘*asiwe na lawama*’. Hii inamaana gani hasa? Kwa sababu, baadhi ya watu wanaposoma mstari huu, hufikiri kwamba, mchungaji anapaswa kuwa mkamilifu, na asiye na dhambi! Na sote tunajua kwamba, wachungaji siyo wakamilifu! Ni kama watu wengine katika kanisa, ni watu wanao tenda dhambi. Kwa hiyo, maneno ‘*asiye na lawama*’, hayana maana ya kwamba ‘*asiye tenda dhambi*’. Kama yangekuwa na maana hiyo, hakuna hata mmoja ambaye angeweza kuwa kiongozi – isipokuwa Yesu mwenyewe, kwa sababu hakuna binadamu asiye tenda dhambi. Neno la Kigriki ambalo Paulo anatumia hapa, kutuonesha kwamba mtu asiye na lawama, ni mtu ambaye, “*hatuhumiwi kwa makosa*”. Inahusu ushuhuda.

Hebu jaribu kupata picha, kama Askofu angekuwa anachagua kiongozi mpya. Askofu aliyeamua kuitisha mukutano mkubwa. Amemwalika kila mtu, anayemjua mtu anayetarajia kuchaguliwa. Watu kutoka kanisa hilo wamekuja. Watu kutoka familia yake wamekuja. Watu kutoka mji wake wamekuja. Kuna watu wengi mahali hapo. Na kisha, Askofu anasimama, na kusema kwa watu hawa wote: “*Je, unaweza kuleta tuhuma yoyote zidi ya mtu huyu? Je, amewahi kufanya jambo baya, katika kanisa, au jamii?* *Je, unaweza kusema jambo lolote baya, kuhusu tabia ya mtu huyu?*” Kama hakuna mtu ambaye angeweza kusema jambo lolote baya, kuhusu huyu mtu – basi angekuwa mtu ‘*asiye na lawama*’. Asinge-laumiwa kwa jambo lolote baya. Ushuhuda wake ungekuwa safi sana. Hii ndiyo maana ya maneno ‘*asiye na lawama*’, katika aya hii.

Aya hizi zote zinataja ndoa, na umuhimu wa uhusiano katika familia. Paulo anasema katika **Tito 1:6**, kwamba mchungaji “*anapaswa kuwa na mke mmoja tu*”. Sasa, inaonekana rahisi kuelewa, lakini nadhani watu wengi, wamefikia hitimisho, ambalo siyo sahihi kuhusu mstari huu. Mimi nafikiri mstari huu, unamaana hii. Mstari huu unahu – Askofu, na mchungaji, na mwinjilisti - aliyeoa. Hawezi kuwa na wake wawili au watatu, na lazima awe mwaminifu kwa mke wake. Kwa kweli, kama unaangalia katika neno la Kigriki, Paulo anamaanisha kwamba: “*lazima awe mwanamume wa mwanamke mmoja*”. Kwa maneno mengine, lazima awe amejitoa kwa mke mmoja, na kwamba mwanamke huyo ni mke wake. Haipaswi kuwepo wanawake wengine, katika maisha yake. Hii inamaana kwamba, kama mtu anataka kuwa kiongozi, na anajulikana kwamba yeze siyo mwaminifu kwa mke wake, hapaswi kuruhuswa kuwa kiongozi katika kanisa. Jambo hili liko wazi sana, katika mstari huu.

Pia ninafikiri kwamba, kama mchungaji au mwinjilisti atapatikana na kosa la kukosa uaminifu katika ndoa, na kuna ushahidi kwamba amekuwa siyo mkweli kwa mke wake, basi anapaswa kuondolewa katika nafasi yake ya uongozi katika kanisa. Anahitaji kupewa nidhamu. Mchungaji aliyeoa anapaswa kuwa mwaminifu kwa mke wake. Lakini ngoja pia, nikuambie ambacho mstari huu housemi. Paulo hasemi kwamba, wachungaji wote wanahitaji kuo. Nitasema tena: Paulo hasemi kwamba, wachungaji wote wanahitaji kuo. Anasema kwamba, kama mchungaji ameo, anahitaji kuwa mwaminifu kwa mke wake. Paulo alipoandika barua hizi, hakuwa ameo! Na bado, alikuwa mmoja wa mitume, na mmoja wa viongozi wa juu, katika kanisa! Kwa hiyo, haiwezi kuwa na maana kwamba, mchungaji anapaswa kuwa ameo - la sivyo Paulo asingekuwa nasifa za kuwa kiongozi! Pia Tito asingeweza, kwa sababu wasomi wengi, wanakubaliana kwamba, hakuwa ameo pia!

Kama utasema kwamba, mstari huu unamaana ya kwamba, mchungaji anapaswa kuwa ameo, pia, utakuwa unasema kwamba, anapaswa kuwa na watoto! Angalia tena **Tito 1:6**: “*Mchungaji anapaswa kuwa mtu asiye na lawama; anapaswa kuwa na mke mmoja tu, na watoto wake lazima wawe waumini*”.

Paulo anamwambia mtu fulani, ambaye anataka kuwa kiongozi, kama una watoto, lazima wawe waumini pia, na wawe na tabia njema. Hasemi kwamba, kama unataka kuwa mchungaji, inakupaswa uwe na watoto! Hapana. Kuna mengi ambayo ningeweza kusema kuhusu jambo hili, lakini ninafikiri kwamba, jambo la muhimu kukumbuka, ni kwamba, moja ya sifa za uongozi katika kanisa, ni kwamba, mchungaji anapaswa kuwa mwaminifu kwa mke wake, kama ameo.

Aya hizi zote zinasema kwamba, mchungaji hapaswi kuwa mgonvi – badala yake anapaswa kuwa mpole. Lakini, hata kanisani kuna watu, ambao hawawezi kuzuia hasira zao, na wanapenda kuwa wagonvi, kwa mikono yao, na pia kwa maneno yao. Hakuna nafasi ya kuwa mchungaji kwa mtu, anayepiga mke wake. Hakuna nafasi ya mchungaji, anayependa kupigana. Paulo anasema: mchungaji hapaswi kuwa mgonvi.

Hadithi kutoka Bethlehemu:

Kwa kweli, unapoangalia katika aya hizi mbili, ambazo tumekuwa tukijifunza, utaona kwamba makuhani hawa katika Bethlehemu, wameshindwa katika mambo mengi! Hawakuwa na kiasi. Hawakuwa wapole. Walikuwa wakorofi. Hawakuwa na ushuhuda mzuri. Hawakuwa watu wasiyo na lawama. Hawakupenda mambo mema, na hawakuwa watakatifu, au wenye nidhamu. Kwa kuhitimisha, tunaweza kusema kwamba, walikosa sifa nyingi anazopaswa kuwa nazo kiongozi. Hawakuwa viongozi waadilifu!

Kuna sifa nyingine ambayo nataka tuangalie kabla ya kumaliza, na hili ni jambo la uaminifu. **Tito 1:7**, inasema kwamba, kiongozi wa kiroho: “*asiwe mpanda mapato ya aibu*”. Maneno haya haya, yametumika kuwalhusu mashemasi katika **1 Timotheo 3:8** – na neno ‘*mwaminifu*’ pia limetumika. Toleo la Habari Njema, linasema hivi: “*Awe mwaminifu katika mambo yote*”. Ni muhimu sana, kwa mchungaji kuwa mtu mkweli. Unapaswa kuwa na ushuhuda mzuri kwa kuwa mwaminifu. Inasikitisha kwamba, kumekuwa na uharibifu mwangi katika kanisa leo, ambao umesababishwa na kukosekana kwa uaminifu na ukweli. Paulo ni muwazi sana kuhushu jambo hili, anapoandika barua yake kwa kanisa la Efeso. **Waefeso 4:25**: “*Acheni kusema uongo. Kila mmoja wenu anapaswa kusema ukweli, kwa sababu sisi sote ni mwili mmoja*”.

Askofu Mtetemela anarejea jambo hili la ukweli, na uaminifu katika kitabu chake. Anatukumbusha kwamba, huko nyuma mwaka **1962**, wakati misingi ya taifa ilipoanzishwa, **Mwalimu Nyerere** aliona umuhimu wa sifa hii. Alisisitiza kwamba, inapaswa kuingizwa, katika katiba ya Chama cha TANU, ambacho kilikuwa chama tawala kwa wakati huo. Moja ya viapo katika katiba kilisema hivi: “*Nitasema ukweli daima: utengano kwangu litakuwa jambo lisilo kubalika*”. Na kila mjjumbe wa chama, alipaswa kusema kiapo hiki, na kuweka ahadi ya kusema kweli. Nyerere alifikiri kwamba, kuwa na uaminifu na ukweli, katika tabia yako, ilikuwa njia nzuri ya kujenga uadilifu, katika jamii ya Tanzania. Rais wa tatu, baada ya Nyerere, **Benjamin Mkapa**, pia aliendelea kuamini hivyo. Aliwasihii Watanzania kufanya kweli kuwa msingi katika huduma zao. Alisema hivi: “*sema kweli, na uwe na tabia ya uwazi*”. Sasa, sijui ni wanasiwa wangapi, au ma-rais wangapi, wametunza ahadi zao, na sijui kama jambo hili bado lipo katika katiba ya Tanzania – lakini najua kwamba, bado lipo katika Biblia, na ni jambo ambalo mchungaji anahitaji kujitoa kulifanya. Kusema kweli, na kuwa mwaminifu.

Lakini hapa, kuna onyo! Na hii ni changamoto, ambayo kiongozi anapaswa kukutana nayo. Wakati mwingine, unaposema kweli – inaweza kufanya maisha yaye magumu kwako. Inaweza hata kukufanya usipendwe na wengi! Na kwa baadhi ya watu, kwa karne nyingi, kusema kweli, limekuwa jambo la kuhatarisha maisha ya mtu. Kama tunafikiri kuhusu uongozi katika ulimwengu wa siasa, viongozi wengi wamewaua watu, ambao wamejaribu kuwapinga. Wamewaadhibu watu, kwa sababu wamewaambia kweli. Viongozi hawa, hawakuweza kuvumilia kusikia kweli. Kwa hiyo, waliwafunga watu, wakawaumiza, na hata kuwaua, kwa sababu waliwanyoshea kidole cha kweli.

Katika Agano Jipy, Yohana Mbatizaji aliuawa kwa sababu alisema kweli. Aliuawa na mfalme Herode, kwa sababu alisema kweli, kuhusu tabia mbaya ya Herode. Katika kitabu cha **Matendo**, Stefano, mmoja wa wale mashemasi **7**, katika Yerusalemu, alisema kweli kuhusu Yesu Kristo. Viongozi wa dini, hawakupenda kusikia hivyo – na kwa hiyo walimuua kwa kumpiga mawe. Katika baadhi ya sehemu ulimwenguni, hata leo, Wakristo wengi wanauawa, kwa sababu wanasmamia kweli ya injili. Katika kanisa, baadhi ya watu, ambao wamewahi kusema kweli, wameambulia kufukuzwa na viongozi wao wa kanisa! Je, unaweza kuamini hii?! Labda, baadhi yenu mmewahi kusema kuhusu jambo fulani, unajua kuwa unasema kweli, na unajisikia kwamba linapaswa kusemwa, na hii inaweza kukufanya usipendwe. Sisemi hivi ili kukuzuia kusema kweli. Ninasema hivi ili kukupa tahadhari, kiongozi anapokuwa mwaminifu na mkweli, wakati mwingine, inaweza kufanya maisha yaye magumu kwake.

Hadithi kuhusu mmisionari mmoja:

Wakati mwingine, kuna gharama ya kusema kweli, lakini tunapaswa kuendelea kuwa wenyewe nguvu, na tunapaswa kufanya ambacho Biblia inatuambia kufanya, na siyo ambacho watu wanatuambia kufanya. Kuna mambo mengi sana, ambayo tungeweza kusema katika aya hizi, lakini sasa hatuna muda wa kutosha. Pia kuna habari nyingi katika sura **4**, ya kitabu hiki, na kwa hiyo ndiyo maana, kesho tutaendelea kuangalia sifa za kiongozi mwadilifu. Ni somo kubwa, na muhimu sana! Je, tunavezaje kutambua yupi ni mchungaji mzuri, au mwinjiisti mzuri? Je, wanapaswa kuwa watu wa aina gani? Tunapaswa kuangalia, ili kuona kama wanazaaz tunda zuri. Na tunaweza kutumia aya hizi, ambazo tumejifunza leo, ili kuona aina ya sifa ambazo kiongozi, anapaswa kuwa nazo. Mungu atusaidie kuelewa Neno lake, na kuliishi katika maisha yetu leo.

NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU: KIPINDI 5:
Je, nisifa gani tunapaswa kuziona ndani ya kiongozi?
“Kiongozi anaye tumika - Kiongozi mtumishi”.

Asubuhi hii, tutaendelea kuangalia sifa za kiongozi mwadilifu. Nataka tulenge kwenye somo la kiongozi mtumishi, na mnyenyeketu. Je, inamaana gani, kuwa kiongozi anaye tumikia watu wake? Je, inamana gani kuwa mchungaji anaye tumikia watu wake, ambao anafanya kazi pamoja nao? Katika sura ya nne kitabu hiki cha Askofu Mtetemela, anaonesha umuhimu wa sifa za kiongozi mtumishi. Anasema hivi: “*moja wapo ya malengo ya kitabu hiki, ni kuweka mkazo juu ya aina hii ya uongozi. Hii ni kuhusu huduma. Haihusu kutafuta cheo cha juu, au umuhimu. Utumishi ni kitu ambacho ni msingi wa watumishi wote wa Kikristo. Kuwa kiongozi ni ishara ya mtu aliye jitoa kumfuata Yesu Kristo*”.

Ninafikiri, hili ni jambo kubwa katika Afrika, na katika nchi nyngi ulimwenguni. Katika siasa, na biashara; katika jamii tunazoishi – sote tumesikia hadhithi za viongozi, ambao hawafikiri kwamba uongozi nikuhusu kuwatumikia wengine. Badala yake, wanafikiri kwamba kila mtu anapaswa kuwanyenyekeea na wao! Wanafikiri kwamba wengine wanapaswa kuwatumikia wao! Lakini, nafikiri pia, kwamba hili nitatizo katika makanisa mengi. Viongozi wengi, na wachungaji wengi, hupata shida kuiga mfano huu wa uongozi. Bila shaka, kuna wachungaji, na hata maaskofu, ambao hutaka tu kuwa kwenye nafasi hizo za uongozi, ili wawe watu wa kubwa! Wanafikiri kwamba wao ni watu muhimu sana. Nataka kusema kwamba, hakuna nafasi ya viongozi katika kanisa, ambao wanatenda hivyo. Haya siyo ni maoni yangu tu. Pia siyo kwamba ni maoni ya mwandishi wa kitabu hiki. Haya ni maoni ya Yesu Kristo mwenyewe! Na kwa dakika chache, tutakuwa tunaangalia katika mfano aliotupa Yesu, kuonesha jambo hili. Kabla ya kuangalia Biblia zetu, nitawaambia hadhithi kutoka kitabu hiki, ambacho kinatupa mfano wa kiongozi aliyejaa kutumikia wengine:

Hadithi kuhusu mkuu wa shule:

Mkuu wa shule huyu; ambaye alikuwa mkuu wa shule yote, aliacha ofisi yake, na akaenda kwenye vyoo vya wanafunzi. Alikuwa ameiandaa kufanya kazi, ambayo haikuwa kawaida yake kuifanya – kusafisha vyoo. Alitoka kwenye ofisi yake; kwenye kiti chake cha mamlaka, na kuwa tumikia watu aliokuwa akiwaongoza. Alionesha uongozi wake kwa vitendo. Hakuogopa kufanya kazi za kitumwa au za chini, na alimwonyesha mwanafunzi mfano halisi wa jinsi ya kuwa kiongozi mtumishi.

Tufungue Biblia zetu – **Yohana 13:1-17***. Mafundisho haya yametolewa na Yesu katika Chumba cha Juu, masaa machache tu, kabla ya kukamatwa na kusurubiwa kwake. Huu ni mlo wake wa mwisho hapa duniani. Huu ni muda wa mwisho wa kua pamoja, kabla ya msalaba.

Yesu na wanafunzi wake wako Yerusalem. Kulikuwa na watu wengi sana katika jiji, na wengi wao walikuwa wakijiaandaa kwa ajili ya siku kuu ya pasaka. Najiuliza ni mara ngapi Yesu alifikiri kuhusu usiku huo? Huu ulikuwa mlo wake wa mwisho, kabla ya mateso ya msalaba, na ingawa **Luka** anatuambia kwamba Yesu alikuwa akiutarajia mlo huo, lazima kulikuwa na hofu ya Yesu, kwa ajili ya kile ambacho kingeuka katika masaa ishirini na nne. Ingawa Yesu sasa amezungukwa na rafiki zake wakaribu – ni yeze peke yake anayejua nini kitatokea. Wanafunzi hawajui. Ingawa Yesu alikuwa amewaambia kuhusu msalaba – bado hawamwamini. Angalia mstari **2**. Unatuambia kwamba chakula cha jioni kilikuwa kinapakuliwa. Labda hiki kilikuwa ni chakula maalum kwa ajili ya pasaka. Lakini angalia mstari **4** kwa sababu inaonekana kwamba, badala ya kuanza kula chakula, “*Yesu anaondoka mezani; anavua vazi lake la juu, na kujifunga kitambaa kiunoni mwake*”.

Hapa ni wanafunzi kumi na wawili wenye njaa wanabidhi kula! Lakini Yesu anatoka mezani, na kufanya kitu ambacho haki kutarajiwa, na cha kushtua! Na ghafla, ninafikiri kila mmoja katika Chumba cha Juu, alikaa kimya. Kwa sababu hapa alikuwa ni mwalimu akijiweka katika mwonekano wa mtumishi mnyenyeketu. Na hiki anachofanya Yesu, lazima kiliwaacha wanafunzi wakiangaliana kila mmoja bila kuamini! Hawakuamini walichokuwa wanakiona. Yesu alichukua beseni la maji, na akaenda karibu na mwanafunzi mmoja. Angalia mstari **5**: “*Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwaosha wanafunzi wake miguu na kuipangusa kwa kile kitambaa alichojifungia*”. Sasa, tunahitaji kuelewa kitu fulani hapa. Katika jamii hiyo, kazi ya kuosha miguu siku zote ilikuwa kazi ya mtumishi wa chini wa nyumbani.

Hii ilikuwa kazi ya mtu aliyejaa na cheo cha chini sana. Kazi ya kuosha miguu ilichukuliwa kama kazi mbaya. Hakuna aliyependa kuifanya.

Wanafunzi wanafikiri – haiwezekani kwamba mwalimu kama Yesu, angeweza kufikiri kufanya kitu kama hicho. Lakini hapa, katika Chumba cha Juu, anayepiga magoti mbele yao, ni bwana wao, na pia mwalimu

wao. Anaweka pemberi kanzu yake; anaweka pemberi utukufu wake, na sasa anaosha miguu yao michafu kwa maji, na taulo. Watu amba ni Waislamu, wangejua kwa nini jambo hili ni la kusitusha.

Kama unajua kitu chochote kuhusu Uislamu, utajua kwamba mguu unachukuliwa kama sehemu ya mwili iliyo chafu sana. Wanaamini kwamba haipaswi kuonesha sehemu ya chini ya mguu mbele za watu. Imechukuliwa kama tusi kuonyesha mguu kwa uma; ni ishara ya kukosa heshima. Baadhi yenu mnawenza kukumbuka vita vya Iraq. Vita hivyo vilianza mwaka elfu mbili na tatu, na nchi nyingi, ikiwemo Marekani na UK, ziliivamia Iraq na walijaribu kumkamata Saddam Hussein. Labda unakumbuka pia, mwaka elfu mbili na nane, Rais wa Marekani, George Bush, akizumgumza katika mkutano huko Baghdad. Ghafla, mwandishi wa habari alimrushia viatu Rais George Bush. Na hii ilioneshwa kwenye TV. Mtu ambaye alirusha viatu, alikamatwa na kufungwa, ingawa viatu havikumpiga Rais.

Watu wengi ulimwenguni ambao hawakuwa Waislamu, hawakuweza kujua kwa nini mtu huyo alitaka kurusha viatu. Lakini, kama ni Mwislamu, utajua kwamba kumrushia viatu mtu ni tusi kabisa. Mguu na kiatu huchukuliwa kama uchafu, na pia najisi. Na kwa hiyo, mtu huyo aliporusha viatu, hakuwa anataka kumjeruhi Rais, lakini alikusudia kumtukana. Alikuwa akimwonesha kwamba hamheshimu. Kama unatembea ukipita karibu na msikiti, wa kati wa kusali, huwa unaona nini? Viatu vingi sana vimepangwa nje ya msikiti. Mwislamu anafikiri kwamba, kwa sababu viatu ni vichafu, na najisi, siyo sahihi kuvichukua na kuvipeleka katika sehemu takatifu, na kwa hiyo, wanavivua kabla ya kuingia kwenye msikiti.

Ngoja turudi kwenye Chumba cha Juu. Ingawa wanafunzi wa Yesu hawakuwa Waislamu, walikuwa Wayahudi, bado walifikiri kwamba, mtu ambaye aliosha miguu alikuwa mtu wa hadhi ya chini sana. Kwa hiyo, fikiri ni jinsi gani iliwa situa wanafunzi kuona mwalimu wao, akipiga magoti mbele zao, na kuosha miguu yao. Lakini si kwamba alikuwa mwalimu wao tu, alikuwa Mwana wa Mungu, akipiga magoti kwa unyenyekevu. Alikuwepo tangu mwanzo. Alimsaidia Baba Mungu kuumba ulimwengu. Kwa kweli, ni kiongozi wa viongozi wote, ambaye siku moja ata-abudiwa na mamilioni ya watu! Huyu ni Mwana wa Mungu, akipiga magoti kwa unyenyekevu, na kufanya kitu ambacho mtumishi wa chini alipaswa kufanya. Je, unaweza kupata picha mambo yalikuwaje katika Chumba cha Juu?

Ninahisi kwamba wanafunzi waliacha kuongea – na kulikuwa kimya. Kelele pekee ambayo wange-isikia, ni ya maji yakidondoka kwenye beseni. Lakini, angalia kilichotokea katika mstari 6: Wakati Yesu akiosha miguu yao hakuna mtu aliyesema kitu chochote, isopokuwa Petro! Hawezi kuamini kinachotokea!

Hawezi kukaa kimya wakati huu – na kadri Yesu anavyoosha miguu ya Petro, labda Petro alivuta miguu yake, na kumwambia Yesu: “Bwana siwezi kukuruhusu uoshe miguu yangu”. Na Yesu kwa upole anamwambia katika mstari 7: “*Huelewi sasa ninachofanya lakini utaelewa baadaye*”. Lakini, kama tunavyoona katika mstari 8, Petro bado hanafuraha, na anamwambia Yesu: “*Haupaswi kuosha miguu yangu*”. Haya ni maneno yenye nguvu sana, kutoka kwa Petro. Labda, Petro alikuwa na hasira juu ya Yesu kwa kumwona akifanya hivyo. Labda, Petro alijisikia kwamba, alichokuwa anikifanya Yesu, kilipaswa kufanya na mtumwa. Labda, alifikiri kwamba hakustahili kuosha miguu na kiongozi mwenye nguvu kama huyu. “*Yesu, wewe ni mwalimu wangu. Wewe ni Bwana wangu. Hupaswi kuosha miguu yangu*”.

Angalia kinachotokea katika mstari 8. Yesu analazimika kuwa mwazi kwa Petro. Anamwambia: “*Petro kama sitakuosha miguu yako, huwezi kuwa mwanafunzi wangu*”. Kwa maneno mengine, kama sitakuosha miguu yako, hatuwezi kuwa marafiki. Labda, Petro alisitishwa kusikia maneno hayo katoka kwa Yesu. Angalia jibu lake katika mstari 9: “*Sawa Bwana, kama unachosema ndyio hicho, usioshe miguu yangu tu, bali osha mikono yangu, na kichwa changu pia*”! Inatuonesha kwamba Petro alitaka kuwa mwanafunzi wa Yesu kweli kweli. Lakini, utaona kwamba Yesu hataki kufanya hivyo.

Angalia mstari 10. Yesu anamwambia Petro: “*Mtu aliyekwisha kuoga anahitaji kuoga miguu tu; mwili wake wote ni safi*”.

Je, jambo hili lina maana gani? Tunapokuja kwa Kristo, kama waamini katika yeye, tulipokuja kwa Yesu dhambi zetu zilioshwa zote; na tumekwisha kuosha mara moja, na hatuhitaji kuosha tena. Kwa maneno mengine, hatuhitaji kubatizwa tena! Tumesafishwa na kusamehewa kwa sababu ya msalaba – lakini kwa sababu asili yetu ya dhambi, na kwa sababu tunaendela kufanya dhambi, tunahitaji kuja kwa Mungu, na kuomba msamaha kila siku. Ingawa tumekwisha safishwa, kadri tunavyotembea katika ulimwengu huu, miguu yetu huchafuka, na kwa hiyo bado tunahitaji kuosha miguu yetu.

Angalia maneno ya Yesu kwa Petro, katika mstari 10: Nafikiri kwamba hiki ndicho anachozungumzia Yesu hapa. “*Petro, kabla ya kuja hapa jioni hii, inawezekana ulioga. Wewe ni msafi. Lakini ulipotembea kuja hapa*

usiku huu, kupitia mitaa yenyeye vumbi, miguu yako ilichafuka, kwa hiyo, kitu pekee ninacho hitaji kufanya ni kuiosha miguu yako. Mtu aliye kwisha kuoga, na amekwisha safishwa anahitaji kuoshwa miguu yake pekee". Mtu ambaye anakuja kwa Yesu, na dhambi zake zime-samehewa, ni msafi – lakini tunapaswa kuja kwa Yesu kila siku kwa ajili ya kutubu dhambi zetu za kila siku; kuoshwa miguu yetu. Je, unelewa anachokifanya Yesu hapa?

Hapa katika Chumba cha Juu, Yesu alipomaliza kuosha miguu yao, alisimama, na kurudi mezani. Na kisha kuwaambia wanafunzi wake katika mstari **12**: “*Je, mnaelewa nilicho wafanya?*” Ni swali pia ambalo tunapaswa kuendelea kujiliza sisi wenyewe. Je, tunaelewa ambacho Yesu alifanya kwa ajili yetu? Tunaweza kusema, ni kweli tunaelewa ambacho Yesu alifanya kwa ajili yetu – sisi ni wachungaji na wainjilisiti. Lakini, je, tunafahamu kikamilifu umuhimu wa kile alichofanya Kristo kwa ajili yetu? Je, tunaishi maisha yetu kama watu wenyeye shukrani, kwa Kristo kwa sababu ya kile alichofanya kwa ajili yetu? Je, bado tunashangazwa na maana ya msalaba? Je, unelewa alichokufanya Kristo? Unapaswa kuelewa – kwa sababa kama kiongozi wa kanisa, ni kazi yako kuelezea ambacho Yesu amefanya, kwa wale wasio elewa.

Yesu anawauliza wanafunzi wake, kama wanaelewa alichofanya alipoosha miguu yao. Nafikiri anawaambia, je, mnajua ni kwa nini nimefanya hivi kwa ajili yenu? Angalia mstari **14-15**: “*Basi, ikiwa mimi niliye Bwana na Mwalimu nimewaosha nyinyi miguu, nanyi pia mnapaswa kuoshana miguu. Nimewapeni mfano, ili nanyi pia mfanye kama nilivyo-wafanyien!*”.

Yesu anawataka waelewe nini maana ya utumishi; anawataka waelewe nini maana ya unyenyekevu. Yesu anasema, rafiki zangu, ingawa mimi ni Mwalimu na Bwana wenu, nimekuja kutumika, na ninyi kama wanafunzi wangu, nataka pia muwe viongozi wanaotumikiana kila mmoja. Ninataka mjishushe wenyewe, na ninataka mjitayarische kufanya kazi za chini, ili muwe mfano kwa wengine. Yesu anasema: “*Je, unelewa maana ya kutumikiana kila mmoja*”?

Kwa nini Yesu anauliza swali hili? Kwa sababu anataka kuwa mfano wao. Anawapa mafundisho jinsi wanavyopaswa kuishi maisha yao, na jinsi wanavyopaswa kutenda kama viongozi, katika kanisa la mwanzo. Lakini, pia anawauliza swali hili, kwa sababu ya kitu kilichotokea mapema, katika Chumba cha Juu. Fungua **Luka 22:24**. Jambo hili katika injili ya Luka, Yesu alikuwa amekwisha kuumega mkate, na kumimina mvinyo. Pia alikuwa amewaambia wanafunzi wake kwamba mmoja wao atamsaliti. Lakini, sikiliza nini kinatoka katika mstari **24**: “*Kulitokea ubishi kati ya hao mitume, kuhusu nani mionganii mwao anaye-fikiriwa kuwa mkuu kuliko wengine*”. Ni vigumu kuamini jambo hili, siyo hivyo! Kumbuka, huu ni mlo wa mwisho wa Yesu kula pamoja na wanafunzi wake. Katika masaa machache tu yajayo, Yesu atakamatwa na kuwekwa katika majaribu. Katika saa yake ya uhitaji; wakati Yesu alipowahitaji rafiki zake wakaribu kuwa na yeye – je, wanafanya nini? Wanahoji nani ni mkubwa mionganii mwao! Wanakuwa wabinagsi. Wanafanya kama kundi la watoto!

Je, hali hii hutokea kwetu? Kama wachungaji na wainjilisti; kama viongozi katika kanisa, je, huwa tunafikiri kwamba sisi ni wa kubwa kuliko mtu ye yote? Tunaweza tusijadili jambo hili katika kundi la watu. Tunaweza tuiseme ana kwa ana – lakini, mara kwa mara tunaweza kufikiri wenyewe, kwamba sisi ni bora kuliko yule, au huyu. Tunaweza kujisikia kwamba sisi ni muhimu kuliko wengine. Kama tunafikiri mawazo haya, Yesu anaujumbe kwetu: Ngoja nisome mstari **25-26**: Hiki ndicho Yesu alisema kwa wanafunzi wake, baada ya mabishano**. Rafiki zangu, msiwe kama wafalme hao, ambao hutaka kujifaidisha kupitia madaraka yao – lakini uwe kiongozi anayetumikia wengine.

Je, umewahi kufikiri – kwa nini miguu ya wanafunzi haikuoshwa, kabla ya chakula? Katika utamaduni huo, kwa wakati huo, jambo la ukarimu ambalo mwenyeji alifanya, kila mgeni alipofika, ilikuwa ni kumuliza kama angependa kuwohwa miguu yake. Na kama wangependa, mwenyeji alimwambia mtumwa kufanya. Hiyo ilikuwa kawaida katika Israeli wakati huo. Kwa nini? Kwa sababu katika siku hizo, hapakuwa na barabara za lami, na mitaa ilikuwa na uchafu na vumbi – na watu walivaa viatu vya wazi. Hawakuva viatu vya kufunika miguu. Na kwa hiyo, watu walipotembea mitaani, miguu yao ilichafuka sana.

Hii ndivyo ilivyo hata leo, katika maeneo ya vijiji Tanzania. Si ndiyo? Watu wengi leo, wanavaa viatu vya wazi, au ndara, na wanaishi katika mazingira ambayo ni makavu na yenyeye vumbi. Kwa hiyo, miguu yao inachafuka kwa urahisi. Pia hapa Tanzania, mna-utamaduni ambao huwa mnaufanya, kabla ya chakula. Ni kitu gani? Ni kunawa mikono. Kama unatembelea familia, na unajiandaa kwa ajili ya chakula, mtu mmoja huwa anakuja karibu yako na bakuli la maji, na sabuni - na kumimina maji kwenye mikono yako. Kama mwenyeji hatafanya hivyo – hiyo itakuwa siyo kawaida, na itachukuliwa kama tabia mbaya. Itakuwa ni kukosa adabu.

Kwa jinsi hiyo hiyo - katika Israeli wakati huo, ilikuwa ni kukosa adabu, kama mwenyeji hakukunawisha miguu. Kwa hiyo – hapa ni swali. Kama miguu ya wanafunzi ilikuwa michafu, na kama ilikuwa ni kawaida kwa mtumishi kuosha miguu ya wageni wanapofika, je, kwa nini miguu yao haikuwa imeoshwa, kabla ya chakula? Hatujaambwa sababu ni nini katika injili. Labda mtumishi wa nyumba alishindwa kufika. Labda mtumishi alikuwa mgonjwa. Hatujui – lakini tunajua miguu yao, haikuwa imeoshwa wakati waliopokaa kula chakula.

Hapa kuna wazo. Labda, wanafunzi waligundua kwamba mtumishi wa nyumba hakufika. Lakini, walipuuza kufanya kazi hiyo wenye, kwa sababu walifikiri kwamba ilikuwa ni kazi ya mtumwa, au mtumishi pekee. Kumbuka – walibishana kuhusu nani ni mkubwa. Labda, mmoja wa wanafunzi alikuwa amependekeza mmoja wao awaoshe miguu yao, lakini walikataa. Labda waliambiana: siwezi kufanya kazi hiyo. Ni chafu sana kwa mimi kuifanya. Ni kazi ya mtumishi, na mimi ni mkuu kuliko mtumishi! Labda, walijivuna sana na hivyo hawakutaka kufanya hiyo kazi. Na kama Yesu alivyokaa pembeni chumbani, akiangalia matendo ya wanafunzi wake – aliamua kufanya kazi hiyo mwenye, na kuwafundisha somo. Na kwa hiyo, ni Yesu aliyechukua taulo, na kufanya kazi ya mtumishi.

Rafiki zangu, je, mnaelewa nilicho-wafanya? Mnaniita Mwalimu na Bwana, hivyo ndivyo nilivyo, lakini pamoja na kwamba mimi ni mwalimu wenu, nimechagua kufanya kazi ya mtumishi. “*Nimewapa mfano, ambao mnapaswa kufuata kama nilivyo wafanya, kwa sababu hakuna mtumwa aliye mkuu kuliko bwana wake*”. Yesu anatuambia kwamba tunapaswa kuwa viongozi, ambao wanaoshana miguu kila mmoja. Sifikiri kwamba hii inamaana wanapaswa kufanya hivyo. Sifikiri kwamba kila mara tukienda kanisani, mchungaji anapaswa kuosha miguu ya kila mmoja. Yesu hasemi hivyo, lakini anajaribu kutupa fundisho hapa. Mfano wake unatuonesha kwamba, tunapaswa kuwa viongozi, wanao tumikia watu wetu katika kanisa letu. Tunapaswa kuwa watu waliotayari kufanya kazi za chini – kama vile mkuu wa shule, ambaye alikuwa tayari kutumikia shule kwa kusafisha vyoo, na kama vile aliviyotaka kuwa mfano mzuri, kwa mwanafunzi.

Na bado, mara kwa mara, huwa tunaona ni vigumu kufanya hivyo – siyo? Kama ni waaminifu; kama viongozi katika kanisa, wakati mwingine huwa hatujisikii kuwa tumikia wengine. Tuna kazi nyingi, na hatutaki kutumika. Kutakuwa na wakati, ambapo tunaweza kutojisikia kupenda kumtumikia mtu, ambaye tumeitwa kuosha miguu yake; hata mionganoni mwa kundi la waamini.

Kwa kweli, inaweza kuwa vigumu sana, katika kanisa kutumikiana kila moja - kwa sababu wakati mwingine kuna tokea uhusiano mbaya kutokana, na matatizo ya zamani. Ni rahisi kuosha miguu ya mtu tunayempenda, na tunayemjua vizuri, lakini mara nyingi ni vigumu sana kuwa tumikia wale tusio wapenda, au wale ambao wametumiza siku zilizo pita. Unaweza kuniuliza: kama ungejua alichosema kuhusu mimi huyu mtu, ungeona vigumu kuosha miguu yake.

Je, Yesu angesema na kufanya nini? “*Basi, ikiwa mimi niliye Bwana na Mwalimu nimewaosha ninyi miguu, nanyi pia mnapaswa kuosha miguu*” – mnapaswa kutumikiana kila mmoja. Hakuna visingizio. Yesu anaamuru hivyo. Na hili ni fundisho lenye changamoto, siyo? Lakini, fikiri kuhusu hili: Je, unafikiri Yesu alijisikiaje katika Chumba cha Juu, alipoosha miguu ya wanafunzi wake? Walikuwa ni rafiki zake, lakini wote walikuwa wamekosea, na wote wange mkimbia Yesu badaye. Katika masaa machache tu, miguu yote hiyo ingekuwa inamkimbia Yesu, katika Bustani ya Gethsemane.

Je, Yesu alijisikiaje alipoosha miguu ya Petro? Yesu alijua kwamba ndani ya masaa machache tu, Petro angemkana. Yesu alijua kwamba Petro angemwambia mtumishi msichana kwamba, hakumjua Yesu ni nani! Lakini bado, Yesu aliosha miguu yake! Na kisha, Yesu akaenda kwenye miguu ya Yuda. Yesu alijua kwamba Yuda alikuwa anapanga kumsaliti. Yesu alijua jinsi alivyo kuwa Yuda. Tumeambiwa na Luka, kwamba Yuda alikuwa akiiba pesa, kutoka kwa wanafunzi wengine! Je, Yesu alifanya nini? Je, alisema “*sioshi miguu yake. Yeye ni mtu mbaya, na hastahili ukarimu wangu*”?

Yesu alichagua kumtumikia, na alichagua kuosha miguu yake. Na hivi ndivyo ilivyo kwetu, siyo? Yesu anajua kila kitu kuhusu wewe na mimi; anajua makosa yetu, na udhaifu wetu. Anajua kuhusu usaliti wetu, na kumkataa kwetu. Anajua kuhusu nyakati, ambazo tumeponga kumkana Mungu kwa kijiweka sisi wenye kwanza, na wengine mwisho. Na bado – anaendelea kuwa mtii kwa kufa kwa ajili yako na mimi. Huu ni upendo usio na mashariti. Tufurahie na kuwa wenye shukrani, kwamba tunamwabudu mtumishi bora kuliko wote, ambaye alikuwa duniani, si kutumikiwa, bali kutumika.

Wafilipi 2:3-8*

Na kama viongozi leo – kama ni mchungaji au mwinjili – Yesu angekwambia: Nimekupa mfano. Ninakutaka ufanye kama mimi. Uwe kiongozi mnyenyeketu, na aliyetayari kutumika. Katika sura ya nne kitabu hiki cha Askofu Mtetemela, anaonesha umuhimu wa sifa za kiongozi mtumishi. Anasema hivi: “*moja wapo ya malengo ya kitabu hiki, ni kuweka mkazo juu ya aina hii ya uongozi. Hii ni kuhusu huduma. Haihusu kutafuta cheo cha juu, au umuhimu. Utumishi ni kitu ambacho ni msingi wa watumishi wote wa Kikristo.* Kuwa kiongozi ni ishara ya mtu aliye jitoa kumfuata Yesu Kristo”.

“NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU”. VIPINDI 6&7: “Viongozi na Migogoro”

Katika kitabu hiki, sura ya sita inahusu kiongozi na migogoro. Hivi ndivyo anavyosema **Askofu Mtetemela**: “*Katika sura hii, ninataka tuangalia kugawanyika na migogoro katika kanisa. Tunapaswa kupata muda wa kuangalia jambo hili, ili kwamba tuweze kuchukua hatua sahihi kujilinda na changamoto hizi. Je, kitu gani husababisha kugawanyika katika kanisa? Je, migogoro huanza vipi? Ni muhimu kwamba tunapaswa kutaja baadhi ya mambo, ambayo husababisha migogoro, ili kwamba tunaweza kujiaandaa, kwa ajili ya kukabili migogoro hiyo, na kisha kujiliinda wenyewe na watu wetu dhidi ya migawanyiko*”. Kwa hiyo, ngoja nitaje mambo machache, ambayo Askofu Mtetemela anasema katika kitabu hiki. Baadhi ya mambo, unaweza kuyatambua, kwa sababu umeyapitia, lakini mengine, unaweza kuwa hujawahi kuyaona.

Namba moja: Migogoro hutokea kwa sababu ya viongozi wabaya. Mara kwa mara, sababu ya migawanyiko na migogoro, katika kanisa, ni mwenendo wa maisha, na tabia mbaya za kiongozi. Kama kiongozi haishi maisha matakatifu, watu katika kanisa wataona, na wanaweza kusimama na kusema atolewe kwenye uongozi. Na kwa hiyo, katika hali hii, sababu ya migogoro ni mchungaji mwenyewe. Anapaswa kulaumiwa kwa hiyo migawanyiko na machafuko. Labda kiongozi amekuwa siyo mwaminifu. Labda amekuwa mzembe katika kazi yake. Labda anapungukiwa uadilifu na amekamatwa katika uzinzi. Labda amekuwa akiiba kanisani.

Hakika tunajua kwamba mambo haya huwa yanatokea hata katika AIC! Inahuzunisha kwamba, tunajua kuhusu mifano halisi. Uongozi mbaya mara zote utasababisha migogoro. Kama viongozi katika kanisa, kumbuka kwamba watu siku zote huwa wanakuangalia ili waone jinsi unavyoishi, na ndiyo maana Paulo anasema katika **1 Timotheo 3:2**, kwamba kiongozi, mzee, askofu: “*lazima asiwe na lawama*”. Anapaswa kuwa mfano mzuri kwa wale anaowaongoza.

Pia, mgogoro unaweza kutokea, pale kiongozi anaposhindwa kufanya kazi yake vizuri, siyo kwa sababu ya tabia mbaya, lakini kwa sababu ya kupungukiwa uwezo – na hili linaweza kuwa kosa la mwajiri. Mchungaji au kiongozi anapochaguliwa, tunaamini kwamba kiongozi huyo amechaguliwa, kwa sababu ana uwezo wa kufanya kazi hiyo. Lakini wakati mwingine, kanisa hufanya makosa. Huteuwa mtu fulani ambaye hana uwezo, au sifa sahihi kwa ajili ya kazi hiyo. Na kwa hiyo, kinachotokea ni kwamba, baada ya kuwa kazini kwa miezi michache, inatokea kwamba kiongozi hawezo kuongoza. Hii inaweza kusababisha mgogoro, siyo kwa kiongozi, lakini kwa wale walio mteua. Kwa hiyo, katika hali hizi zote, migogoro hutokea pale kiongozi anapokuwa haishi maisha matakatifu, na pale uamuzi mbaya unapofanywa na mamlaka ya kanisa.

Namba mbili: Migogoro hutokea kwa sababu ya mafundisho ya uongo. Hili ni jambo kubwa. Tungeweza kutumia masaa mawili, yanayofuata kuzungumzia kuhusu mafundisho ya uongo, katika kanisa – lakini hili siyo somo letu kwa leo, kwa hiyo nitasema kwa ufupi. Je, ninamaana gani ninaposema ‘*mafundisho ya uongo*’? Neno jingine, ambalo tungetumia ni ‘uzushi’. Mafundisho ya uongo ni mahubiri, au mafundisho yoyote, ambayo hayakubaliani na Neno la Mungu. Hili lilikuwa tatizo kubwa sana, katika kanisa la mwanzo, na ni tatizo kubwa katika kanisa leo. Katika barua za Agano Jipy, kuna maonyo mengi sana, kuhusu walimu wa uongo. Na ujumbe ni ule ule hata leo. Wachungaji wengi wanahubiri uongo! Baadhi ya wachungaji hata hawasomi neno la Mungu wanapohubiri!

Katika **1 Timotheo 1:3** Paulo anamwambia Timotheo: “*Hakikisha kuwa unawaagiza watu kutofundisha mafundisho ya uongo*”, na kisha katika mstari **6**: “*baadhi ya walimu, wameacha kweli, na wamegeukia mazungumzo yasiyo na maana. Wanataka kuwa wahubiri, lakini hawajui wanachosema*”. Jihadhari na walimu wa uongo, katika kanisa – na hakikisha kwamba, unafundisha kutoka kwenye Biblia, na siyo kutoka kwenye

kichwa chako mwenyewe! Ngoja tuangalie **Tito 1:9**, kwa sababu ninataka tuweke jambo hili wazi sana: “*Mzee lazima ashike mafundisho ya kweli, kama yalivyofundishwa, ili kwamba aweze kuwatia moyo wengine, kwa mafundisha ya kweli, na kupinga mafundisho yaliyo kinyume*”. Na halafu angalia mbele katika **Tito 2:1**: “*lazima afundishe mafundisha, ambayo yanakubaliana na mafundisho ya kweli*”. Hii inaeleweka vizuri, siyo? Nina swali. Je, unafundisha mafundisho ya kweli katika kanisa lako? Kwa sababu kama haufundishi kweli, hautii Neno la Mungu, na unalipoteza kanisa lako. Hii ni mbaya sana – ni jambo kubwa sana. Mafundisho ya uongo yatasababisha migogoro, na migawanyiko.

Katika Agano Jipyä, baadhi ya watu walikuwa wanasema kwamba, Yesu hakuwa binadamu kamili. Wengine walikuwa wanasema kwamba, kwa sababu walikuwa wameokolewa na Yesu, haikuwa jambo la kujali kuhushu tabia zao. Wakati wa zamani, kanisa lilipaswa kushugulika na uzushi mwingi sana, lakini hata leo, bado kuna mafundisho ya uongo. Katika baadhi ya makanisa, katika nchi za magharibi, kuna wachungaji, ambao hawaamini kwamba Yesu alizaliwa na bikira! Hawaamini kwamba kufa na kufufuka kwa Yesu kuliliwa halisi! Hii ni kweli? Ndiyo – na pia inastusha! Kuna baadhi ya mafundisho kutoka kanisa la Roman Katholiki, ambayo siyo ya kibiblia. Pia, vipi kuhusu Mashahidi wa Jehova? Mafundisho yao kwa hakika yamebeba uzushi.

Ninajua kwamba katika Afrika, unaweza kuwasha TV yako, na kuangalia wachungaji wakihubiri. Kuwa makini sana, kwa kile unachotazama. Baadhi ya mahubiri siyo ya kibiblia. Baadhi ya mahubiri yanafundisha kwamba, mkristo hawezi kupata ugonjwa! Mengine yanafundisha kwamba, unaweza kuomba kwa Mungu chochote unachotaka, na atakupa, kama tu una imani kubwa. Mengine hujaribu hata kukuibia pesa zako! Mafundisho ya uongo, siku zote yatatikisa kanisa, na kusababisha migogoro. Na hii ndiyo maana mchungaji au Askofu, ana wajibu wa kusimamia ukweli wa Biblia. Kama haufundishi kutoka kwenye Biblia, utaishia kwenye migogoro. Na pia ningeongeza kwamba – kama haufundishi kutoka kwenye Biblia – kwa nini ni mchungaji?!

Namba Tatu: Migogoro hutokea kwa sababu ya ubaguzi. Na ninahisi, unaweza hata kuongeza ukabila katika sehemu hii. Ndani ya kanisa, unaweza kukuta kwamba, waumini wa kibili moja kubwa, wakifiki kwamba, wana haki ya kuongoza, watu kutoka makabila mengine. Je, kitu gani kitatokea kama mchungaji atachagua wazee wake, au wahasibu wake, kutoka kabilia lake tu? Hii itasababisha ugonvi mkubwa, kwa waamini kutoka makabila mengine. Hali hii inajulikana kama ubaguzi na upendeleo. Wakati mwagine – mchakato wa kuchagua viongozi, na wachungaji wapya, imesababisha kuibua maswali kuhusu jinsi inavyofanyika. Kwa nini mchungaji yule alitumwa pale – lakini huyu hapa akatumwa kule? Tunapaswa kuwa makini zidi ya upendeleo, na ukabila katika kanisa. Katika baadhi ya makanisa, pia kunaweza kukawa na ubaguzi wa kijamii. Watu ambao ni matajiri na wasomi, wanaweza kujitenga na watu masikini. Hawataki kujumuika nao, kwa sababu ya hadhi zao. Je, hii inapaswa kutokea katika kanisa? Kwa kweli hapana, lakini inatokea. Iilitokea katika kanisa la mwanzo. Katika barua yake **Yakobo** anazungumza kuhusu jambo hili. **Yakobo 2:1-4***. Kama viongozi, msioneshe upendeleo – kwa sababu kama mtafanya hivyo, mnapaswa kutarajia migogoro.

Namba nne: Migogoro hutokea kwa sababu ya usimamizi mbaya wa fedha. Sitasema sana kuhusu jambo hili hapa, kwa sababu tutaongea kuhusu hili katika kipindi chetu kinachofuata. Kiongozi wa kanisa ameaminwa kutunza fedha za kanisa. Anawajibika katika swala hili. Anapaswa kuangalia maswala ya fedha kwa uangalifu. Anapaswa kutoa taarifa ya pesa kwa kanisa, na kwa Askofu. Lakini, kama tulivyosema mwanzo, kuna baadhi ya viongozi ambao hulewa madaraka na vyeo, na wanaanguka katika mtego wa matumizi mabaya ya fedha. Huwa wanaanza kutumia fedha za kanisa kwa kazi zao wenyewe. Na hili linapogundulika kwa kanisa, huwa kuna hasira nydingi – na watu wa kanisa. wanahaki yakuwa na hasira kwa jambo hili, kwa sababu imani yao imesalitiwa. Hujuma na mambo yanayohusu fedha yanaweza kuwa chanzo kikubwa cha migogoro, katika makanisa mengi ya Kiafrika. Mtume Paulo anasema jambo hili vizuri sana, katika **1Timoteo 3:3** kwamba kiongozi lazima asiwe “*mpenda fedha*”. Ili migogoro idhibitiwe, na kujilinda mwenyewe, ni muhimu kwamba uwe na utaratibu kuhusu mambo ya fedha, ili kwamba watu waweze kuona kinachotokea kuhusu fedha zao.

Namba tano: Migogoro hutokea kwa sababu ya uongozi wa ki-dikteta. Je, ninamaana gani katika kusema hili? Basi, sote tunajua kuhusu Marais, ambao hugeuka madikteta. Watu hawa wanajiamini sana. Wanafanya wanachotaka, na hawazingatii sheria. Watu ambao hupuuza kusikiliza sauti ya mtu yeoyote, na huwa wanafikiri kwamba wanamamlaka yote. Watavunja sheria, na kuwa wakatili dhidi ya mtu yeoyote, ambaye hakubaliani nao. Wanaweza hata kuwatishia, na kuwaua watu, ambao watawapinga. Kwa mfano: Adolf Hitler aliyekuwa Rais wa Ujeruman, wakati wa vita vyä pili vyä dunia. Idi Amini wa Uganda; Mengistu wa Ethiopia, na Robert Mugabe wa Zimbabwe. Tungeweza kuendelea na orodha ndefu ya watu kama hawa; watu ambao wamesababisha mateso mengi, na ambao wamefanya maovu mengi katika nchi zao.

Sisemi kwamba baadhi ya wachungaji, na viongozi wa makanisa, huenenda kama hawa watu tuliovatata! Lakini, ninachosema ni kwamba baadhi ya wachungaji, wanapokuwa viongozi, huenenda kama vile wanajiongoza wenyewe, na huwa wanapuuza kusikiliza mtu yelete, hata watu ambaa wanamamlaka juu yao! Katika dhehebu la AIC, muundo wa uongozi umewekwa. Viongozi wa kanisa, wanapaswa kutimiza kazi zao, kwa mujibu sheria mbali mbali za AIC. Kuna katiba inayopaswa kufuatwa. Lakini migogoro hutokeea pale kiongozi, au mchungaji, anapofikiri kwamba yeye yuko juu ya sheria. Wanataka kucheza na sheria zao wenyewe! Na kisha, ufanya maamuzi bila kutumia katiba, au bila kumshirikisha mtu yelete. Wanashau kwamba wao ni watumishi, na badala yake, kufikiri kwamba wao ni wamiliki! Kwa hiyo, kumbuka, kama unataka kuzuia migogoro katika kanisa lako, na katika AIC yote, usiwe dikteta!

Namba sita: Migogoro hutokeea kwa sababu za kisiasa. Hapa Tanzania tunaishi katika wakati, ambaa watu katika kanisa, wana uhuru wa kuijunga na vyama mbali mbali vya siasa. Na hiki ni kitu kizuri. Hapa Tanzania, hasa wakati wa mwaka wa uchaguzi, kuna mambo mengi yakuvutia kuhusu siasa. Baadhi yenu mnawenza msikubaliani na wazo hili, kwa hiyo hapa nitatumia maneno ya Askofu Mtetemela tu. Yeye ni Mtanzania ambaye amekuwa katika uongozi kwa miaka mingi – na kwa hiyo anajua mambo mengi zaidi kuhusu siasa, katika nchi hii kuliko mimi. Ninafikiri kwamba, yeye anasifa za kutupa ushauri juu ya somo hili.

Anasema hivi katika sura 6 ya kitabu chake: “*Ni muhimu sana kwa kiongozi wa kanisa kuwa makini kuhusu jambo hili. Kiongozi hapaswi kusimama upande mmoja, au kuunga mkono chama kimoja cha siasa, mbele ya kanisa. Kwa kufanya hivyo, anaweza kusababisha mgogoro mionganoni mwa Wakristo. Haipaswi chama fulani kupewa nafasi ya kutangaza itikadi zake katika kanisa. Kiongozi katika kanisa, hapaswi kuwa chanzo cha migogoro ya kisiasa. Badala yake, anapaswa kuwafundisha watu wake, kuishi kwa amani, na siyo kusababisha mgawanyiko*”.

 Haya ni maneno ya Askofu Mtetemela.

Namba saba: Migogoro hutokeea kwa sababu ya kukosekana kwa usawa katika mgawanyo wa rasilimali. Na tena, ninaenda kunukuu kutoka kitabu hiki, ili kukupa mfano anaosema Askofu Mtetemela. Ninafikiri kwamba, mgogoro huu katika kanisa yawezakuwa ulisababishwa na mamlaka za kanisa, na siyo wachungaji binafsi. Kiongozi wa kanisa ni mwangalizi wa fedha, zinazokusanywa katika kanisa lake, na anawajibika kwa hilo. Anaweza kuamua wapi zitumike hizo fedha. Ana mamlaka ya kufanya hivyo. Lakini hana mamlaka yoyote ya kuamua jinsi diyosisi inavyopaswa kutumia fedha zake. Kwa hiyo, eneo hili la mgogoro, ambalo tunaangalia kwa sasa, linaweza kuwa husu sana walio katika mamlaka ya juu.

Askofu Mtetemela anatuambia hadithi hii kuhusu uzoefu wake binafsi. Anasema kwamba: “*Nilipokuwa mwenyekiti wa baraza la Wakristo Tanzania, nilipaswa kutatua migogoro katika kanisa husika. Tatizo kubwa ambalo lilikuwa limesababisha mgogoro, lilikuwa ni malalamiko kwamba, ofisi kuu lilikuwa imeshindwa kuonesha usawa, katika ugawaji wa fedha za maendeleo na rasilimali. Waliamini kwamba, eneo lao lilikuwa limepuuzwa na kusahaulika. Wakati huo huo waliona kwamba, maeneo mengine yalipewa upendeleo, katika ugawaji wa misaada ya miradi ya maendeleo. Huu ulikuwa mwanzo wa mgogoro mkubwa, ambao ulisababisha mpasuko katika kanisa. Baadhi ya jumuia za kanisa, zilikuwa zimejitenga kutoka kwenye uongozi wadhehebu hilo, na kuanzisha kanisa jingine, lenye viongozi wake wa kujitegemea. Walikuwa wamewakataa viongozi wa kanisa mama – yote hayo ni kwa sababu ya jambo hilo*”.

Na kwa hiyo, unaweza kuona kwamba, kama hakuna haki, au usawa katika ugawaji wa rasilimali za kanisa, inaweza kusababisha migogoro mikubwa. Siyo kwa sababu ya fedha tu; kuna njia zingine ambazo upendeleo, au kupuuzwa, kunaonekana. Mchungaji ambaye ametumwa katika kanisa dogo, umbali wa kilomita nydingi kutoka ofisi kuu – anaweza kujisikia kwamba amesahaulika; kifedha na kinafsi. Hakuna mtu yelete anamtembelea kutoka makao makuu, na hakuna fedha zinazopatikana kutoka makao makuu - na bado anasikia kwamba katika miji mikubwa, ambako kuna makanisa makubwa, fedha zinapatikana kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya ya makanisa! Je, hii itamfanya mchungaji ajisikie vipi? Je, anajisikia kuthaminiwa na kusaidiwa? Bila shaka hapana. Unaweza kuona namna gani jambo hili lingesababisha kukata tamaa na mgogoro. Nimetaja eneo hili la mgogoro, kwa sababu Askofu Mtetemela amefanya hivyo katika kitabu chake, lakini kama nilivyo sema mwanzo, huu ni mgogoro ambaa umesababishwa na mamlaka ya kanisa, na siyo mchungaji binafsi.

Namba nane: Migogoro hutokeea pale viongozi wanapotaka kubaki madarakani kwa muda mrefu zaidi. Na ninafikiri hali hii huwa hatokea kwa wachungaji na wainjilisti, lakini hali hii inaweza kutokea hasa kwa maaskofu, ambaa wako katika mamlaka ya juu. Wakati mwingine wanaweza kukataa kuachia nafasi zao za uongozi, hata kama mikataba yao imeisha. Hapa kuna mfano: Katiba ya kanisa inaweza kusema kwamba, mtu anapaswa kuwa kazini kwa kipindi cha miaka 5 tu, na baada ya hapo anapaswa kujiuzuru. Lakini mtu anaweza kupuuza sheria hii!

Mtu kama huyo, anaweza hata kujaribu kutafuta sababu ya kubaki katika kazi yake; anaweza kuomba kuongezewa muda; anaweza hata kulinda kazi yake kwa nguvu, na kupuuza kuondoka! Katika kitabu hiki, Askofu Mtetemela anasema kwamba, hata baadhi ya maaskofu wakuu wamekataa kustaafu! Kwa nini? Kuna sababu chache. Labda wanatamani madaraka! Labda wamezoea kiwango cha maisha ya juu, na kwa hiyo hawataki kuachia. Labda wamekuwa na kiburi, na hawafikiri kwamba, kuna mtu mwininge anaweza kufanya kazi hiyo kama wao.

Askofu Mtetemela pia anasema kwamba, kama utakutana na watu kama hawa, kuna uwezekano mkubwa kwamba, watu hao walitaka uongozi kwa sababu zao binafsi. Labda walifanya juhudhi nydingi kupata uongozi huo; wakipiga kampeni kwa bidii, labda hata kutumia rushwa, wakitoa zawadi na mambo mengine. Na kwa hiyo, wanaona kwamba, ni vigumu sana kuachia nafasi, ambazo wamezitafuta kwa muda mrefu sana. Hii inasababisha migogoro mingi. Hii ni aina ya mambo ambayo tunayaona katika siasa, siyo? Nafikiri kwamba, nchi nydingi katika ulimwengu, zina katiba inayosema kwamba, Rais anaweza kutawala kwa mihula miwili tu. Labda kwa jumla ya miaka **8** au **10**.

Lakini, mara kwa mara tunaonaje, kwamba Rais anapofika mwisho wa mihula yake miwili, anataka kubaki katika madaraka. Na kwa hiyo, anabadilisha katiba, ili imruhusu kutawala kwa muhula wa tatu. Tuliona katika nchi ya **Burundi** mwaka **2015**. Je, matokeo yalikuwaje? Bado ni Rais – sasa yuko katika mulula wake wa tatu. Lakini hii ili sababisha migogoro mingi sana. Zaidi ya watu **3000** walikufa, na zaidi ya watu **200,000** walikimbia nchi – kwa sababu ya mtu mmoja, ambayo hakutaka kustaafu. Labda, katika siku zizajo, baadhi yenu mtakuwa katika nafasi ya uongozi wa madaraka, ambayo yamewekewa kikomo na katiba. Anda fikira zako sasa. Achia madaraka unapopaswa kufanya hivyo, na epuka kusababisha migogoro.

Kwa hiyo, tumeona baadhi ya migogoro ambayo viongozi, na wachungaji hukutana nayo. Baadhi ya migogoro hiyo inaeleweka kwako, na labda umewahi kukutana nayo. Bila shaka, kuna migogoro mingi zaidi, ambayo tungeweza kuangalia, kama tungekuwa na muda wa kutosha. Hebu kumbuka kwamba, migogoro katika kanisa, hufanya ushuhuda wakanisa kuwa dhaifu katika jamii. Migogoro wakati mwininge pia, husababisha kanisa kutumia gharama kubwa, katika kutatua migogoro - na kutumia muda mwingu, na nguvu nydingi hypotea katika mabishano na chuki, badala ya kufanya mambo mengine ya msingi. Kwa hiyo, tunapohitimisha, kwa ufupi sana, ngoja nitaje miongozi **7** ambayo Askofu Mtetemela anazungumzia katika kitabu. Kuna muhitasari wa mambo, ambayo tumekuwa tukijifunza, natumaini kwamba, yatakusaidia kuepuka, na kutatua, migogoro inapotokea katika huduma yako.

1. Tambua mipaka ya mamlaka yako: Kumbuka kwamba, kazi yako ni kazi ya Mungu kabisa. Wewe unafanya kazi yake tu, na kwa hiyo, yeye ndiye mwenye kazi. Wewe unawajibika kwake; kwa Askofu, na kwa watu wengine. Una jukumu kubwa – lakini usifanye mambo ambayo haya kuhusu.

2. Zingatia sheria: Kumbuka kwamba, kiongozi anapaswa kuwa mfano. Anapaswa kuzingatia utaratibu, na kanuni ambazo zimebekwa katika katiba ya taasisi yake. Na hii inamaana kwamba, kiongozi hapaswi kutumia fedha kwa ajili ya malengo mengine, tofauti na yale yaliyo wekwa katika utaratibu. Kiongozi hayuko juu ya katiba!

3. Kubali ushauri: Kuwa kiongozi haina maana kwamba unajua kila kitu! Unapokubali ushauri, inaonesha kwamba, wewe ni mnyenyeketu, na uko tayari kusikiliza wengine. Tafadhalii kumbuka hili: kupokeea ushauri kutoka kwa wengine, haina maana kwamba kiongozi ni dhaifu. Baadhi ya watu wanaweza kufikiri hivyo – lakini hii ni ishara ya unyenyekevu. Na kama kiongozi atapata ushauri mzuri, anapaswa kuwa tayari kukubali, na kutumia ushauri huo kama anaweza. Hii itakuwa faraja kubwa, kwa wale amba wanafanya kazi naye, na itajenga roho ya umoja kadri mnavyo fanya kazi kwa pamoja.

4. Kuwa na bidii katika kudadisi mgogoro: Kama mtu fulani atakuja kwako, na malalamiko kuhusu jambo fulani katika kanisa, usifanye haraka kufanya maamuzi. Ni muhimu kwamba, kiongozi apate maelezo kamili kuhusu mgogoro, kabla ya kuchukua hatua. Kusanya taarifa zote kuhusu mgogoro. Na unapofika hatua ya kufanya maamuzi, hakikisha kwamba ni ya haki, na hakikisha kwamba hayana upendeleo.

5. Usiwe na kinyongo! Hii mara zote, ni vigumu sana kufanya. Sote tunajua kwamba ni vigumu sana kuwasamehe watu fulani, wanapokuwa wametutendea jambo baya. Lakini inapowezekana, baada ya mgogoro, kutatuliwa hakikisha kwamba kuna mapotano na siyo chuki.

6. Kubali kurekebishwa, na kukosolewa: Siyo viongozi wote wako tayari kuoneshwa makosa yao. Tunahitaji kukumbuka kwamba, kiongozi ni binadamu tu. Na tunajua kwamba binadamu hufanya makosa. Hivyo, tunapofanya makosa, tunahitaji kukubali kukosolewa, na kuwa tayari kurekebishwa .

7. Shughulikia migogoro mapema: Ni jukumu la kiongozi kutopuuza matatizo yanopotokea. Anapaswa kuyashugulikia, na kuwa tayari kuongea na watu wanaohusika katika matatizo hayo. Kuwa tayari kuwasikiliza watu wenye manung'uniko, hujenga ujasiri miongoni mwa watu anaowaongoza. Shughulikia matatizo yanapokuja; usiyazike na kutarajia kwamba yataondoka menyewe. Fahamu kwamba, nyufa ndogo hugeuka kuwa kubwa – kwa hiyo, tatu matatizo wakati yakiwa madogo.

Kwa hiyo, tumetaja baadhi ya migogoro ambayo imezoeleka, ambayo wachungaji na wainjilisti, hukutana nayo katika kanisa - na ninahakika kwamba, kuna mifano mingine mingi zaidi, ambayo unaweza kutafakari. Mara zote kutakuwa na migogoro, ambayo tunapaswa kukutana nayo, lakini ngoja ni waachie maneno machache ya ushauri kutoka kwenye Biblia, kwamba tunahitaji kuthubutu na kuchukua hatua: **Waebria 12:14:** “*Tafuteni kwa bidii kuishi kwa amani na watu wote*”. Na **Warumi 12: 17-19** “*Usilipe ubaya kwa ubaya. Kuwa makini kufanya ambacho ni sahihi machoni pa kila mmoja. Kama inawezekana, kadri unavyoweza, ishi kwa amani na kila mmoja. Usilipe kisasi, rafiki yangu, lakini acha kisasi kwa Mungu*”.

“NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU”. KIPINDI 8:
Je, ni sifa gani tunapaswa kuziona kwa kiongozi mwadilifu?
“Kiongozi aliyeitwa” (Kuitwa, utii, kujitoa, kutumika)

Mchana huu tunaendelea na masomo yetu, tukiangalia katika swalii: Je, ni sifa gani tunapaswa kuziona kwa kiongozi mwadilifu? Na katika kipindi hiki, tunaangalia somo la ‘kuitwa’: “*Kiongozi wa Kikristo anapaswa awe ameitwa*”. Askofu Mtetemela, ameandika kuhusu jambo hili, katika sura ya **nne** ya kitabu hiki, kwa hiyo, ngoja nianze kwa kusoma moja ya nukuu zake: “*Ni muhumi kwamba, kiongozi anapaswa kujua katika moyo wake, kwamba ameitwa na Roho wa Mungu, na kwamba anataka kuingia katika huduma yake, ili kumtukuza yeye, na si kwa sababu nyininge. Tunahitaji kuona viongozi, ambaao nia yao siyo kuwa katika nafasi za uongozi kwa ajili ya faida yao binafsi, lakini, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Wito lazima uwe wa uhakika, katika maisha yao*”. Mtetemela, anasema nini? Kiongozi wa Kikristo, anapaswa kujua katika moyo wake, kwamba ameitwa na Roho Mtakatifu, kuchukua jukumu la uongozi, katika kanisa. Kwa maneno mengine, kiongozi anahitaji kupokea wito, kutoka kwa Mungu, ili aingie katika jukumu hilo.

Na kisha anasema hivi: “*Katika kanisa, kiongozi hapaswi kuchaguliwa, kwa sababu tu amepata kura nydingi, au kwa sababu tu anaujuzi wa mambo ya pesa, au kwa sababu tu anajulikana vizuri. Hapana. Nafasi ya uongozi, katika kanisa, ni kwa ajili tu ya mtu, ambaye anaamini katika moyo wake, kwamba ameitwa kweli na Mungu - na kanisa linapaswa kukubaliana na wito wake*”. Na kisha, Askofu Mtetemela, anatupa baadhi ya mifano ya viongozi, katika Biblia, ambaao walikuwa wameitwa na Mungu, kufanya kazi maalumu ya uongozi. Na pia, ananukuu kutoka Yeremia, ili kutupa mfano kuhusu viongozi, ambaao hawakuwa wameitwa na Mungu.

Ngoja tuone mfano huo kwanza. **Yeremia 14:14***. Mara kwa mara, hili lilikuwa ni tatizo katika Agano la Kale. Manabii walipaswa kuwa viongozi. Nabii wa kweli, alikuwa na mamlaka ya kusema mambo kwa watu, kwa niaba ya Mungu, lakini pia, kulikuwa na manabii wa uongo, ambaao walidai kwamba walikuwa na ujumbe kutoka kwa Mungu. Ukweli ni kwamba, Mungu hawakuwa amesema nao, na hakuwa amewapa mamlaka ya kuongea kwa watu. Mungu anamwambia Yeremia: Mimi sikuwatuma. Sikuwachagua. Kwa maneno mengine, sikuwaita kuwa manabii wangu. Wamejifanya wenyewe kuwa manabii. Kwa huzuni, kwa namna hiyo hiyo, katika kanisa leo, kuna baadhi ya viongozi, wachungaji, wainjilisti, na hata maaskofu, ambaao hawakuitwa na Mungu kuwa katika nafasi hizo za uongozi. Mungu hakuwatuma, au hakuwa chagua, lakini badala yake wamejichagua wenyewe, au walichaguliwa na kanisa, bila kumshirikisha Mungu.

Labda, wana sifa sahihi kwenye makaratasii. Labda walikwenda chuo cha Biblia. Labda sinodi ya kanisa iliwapigia kura - lakini hapa kuwa na upimaji kamili wa tabia zao, au kama wameitwa na Mungu katika huduma hiyo. Kwa baadhi ya wachungaji, na viongozi wa kanisa, wanaona ni kama kazi tu, lakini hawajasikia moto wa wito ukiwaka ndani yao, na hawakuitwa na Mungu kufanya kazi ya utumishi. Na katika mazingira hayo, Mungu angesema: ‘*mimi sikuwatuma. Sikuwachagua. Sikuwaita*’. Walifanya uamuzi wenyewe, na watu wengine waliwachagua. Usifanye kosa kwa kufikiri kwamba yelete, ambaye ni mchungaji, au kiongozi wa kanisa, ameitwa na Mungu katika nafasi hiyo. Askofu Mtetemela anasema hivi: “*Ni hatari kwa kanisa kuwa na viongozi, ambaao hawakutumwa na Mungu*”. Kwa nini? Kwa sababu wanaweza kuharibu kanisa. Wanaweza kuwapoteza watu, na kusababisha kila aina ya matatizo.

Pia anataja baadhi ya mifano mizuri kutoka kwenye Biblia; viongozi ambaa walikuwa na wito kamili, na ambaa walikuwa viongozi wenye nguvu, kwa watu wa Mungu. Kwa hiyo, ngoja tuangalia mifano michache. Fungua **Yeremia 1:5***. Huu ni wito uliowazi sana kutoka kwa Mungu! Hapa hakuna kosa lolote! Yeremia, hakwenda kwa Mungu na kusema: “*nataka kuwa kiongozi!*”! Mungu alimjia Yeremia, alipokuwa bado kijana mdogo. Baadhi ya walimu wa Biblia, wanafikiri kwamba, alikuwa na umri wa miaka **16** tu! Angalia jibu la Yeremia, katika mstari **6**: “*Ah Bwana Mwenyezi Mungu. Mimi sijui kusema, kwa kuwa bado ningali kijana*”. Je, unagundua nini kuhusu jibu lake?

Yeremia kwa kweli hakutaka kuwa kiongozi! Alijaribu kukataa wito wake. Hakutaka kufanya kazi ambayo Mungu alikuwa anampa. Na mara kwa mara, Mungu anaita viongozi, kufanya kitu fulani ambacho hawajisikii kwamba wanaweza kufanya. Yeremia anamwambia Mungu, mimi **sina** sifa za kufanya kazi, unayoniambia kufanya. Kwa kweli, jibu hili ni alama ya kiongozi mnyenyeketu. Angalia kinachotokea mstari **9**: “*Kisha Mwenyezi Mungu akaunyosha mkono wake, akagusa kinywa changu, akaniambia, tazama nimeyatia maneno yangu kinywani mwako. Leo nimekupa mamlaka juu ya mataifa na falme*”.

Hapa ni Mungu akimpa Yeremia uwezo wa kufanya kazi aliyomwitia. Tafadhal kumbuka **hii**: kama Mungu anakuita kufanya kitu fulani kwa ajili yake; kama anakuchagua kwa ajili ya jukumu fulani; kama unajisikia katika moyo wako kwamba, Mungu anakuambia kufanya kitu fulani – ye ye atakuwezesha kufanya hiyo kazi. Yeye atakupa nguvu. Mungu alinyosha mkono wake na kumgusa mdomo wake Yeremia, na kumwambia – ninakupa maneno ya kusema. Ninakuchagua, na kukupa mamlaka. Na tunajua kwamba Yeremia, ingawa ni mdogo, anakuja kuwa kiongozi mkubwa, na mwenye utii katika wito wa Mungu katika maisha yake.

Tufungue kitabu cha **Kutoka 3**, kwa sababu hapa pia, tunasoma kuhusu kiongozi mwengine asie na utayari – lakini ni kiongozi ambaye aliitwa na Mungu. Katika mstari **1**, tulisoma kwamba, **Musa** alikuwa akichunga kondoo jangwani; alikuwa anafanya kazi ya mchungaji. Je, hii inakukumbusha kuhusu nani? Je, unamkumbuka mfalme **Daudi**? Je, alikuwa nani kabla ya kuwa mfalme wa Israeli? Alikuwa mchungaji mnyenyeketu aliyechunga kondoo za baba yake. Alikuja kuwa kiongozi maarufu katika Israeli. Je, umegundua ni viongozi wangapi, katika Biblia walikuwa wachungaji? Wengi sana.

Ngoja turudi kwenye hadithi ya Musa. **Kutoka 3:2** inatuambia kwamba, ghafla, Musa anaona kichaka chenye moto. Na tumeambiwa kwamba, moto haukuwa moto wa kawaida – alikuwa malaika wa Bwana. Musa alienda karibu na hicho kichaka – na kisha, Mungu akamwita: “*Musa, Musa*”. Musa alisema nini? Angalia mstari **4**: “*niko hapa*”. Hili ni jibu la ajabu! Mungu anasema ‘Musa’ – na Musa anasema: “*niko hapa Bwana*”. Ninaweza kufikiri juu ya viongozi wengine wawili, ambaa waliitika kwa Mungu kwa namna hii hii. Mungu alipomwita nabii Isaya, alimwambia: “*Nimtume nani?*” Na Isaya akajibu: “*niko hapa – nitume mimi*”. Mungu alikuwa amegusa maisha yake kwa nguvu ya maono, na Isaya alikuwa na utayari wakuwa kiongozi, kwa ajili ya Mungu.

Wakati **Samweli** alipokuwa mtoto tu, Mungu alimwita usiku, na jibu lake lilikuwa “*niko hapa, sema nami kwa kuwa mtumishi wako anasikiliza*” – na tunajua kwamba Samweli alikuja kuwa kiongozi mwenye nguvu katika Israeli. Jibu la ajabu kwa Mungu! “*Sema nami kwa kuwa mtumishi wako anasikiliza*”. Nina swali. Mungu anaposema nasi; anapotuita kufanya kitu fulani kwa ajili yake – je, jibu letu ni nini? Je, huwa tunajibu kama lile la Musa? “*Niko hapa Bwana*”. Je, huwa tunajibu kama lile la Isaya? “*Niko hapa Bwana, nitume mimi*”. Je, huwa tunajibu kama lile la Samweli? “*Niko hapa, sema nami Bwana, mimi ni mtumishi wako*”. Au, kama tunajua kwamba Mungu anajaribu katuambia kitu fulani, na tunasikia sauti yake ikituita, je, huwa tunakaa kimya? Je, huwa tunajaribu kupuuza, au huwa hata tunakimbia? Je, huwa tunaitikiae Mungu anopotaka kupata usikivu wetu?

Hapa katika kitabu cha **Kutoka 3**, Musa anasema: “*Niko hapa*”. Na tunajua vizuri hadithi. Mungu anamwambia: “*usisogee karibu. Vua viatu vyako, kwa sababu umesimama mahali patakatifu*”. Na kisha, Mungu anaanza kumwambia Musa, kuhusu mpango ulivyo. Anamwambia: “*nimeona mateso ya watu wangu. Nimesikia kilio chao. Nimeguswa na mateso yao. Ninataka kuwaokoa, na kuwatoa utumwani. Nina kazi kwa ajili yako Musa. Ninataka uwe kiongozi wao!*”! Ninakuita, na kukuchagua kwa ajili ya kazi maalumu”. Angalia mstari **10**: Mungu anamwambia: “*Ninakutuma kwa Farao – ninataka uwatoe watu wangu kutoka Misri*”. Hii ni kazi kubwa sana! Je, nani angetaka kazi hiyo? Na Musa anasema nini? Jibu lake ni kama lile la Yeremia.

Angalia mstari **11**: Musa alimwambia Mungu: “*Mimi ni nani hata nipewe kazi hii? Bwana, hii ni kazi kubwa sana mimi siiwezi. Sina sifa zakufanya kazi hii. Chagua mtu mwengine badala yangu*”. Musa ameogopa, kwa sababu hii ni kazi kubwa sana. Jibu lake ni la hofu, lakini pia, ni la unyenyekevu. Hamwambii Mungu: ‘Ninajua kwa nini umekuja kwangu. Mimi ni mtu bora kwa ajili ya kufanya kazi hii. Mimi ni kiongozi mwenye

akili. Hii itakuwa kazi rahisi kwangu”! Hasemi hivyo. Hasemi hivyo kabisa. Alisema: “Wito huu unaoweka katika maisha yangu, haiwezekani kwangu. Ni mgumu sana. Labda utafute kiongozi mwagine”.

Kwa kweli, kama unaangalia sura 4, mstari 10, Musa anatoa kisingizio kama alivyo fanya **Yeremia**: “*Bwana, unajua kwamba mimi si mzuri wa kusema! Si wezi kuhubiri vizuri! Ninapajaribu kuongea mbele za kundi la watu, maneno yangu yanajichanganya. Ninasikika kama mjinga! Hakuna sababu ya kunituma mimi kwa mtu kama Farao*”. Katika mstari 13, anathubutu hata kumwambia Mungu: “*Bwana, tafadhalii mtume mtu mwagine afanye hii kazi!*” Je, umewahi kusema hivyo kwa Mungu? Kazi hii ni kubwa sana kwangu – mtume mtu mwagine. Je, unakumbuka nilicho sema dakika chache zilizopita? Kama Mungu anakuita kufanya kazi fulani kwa ajili yake; kama anakupa kazi ya kufanya; kama unajisikia katika moyo wako, kwamba Mungu anakuambia kufanya kitu fulani: yeye atakuwezesha kuifanya. Hatakuacha peke yako. Yeye atakupa nguvu unazohitaji. Je, Mungu anamwambia nini Musa? Angalia mstari 12: Mungu anasema: “*Nenda. Nitakusaidia kusema na nitakufundisha cha kusema*”.

Mungu hata anamwambia Musa – nitakuwezesha kufanya miujiza mikubwa, mbele za Farao! Ninauhakika kwamba unafahamu hadithi yote. Musa anajaribu kuhojiana na Mungu, na kumwambia atafute mtu mwagine – na Mungu hata anakuwa na hasira juu yake. Mungu anasema: “*Musa, acha kuhojiana na mimi. Nimekuita kufanya kazi hii. Wewe ni mtu niliyekuchagua – lakini nitakupa msaidizi ambaye atakusaidia kuongea*”. Na Mungu kwa upendo, anamwambia kumchukua Haruni aende naye. Lakini, huu ni wito kamili, wa nafasi ya uongozi kwa Musa, kutoka kwa Mungu.

Kuna mfano mwagine ninaotaka kutaja – na safari hii, ni kutoka katika Agano Jipy. Fungua katika kitabu cha **Matendo 9**: Wito wa Sauli. Tena, tunaijua hadithi vizuri, na kwa hiyo, sitatumia muda mwangi, kuangalia hadithi hii. Sauli anasafiri kutoka Yerusalem kwenda Damaski. Huu ni umbali upatao kilometre 200. Katika siku hizo, umbali huu ungechukua kati ya siku 4 hadi 6. Sauli ni farisayo, asiyé wapenda Wakristo! Na anasafiri kwenda Damaski, kwa ajili ya kuwa kamata Wakristo, na kuwaweka gerezani. Lakini, akiwa njiani anakutana na Yesu!

Angalia mstari 3 na 4, katika sura 9: “*Alipokuwa njiani karibu kufika Damaski, ghafla mwanga kutoka angani ulimwangazia pande zote. Akaanguka chini na kusikia sauti ikimwambia: ‘Sauli, Sauli. Kwa nini unanitesa?’*” Kisha Yesu anamwambia kwenda Damaski. Mtu anayetwa Anania, anakutana naye, na kumwombea, na anamwambia Sauli kuhusu anachomtaka Mungu afanye. Angalia mstari 15: Mungu anamwambia Anania: “*Mtu huyu ni chombo kiteule – atahubiri jina langu kwa Mataifa na watu wengine, katika Israel*”. Kwa maneno mengine, nimemchagua kufanya kazi yangu. Amechaguliwa kama mtumishi wa Mungu kuwa kiongozi katika kanisa, na kuhubiri Injili kwa Mataifa. Mungu alimtuma. Sauli alikuwa ameitwa na Mungu, katika namna ya ajabu.

Hii ni mifano 3 ya watu, ambao walikuwa wameitwa, na Mungu wawe viongozi wa kiroho. Yeremia, Musa na Sauli – ambaye baadaye alijulikana kama Paulo. Watu hawa watatu wote, walikuwa na wito kamili, na walikuwa viongozi muhimu sana. Na bila shaka, kuna mifano mingi zaidi katika Biblia. Ngoja nirudie maneno ya Askofu Mtetemela, ambayo niliyasema mwanzo: “*Ni muhumi kwamba, kiongozi anapaswa kujua katika moyo wake, kwamba ameitwa na Roho wa Mungu. Wito unapaswa kuwa wa uhakika katika maisha yake. Ni hatari kwa kanisa kuwa na viongozi, ambao hawakutumwa na Mungu*”.

Ni muhimu kwa viongozi Wakikristo kuwa na uzoefu wa wito. Lakini, je, tunamaana gani tunapotumia neno ‘wito’? Je, tunujuaje jinsi wito, kutoka kwa Mungu ulivyo? Je, unajua katika moyo wako kwamba, Mungu amekuchagua kuwa katika uongozi wa kiroho? Je, unaweza kusema, katika moyo wako, kwamba Mungu amekuchagua kuongoza? Na kama tunahusika katika mchakato wa kuchagua viongozi wengine, je, huwa tunauliza swali la msingi, kuhusu watu hao? Je, tunujuaje kwamba wana wito kutoka kwa Mungu?

Yote haya ni maswali makubwa, na tunahitaji kuyaangalia kwa undani. Kabla ya kuangalia wito wa Elisha, katika kitabu cha **Wafalme wa Kwanza**, ngoja ni wape mifano binafsi, kuwaonesha jinsi Mungu, anavyowaita watu katika majukumu ya uongozi. Baadhi ya hadithi hizi, tunaweza kutusaidia kuona jinsi Mungu, anavyoita watu leo. Mara kwa mara, Mungu anatuita katika namna ya kawaida sana: kadri tunavyosoma Biblia zetu; tunapoomba; tunapofunga; na pia tunapowahusisha watu wengine katika maisha yetu. Ninahitaji kusema jambo muhimu hapa mwanzo. Tuliangalia mifano 3, katika Biblia ya watu ambao walikuwa wameitwa na Mungu – na hadithi hizi ni za ajabu sana.

Paulo aliona mwanga mkali, na alisikia sauti ya Yesu ikimsemesha. Musa na Yeremia walikuwa na mazungumzo na Mungu. Waliisikia sauti ya Mungu, kama jinsi unavyoweza kusikia sauti yangu sasa. Jambo

hatari ni kwamba, tunaweza kufikiri kwamba Mungu lazima atuite kwa namna hii hii, kama alivyowaita watu katika Biblia. Tafadhali usifikiri kwamba, kuwa kiongozi, unahitaji kuitia uzoefu, kama wa hawa watu. Hauhitaji. Baadhi ya watu leo, hupokea wito kwa njia ya ajabu. Inaweza kutokea ghafla. Baadhi ya watu wanawenza hata kuona maono, au kuota ndoto kutoka kwa Mungu.

Watu wachache wamewahi hata kuisikia sauti ya Mungu. Lakini, kwa watu wengi, Mungu anapowaita, inachukua muda mrefu. Inaweza kutokea taratibu na kuchukua miaka michache. Lakini, katika mazingira haya yote, Mungu anapokuita, lazima kutakuwa na msukumu wa hisia wazi ndani yako, kwamba Mungu anakuita kufanya jambo fulani. Ninapenda nukuu kutoka kwa Askofu Mtetemela: “*Ni muhimu kwamba kiongozi, anapaswa kujua, katika moyo wake, kwamba ameitwa na Roho wa Mungu*”.

Ngoja ni wape mifano michache. Miaka **15** iliyopita, nilikuwa na kundi la vijana katika nchi ya Zambia, na kazi ya kikundi ilikuwa karibu kuisha. Tulikuwa tunasubiri kurudi Uingereza, katika muda wa wiki chache. Nilikuwa nikifikiri, na kuomba kuhusu ni fanye nini siku zi jazo. Nilikuwa nikiomba hivi: “*Bwana – naomba unioneshe*”. Siku moja asubuhi, nilikuwa ninasoma Biblia yangu. Nilikuwa ninasoma kutoka kitabu cha **Ufunuo 3**, na baadhi ya mistari iliteka zaidi ufahamu wangu. Maneno yalikuwa halisi! Nilijisikia furaha sana kuhusu mistari hii – lakini ,sikujua kwa nini!

Nilisoma tena na tena, na mapigo ya moyo wangu, yalikuwa yanaenda haraka! Mistari hiyo ilikuwa ni: **Ufunuo 3:7-8***. Hivyo ndivyo ilikuwa - na kwa sababu fulani fulani, kama nilivyosoma, moyo wangu ulipata msukumo - lakini sikujua kwa nini. Siku hiyo baadaye, mkuu wa kikundi, aliniita ofisini kwake. Aliniambia: “*Tunakikundi kingine kinachokuja mwakani, na ninataka uwe kiongozi wa kikundi hicho*”. Na ghafla, akili yangu ikarudi katika kitabu cha Ufunuo, katika mistari niliyokuwa nimesoma asubuhi hiyo. “*Nimekufungulia mlango ambao hakuna auezaye kuufunga*”. Na hapo hapo, nikajua kwamba huyo alikuwa ni Mungu, akiniita kuwa kiongozi wa kikundi kinachofuata. Kumbuka maneno ya Askofu Mtetemela: “*Ni muhimu kwamba kiongozi anapaswa kujua katika moyo wake, kwamba ameitwa na Roho wa Mungu*”. Ninaamini kwamba, Mungu aliongea na mimi wakati nikisoma Neno lake, na nilijua katika moyo wangu, kwamba Mungu alikuwa ananiita kuwa kiongozi katika kikundi kinachofuata.

Katika tukio jingine – Mungu aliniita kwenda katika chuo fulani cha Biblia! Hapakuwa na maono. Hapakuwa na mwanga mkali, wala kichaka kinachoungua moto. Hapakuwa na mistari kutoka kwenye Biblia, lakini katika moyo wangu, nilijua kwamba, Mungu alikuwa ananisukuma, kwenda kwenye chuo hicho cha Biblia, ingawa sikuwa nimewahi kutembela chuo hicho. Ni vigumu kueleza – lakini Mungu alikuwa ananisukuma katika moyo wangu. Nimetumwa kutoka Uingereza kuja hapa Tanzania kama mwalimu wa Biblia. Lakini, kabla ya kuja, nilihitaji kwenda kwenye usaili.

Watu walionifanyia usaili, walitaka kujua, kama nilifikiri kwamba, Mungu alikuwa anatuita kuja Tanzania. Niliweza kusema ‘*ndiyo*’, na ninaamini kwamba Mungu ametuita kwenda. Na kisha, niliwaambia jinsi Mungu alivyotuita. Sina muda wakutoshua kuwaeleza hadithi yote, lakini katika miyo yetu, tulijua kwamba hiyo ilikuwa sahihi – na hapa tunafanya kazi na AIC! Pia Mungu alinionesha, kwa kutumia hadithi ya Elisha, kwamba ilikuwa sahihi kwangu, kukubali nafasi nyingine ya uongozi, katika shirika la AIM. Inafurahisha sana Mungu anapofanya kazi katika njia hii! Najua kwamba Mungu ameniita – na kwamba ni muhimu, hasa maisha yanapokuwa magumu sana. Ninaweza kuangalia nyuma, na kukumbuka wito wangu. Ninaweza kusema – ‘ingawa mambo yanoweza kuwa magumu, ninajua kwamba niko sehemu sahihi - kwa sababu Mungu aliniita’.

Kama unaamini kwamba Mungu amekuita katika nafasi ya uongozi – utatiwa nguvu ya kustahimili nyakati ngumu. Kwa upande mwingine, kama uko katika nafasi ya uongozi kwa sababu ultaka kujisikia wewe ni mtu muhimu, na kama ulipata mchungaji kutimiza matakwa yako, tambua kwamba uko katika kazi hii kwa sababu isiyo sahihi. Na utaona vigumu sana mambo yanapoanza kuwa magumu. Je, uliingia kwenye huduma bila wito kamili, au unajua bila mashaka, kwamba Mungu amekuita? Wewe peke yako ndiye unawenza kujibu swalii hili. Wewe peke yangu.

**“NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU”. KIPINDI 9:
Je, ni sifa gani tunapaswa kuziona kwa kiongozi mwadilifu?
“Kiongozi aliyeitwa” Eliya na Elisha. 1 Wafalme 19:19-21**

Sasa, ninataka tuangalie hadithi ya Elisha na wito wake, kwa sababu ninaamini kwamba, tunaweza kujifunza mambo mengi, kutoka kwa kiongozi huyu mwadilifu. Kwa hiyo, twende kwenye aya fupi, katika kitabu cha **1 Wafalme 19:19-21**. Je, ni kwa namna gani Mungu alimwita Elisha, katika nafasi yake ya uongozi, na tunaweza kujifunza nini kutoka kwenye andiko hili? Utakumbuka kwamba, katika kitabu hiki, Eliya ni nabii mkuu. Ni mtu ambaye ameitwa na Mungu kuwaonya wafalme wa Israeli. Tunaona katika sura **18** kwamba, Eliya ni mtu aliyeutana na nguvu ya upenzani katika Mlima Karmeli. Je, unakumbuka hadithi hii? Eliya aliomba kwa Mungu – na Mungu alishusha moto kutoka mbinguni, ukachoma sadaka ya ng’ombe. Na manabii wa Baali wakauwawa.

Kwa sababu ya tukio hili, **Yezebeli**, mke wa mfalme **Ahabu**, akatishia kumuua Eliya - na kwa hiyo, Eliya akakimbia kwenda kujificha. Kwa kweli, alisafiri karibu kilometer **500** kuelekea upande wakusini, na kuishia kwenye jangwa la Sinai. Ingawa ni nabii aliyeitwa na Mungu, aliogopa sana! Yuko jangwani ambako Mungu anamsemesha. Anamwambia kurudi kaskazini, na anampa kazi tatu za kufanya. Mojawapo ya kazi hizo, ni kumpaka mafuta Elisha kama mtu atakaye mrithi kama nabii mkuu katika Israeli. Kwa hiyo, ngoja tusome kinachotokea katika sura **19:19-21***

Jambo la kwanza, kutambua katika hadithi hii – ni kwamba wakati mwingine, Mungu anapotuita, inaweza kuwa ni jambo la ghafla. Hebu fikiri kuhusu Elisha. Asubuhi hiyo, aliamka, na katika akili yake, alikuwa anapanga kwenda kulima. Na kwa hiyo, alienda shambani, na kuanza kulima kwa plau. Kadri alivyokuwa akilima shambani, hakuwa anajua kwamba kuna, mtu alitembea nyuma yake. Na kisha, ghafla, kanzu ikarushwa kwenye mabega yake! Na bila shaka, Elisha aligeuka nyuma haraka – lakini alichoona, ni mtu akikimbia kukatiza shamba!

Mstari **20**, unatuambia kwamba, Elisha alimkimbia Eliya! Inaonekana kwamba, Eliya hakusimama kueleza mambo hayo kwa Elisha! Kitu pekee alichokifanya ni kurusha kanzu, kwenye mabega ya Elisha, na kisha, kukimbia! Hii ni ajabu sana, siyo? Mungu alipomwambia Eliya kwenda kumpaka mafuta Elisha, hatujaambiwa kama alimwambia Eliya jinsi ya kufanya jambo hilo. Lakini kwetu, kama tunavyosoma aya hii, inaonekana kuwa kitu cha ajabu – na ninahakika kwamba, jambo hili pia ilikuwa la ajabu kwa Elisha.

Hebu tambua jinsi Elisha alivyoitwa na Mungu, kuingia katika nafasi ya uongozi kwa ghafla, na bila kutegemea. Na inaweza kuwa hivyo kwetu, kama Wakristo leo. Mungu anapotuita, inaweza kutokea taratibu kwa muda fulani, au, inaweza kuwa bila kutegemea, na inaweza kutokea ghafla. Kama umetoa maisha yako kwa Kristo, na umejitoo kumfuata yeeye popote anapokuongoza - yeeye anamamlaka ya kukuita kufanya kazi fulani, kwa ajili yake, wakati wowote anaweza kufanya hivyo. Lakini, tambua pia ni jinsi gani wito wa Elisha, ulikuwa katika mazingira rahisi. Ingawa ilikuwa ghafla, ilikuwa katika mazingira rahisi. Eliya yeeye alirusha kanzu tu, juu ya mabega ya Elisha. Eliya hakutoa sauti kwa kelele ‘*hivi ndivyo Mungu anavyosema*’. Hapana. Hapakuwa na radi kutoka mbinguni. Hapakuwa na kichaka kinachowaka moto. Ilikuwa ni alama ya kawaida, lakini yenye nguvu sana, na Elisha alitambua kuwa ni kitu chenye maana kamili. Katika nyakati za Biblia, ukiweka kanzu namna hiyo, juu ya mtu fulani, ilikuwa ni alama ya urafiki. Lakini, katika tukio hili, pia ilikuwa alama ya kwamba, Elisha angechukua nafasi ya huduma ya Eliya - na siyo kanzu yake tu. Kwa hiyo – ilikuwa ni alama rahisi.

Kama nilivyosema mwanzo, usifikiri kwamba kuongozwa na kuitwa na Mungu, lazima kuwe na radi na sauti kubwa. Mara kwa mara, wito wa Mungu katika maisha yetu, hutokea katika namna ya kawaida sana – ni kama kanzu isiyonekana iliyouewka juu yako, ambayo inakushawishi kufuata wazo, kwamba Mungu anakuita kufanya kitu fulani.

Jambo la pili, ninataka utambue kuhusu mwitikio wa Elisha, kwa sababu tunahitaji kufuata mfano wake hapa. Ni jambo la utii. Elisha anagundua kwamba, Mungu anamwita, na anatii. Na kwa hiyo, anafanya nini? Anamuuliza Eliya, kama ni sawa kwake kwenda na kuaga familia yake. Angalia mstari **20**: “*ni ruhusu kwanza niende kumpa baba yangu na mama yangu busu la kwa heri*”. Na bila shaka, mwisho wa mstari **21**, Elisha ni mkweli katika maneno yake, na anamfuata Eliya. Ni mtii katika wito alioweka Mungu katika maisha yake. Sasa, ninatambua kwamba, katika utamaduni huu, watu hawabusiani, mpaka wawe wanandoa. Lakini, katika utamaduni wa Wayahudi, na hata katika utamaduni wa Magharibi, kumbusu mtu unayemjua, ni aina ya salamu inayokubalika - ni kama kushikana mikono kwa hapa Tanzania. Haichukuliwi kama salamu ya kimahaba.

Katika kitabu chake, Askofu Mtetemela anasema kwamba, ‘*utii*’ ni muhimu kwa kiongozi yeote wa Kikristo. Anasema kwamba utii ni moja ya sifa za kiongozi mwadilifu. Unaona kwamba, kuwa mtii inaonesha kwamba, uko tayari kukubali maagizo, na kutii maagizo, kutoka kwa mtu aliye kuchagua. Elisha alikuwa mtii – alikubali wito wa kuwa mrithi wa Eliya. Alikuwa mtii. Katika kitabu cha **Wafilipi 2:4**, mtume Paulo anasema hivi kuhusu Yesu: “*Alijinyenyekesha, na kutii mpaka kufa, hata kufa msalabani*”. Ingawa Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, alikuwa mtii kwa Baba yake, ingawa alipaswa kufa kifo cha maumivu sana, juu ya msalaba.

Yesu alikubali kwamba alikuwa ameitwa kufa. Ndiyo maana Yesu alikuja hapa duniani. Kumbuka kilichotokea katika Bustani ya Gethsemane. Yesu anaomba kwa Baba yake. Anajua kinachokwenda kutoke. Tunasoma kwamba alijawa huzuni. Katika **Mathayo 26:39** inasema hivi: “*Basi akaenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akasali: ‘Baba yangu, kama inawezekana, kikombe hiki kinipite, lakini isiwe nitakavyo mimi, ila utakavyo wewe’*”. Aliogopa maumivu ya msalaba. Hataki kutenganishwa na Baba yake. Katika moyo wake, hataki kufanya hivyo. Lakini, Yesu anasema nini, mwisho wa mstari **39**: “*Isiwe nitakavyo mimi, ila utakavyo wewe*”. “*Baba Mungu, sitaki kufanya hivyo – lakini, kwa sababu umeniambia kufanya hivyo, na kwa sababu wewe unamamlaka juu yangu, nitafanya hivyo*”. Hapa ni mtu, anayejua maana ya utii ni nini.

Je, wewe ni kiongozi mwenye utii? Je, unautii kwa watu wenye mamlaka juu yako? Je, unaishi maisha yako, kama mchungaji au mwinjili, je, wewe ni mtii kwa Neno la Mungu? Kama Mungu anasema katika maisha yako, na anakwambia kufanya kazi maalumu kwa ajili yake - je, utasema nini? ‘*Ndiyo*’ au ‘*hapana*’? Je, utakuwa kama Elisha, na Yeremia, na Isaya, na Paulo – ambao wote walisema ‘*ndiyo*’ kwa Mungu. Wote walikuwa viongozi wenye uadilifu. Je, utakuwa kama wao – au, utakuwa kama nabii Yona, ambaye alisema ‘*hapana*’ kwa Mungu? Mungu alimwita kufanya kazi maalumu kwa ajili yake; alimwita aende Ninevi, lakini Yona hakutaka kwenda, na kwa hiyo, alisema ‘*hapana*’ kwa Mungu, na alijaribu kukimbilia kwingine – lakini, angalia nini kilimpata! Yona alijifunza somo, katika mazingira magumu, na ulikuwa ni uzoefu usio furahisha kwake. Na Mungu alipomwita kwa mara ya pili, Yona alisema ‘*ndiyo*’. Kiongozi mwadilifu, ni yule ambaye anautii kwa wale walio katika mamlaka, na ni mtii kwa Mungu.

Hapa kuna onyo: Utii wakati mwingine una maana ya kujitoa sadaka. Unapokuwa mtii kwa Kristo, na unafanya anachokuagiza, wakati mwingine kuna sadaka ya kulipa. Mara zote utii siyo kitu rahisi. Hii ilikuwa na maana gani kwa Kristo? Kuwa mtii inamaana ya kufa msalabani. Fikiri kuhusu sadaka, ambazo Elisha alipaswa kufanya, alipokuwa mtii katika wito wake. Labda, alimiliki shamba, na ng’ombe wa kulimia. Kwa kweli, tumeambwa katika mstari **19**, kwamba alikuwa na jozi **12** za ng’ombe wa kulimia. Hii ina maana kwamba alikuwa na ng’ombe **24** wa kulimia! Shamba lazima lilikuwa kubwa sana, na ng’ombe hao, walikuwa na thamani ya pesa nydingi. Kama alimiliki hawa ng’ombe, alikuwa mtu taajiri. Inawezekana kwamba Elisha alikuwa na kila kitu alichohitaji. Alikuwa na familia, na marafiki, na maisha mazuri.

Ghafla, kutoka porini, anatokea huyu Eliya nabii mwehu! Mtu huyu Eliya ni muhubiri mwenye nguvu sana. Ni mtu anaye ongea ukweli, na kwa sababu hiyo, ana maadui. Wakati mwingine, unaposema ukweli, unatengeneza maadui. Kumbuka pia, kwamba Eliya alipata kitisho cha kuwawa, kutoka kwa Yezebeli. Alikuwa anawaua manabii wa Bwana! Sasa, hapa ni Eliya anamwambia Elisha kuwa msaidizi wake! Inaonekana kama kazi ya hatari! Lakini Elisha anamtii Mungu. Ingawa itakuwa vigumu, na hatari kufanya hiyo kazi, amejiandaa kusema ‘*kwa heri*’ kwa familia yake, na rafiki zake. Anasema ‘*kwa heri*’ kwa shamba lake! Alikuwa tayari kuacha kila kitu.

Angalia mstari **21**: “*Basi, Elisha akamwacha Eliya, akairudia jozi yake ya ng’ombe, akawachinja ng’ombe hao, na kuwapika akitumia miti ya nira kama kuni, akawapa watu, wakala. Kisha akaondoka, akamuata Eliya na kuwa mtumishi wake*”. Huu ni mstari wa ajabu! Matendo yake yanasema nini? Ninafikiri kwamba Elisha anasema: ‘*sitarudi tena katika hali hii ya maisha. Ninaamini kwamba, Mungu ameniita kuwa nabii, na kwa hiyo, nitajitoa katika nafasi yangu mpya kwa asilimia mia moja*’. Huu ni utii kamili, kwa wito wa Mungu katika maisha yake. Na hivi ndivyo anavyotutaka Mungu tuwe - siyo? Anahitaji utii kwa Wakristo wote. Kama kiongozi – anakutaka uwe mtii na ujitee kwake. Anakwambia kwamba ujitee katika kazi aliyokuitia kufanya – ndiyo maana unahitaji kuwa na uhakika, kwamba kazi unayofanya sasa, ni ile aliyokuitia.

Hatimaye, tambua maneno ya mwisho katika mstari **21**: Ni ya muhimu sana, na kwa kweli, maneno haya yanaturudisha nyuma katika somo tulilokuwa tunajifunza, asubuhi hii, katika Injili ya **Yohana 13**. Elisha amepokea wito wake. Ameitikia kwa utii, na tumeambwa kwamba, “*Elisha akaondoka, akamuata Eliya, na kuwa mtumishi wake*”. Kwa maneno mengine, alikuwa mtumishi wa Eliya. Hebu fikiri kuhusu hii. Ingawa Elisha alikuwa ameitwa na Mungu kuwa mrithi wa Elia, alipaswa kusubiri kwa muda miaka **7**, mpaka alipokuwa nabii wa Israeli. Huu ni muda mrefu! Hatusomi tena kuhusu Elisha, mpaka **2 Wafalme 2**, wakati

Eliya amechukuliwa kwenda mbinguni. Je, Elisha anafanya nini, katika kipindi hiki cha miaka 7? Anamtumika Eliya.

Je, ninajuaje hii? Fungua katika kitabu cha **2 Wafalme 3:11** – huu ni mstari wa ajabu sana! Wakati huu, Elia amekwisha enda, na Elisha sasa ni nabii mkuu. Kundi la wafalme, walikutana pamoja, kwa ajili ya kufanya uamuzi kama watakwenda vitani kupigana na Mfalme wa Moabu. Lakini, kabla ya kuamua, Yehoshafati, mfalme wa Yuda, alitaka kupata ushauri zaidi. Mstari 11*. Inaonekana kwamba, kwa miaka 7, Elisha alikuwa amejitoa kumtumikia Eliya; alikuwa muhudumu wa Eliya. Nafasi aliyokuwa nayo Elisha haikuwa ya kuvutia sana. Haikuonekana kuwa muhimu. Yeye alikuwa mtu aliyetumika tu, ambaye alifanya kazi za chini. Kumbuka tulivyojifunza asubuhi hii, katika **Yohana 13** – Elisha alikuwa kama mtumishi wa chini wa nyumbani, ambaye alikuwa na jukumu la kuosha miguu ya wageni.

Unaona, kwa miaka hiyo 7, ingawa Mungu alikuwa amemwita katika nafasi ya uongozi, Elisha alikuwa akitumika bila kutambuliwa. Hakurukia moja kwa moja kwenye nafasi ya nabii. Alipaswa kuititia muda wa mafunzo. Na aligundua kwamba, Mungu alikuwa anamtayarisha, kwa ajili ya kazi yake ya baadaye. Kwa unyenyekevu, akawa mtumishi, na alifurahi kuosha mikono ya Eliya. Hili ni somo lenye nguvu kiasi gani kwetu! Mungu anaweza kutuita vizuri katika huduma maalumu – lakini, inaweza kuhitaji kusubiri, na kuangalia na kujifunza, na kutumika, kwa sababu inaweza kuwa hatujawa tayari kwa kazi kubwa. Katika muda huo wa kusubiri – tunapaswa kuwa na mtazamo wa unyenyekevu, na kuhudumu, kwa sababu tumeitwa kutumikiana kila moja, na siyo kufikiri kwa ajili yetu wenyewe tu, kama watu muhimu kuliko wengine. Tunapaswa kuwa wachungaji na wainjilisti, na hata maaskofu, ambao wako tayari kuosha mikono ya wengine.

Ngoja niwarudishe nyuma katika maneno ya Askofu Mtetemela – maneno tuliyo anza nayo. “*Ni muhimu kwamba, kiongozi anapaswa kujua katika moyo wake, kwamba ameitwa na Roho wa Mungu. Anapaswa kutamani kuingia katika huduma ya Mungu, ili kumtukuza yeye, na si kwa sababu nyininge ye yeyote. Tunahitaji kuona viongozi, ambao nia yao, siyo kuwa katika nafasi ya uongozi, kwa ajili ya faida yao wenyewe, lakini kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Wito lazima uwe wa uhakika, katika maisha yao*”.

Tumeangalia watu katika Biblia, ambao walikuwa wameitwa na Mungu. Musa, Yeremia, Elisha, na Paulo – na bila shaka, kuna wengine wengi. Viongozi hawa walikuwa watu waadilifu, na ingawa baadhi yao, walikuwa na mashaka mwanzoni, baadaye walikuwa viongozi muhumi sana, na waadilifu. Walikuwa watii katika wito wao. Walikuwa wamejitoa katika wito wao, ingawa walipaswa kujitoa sadaka. Na walikuwa tayari kuwatumikia wengine, kama sehemu ya majukumu yao. Leo katika kanisa, tunahitaji viongozi kama hawa.
Je, utakuwa mmoja wao?

“NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU”. KIPINDI 10:
Je, ni sifa gani tunapaswa kuziona kwa kiongozi mwadilifu?
Kiongozi na Huruma: Huruma kwa maskini na waliopotea?

Katika kipindi hiki, nataka tuangalie sifa nyininge anayopaswa kuwa nayo kiongozi, kama ni kiongozi nzuri. Kumbuka, katika kitabu hiki, Askofu Mtetemela anataja angalau sifa 15 za kiongozi mwadilfu. Wiki hii, hatuna muda wa kutosha kuangalia sifa hizo zote, kwa hiyo, nimechagua sifa 3, ambazo tutaangalia kwa undani. Na sifa ninayotaka tujifunze, katika kipindi hiki, ni huruma. Askofu Mtetemela anasema hivi: “*kama tunataka kufuata mfano wa Yesu, tunahitaji kuwa viongozi wenyewe huruma*”. Ni somo kubwa – kwa hiyo katika sehemu ya kwanza, ninataka kuangalia ‘*hurma kwa maskini*’; huruma kwa wale wanao teseke kimwili. Na kisha, katika sehemu ya pili, tutaangalia kuhusu nini maana ya kuwa na huruma kwa waliopotea; waliopotea kiroho, na hawamjui Yesu Kristo.

Nafikiri kitu cha kwanza ninachohitaji kufanya, nikueleza maana ya neno ‘hurma’. Wote tunalijua neno hili, lakini linamaana gani? Ngoja niwasomee maana chache, kutoka kwenye kamusi: **1:** Kuwa na huruma ni kuwa na shauku ya kusaidia kupunguza, kuondoa matatizo ya wengine. **2:** Huruma ni kuwa na ukarimu maalumu kwa wale wanao teseke. **3:** Kujisikia huruma utufanya kuchukua hatua.

4: Huruma siyo kuhisi kusikitika tu kwa ajili ya mtu fulani, lakini, nikufanya kitu fulani kwa ajili ya mtu mwenye uhitaji. Kwa hiyo, kwa maana hizo katika akili zetu, ngoja tuangalie hitaji la kiongozi, kuwa na huruma kwa maskini, na wale wanao teseke kimwili. Kama unasoma kitabu hiki, utaona kwamba, Askofu Mtetemela anafikiri kwamba, jambo hili ni muhimu sana, kwa sababu anarejea nyakati nyingi. Nitasoma moja ya nukuu zake: “*Kiongozi katika kanisa, lazima awe amejeitoa kikamilifu katika kazi ya kuwasaidia maskini*”.

Kwa nini? Je, kwa nini anafikiri kuwa jambo hili ni muhimu sana? Je, kwa nini anafikiri kwamba, kiongozi katika kanisa lazima awe na huruma kwa maskini? Hii ni sababu yake: Anasema hivi: “*Karibu kila kitabu cha Biblia, kinaongea kuhusu kuwajali maskini. Hili ni hitaji kubwa katika moyo wa Mungu. Katika Biblia kuna zaidi ya mistari 2000 inayo sema kuhusu maskini, na hitaji la kusimama kwa ajili ya haki za maskini. Katika msingi huu, kama Biblia zetu zimejaa mistari inayohusu maskini, hii inamaana, kwamba yeoyote aliyeitwa kumtumikia Mungu, anawajibu wa kuwajali maskini*”. Mungu ana moyo wa huruma kwa maskini na wanaoteseka. Na mfano anaotumia, ni wa Yesu. Ni mfano halisi.

Kwa kweli, Yesu alinukuu unabii kutoka kitabu cha Isaya, na aliutumia yeye mwenyewe na huduma yake. Fungua **Luka 4:18-19***. Na wakati wa huduma yake hapa duniani, Yesu alionesha huruma kwa watu. Alitumia muda kuwa na watu walio tengwa na jamii. Aliwaponya wagonjwa; aliwaponya vipofu; aliaondolea mapepo waliokuwa wamefungwa. Alihubiri habari njema kwa maskini, ingawa ninahitaji kusema kwamba, neno ‘maskini’ linamaana pia ya watu waliokuwa maskini wa roho, pamoja na waliokuwa maskini kimwili. Na kwa kweli, tunaposoma Biblia zetu, tunaona matukio mengi sana, yanaonesha kwamba Yesu alijaa huruma kwa waliokuwa wakiteseka, na waliokuwa maskini.

Hapa kuna mfano mmoja kutoka Injili ya Marko: Hiki ndicho tunachoambiwa katika **Marko 1:40***. Ukoma ni ugonjwa mbaya sana unao haribu neva, ngozi, na macho. Mara zote mtu mwenye ukoma, hypoteza vidole vya mikono, na miguu, na wakati mwingine, hawezi hata kusikia maumivu, kwa sababu neva zimekuwa. Ugonjwa wa ukoma unaweza kuenea kati ya watu - na unatokea sana kwa watu wanaoishi katika umaskini.

Watu walifikiri kwamba ugonjwa wa ukoma, ulikuwa rahisi sana kuenea. Na kwa hiyo, mtu aliyekuwa na ukoma, aliondolewa kutoka familia yake, na kuwekwa katika jamii ya wenyewe ukoma. Katika siku za Biblia, mtu aliyekuwa na ukoma, alichukuliwa kama najisi. Waliondelewa katika jamii zao. Kwa kweli, walipiga kelele katika mitaa: “*mimi ni najisi, mimi ni najisi*”. Walisema hivyo ili kuwajulisha watu wasije karibu yao. Hapa katika Marko 1 kuna mtu maskini, na mgonjwa, na anateseka, na ametengwa na jamii. Anamwomba Yesu kumtakasa. Katika **Marko 1: 40*** ni mstari wa ajabu! Ninafikira kwamba, mtu huyu, alikuwa amefurahi sana! Yesu alijaa huruma, na ilimsukuma kutenda. Na tunahitaji kuwa viongozi wanao sukumwa kwa huruma, kufanya kitu fulani kwa ajili ya maskini na wanaoteseka.

Unaweza kuwa unafikiri mwenyewe – hadithi hizi zote kuhusu Yesu akiponya watu, zinasikika kwa kufurahisha – lakini yeye ni Mwana wa Mungu! Yesu aliposukumwa kwa huruma, alikuwa na nguvu ya kufanya kitu fulani kuhusu jambo hili; alikuwa na uwezo wa kufanya miujiza, na kuwaponya watu. Lakini, mimi siwezi kufanya hayo mambo! Na hii ni kweli. Kwa ujumla hatuwezi kufanya mambo haya, mpaka pale mtu awe na karama ya kuponya. Je, tunaweza kufanya nini kuonesha huruma yetu kwa maskini? Tunaweza kuwa hatuna uwezo wakufanya miujiza, lakini tunaweza kusaidia kwa njia nyingine. Tunaweza kufanya hivyo kama watu binafsi, na pia kama kanisa. Katika kitabu chake, Askofu Mtetemela anasimulia hadithi kuhusu, alivyotiwa changamoto kufanya mambo mengi kwa ajili ya maskini. Hivi ndivyo anavyo sema:

*Nilikuwa nilisoma **Zaburi 113**, na moyo wangu ukajisikia hatia. Niligundua kwamba sikuwa nimewajali maskini, katika huduma yangu. Sikuwa nimewahi hata kufikiri kuhusu changamoto ya umaskini, ambayo watu walikuwa wanakutana nayo, katika jamii yangu niliko ishi. Na kwa hiyo, nilianzisha mpango wa kuwasaidia maskini. Kila mara nilipita katika mji ambaa niliishi, nilikutana na watu katika mtaa, waliokuwa wakiomba angalau kupata chakula chao cha kila siku. Baadhi yao waliokota vitu katika majalala, ili wapate kitu fulani cha kuweka katika matumbo yao, na wengine walijihusisha na biashara ndogo ndogo sana, kujaribu kupata mahitaji yao. Wengine waliuza matunda, maandazi, au nguu zilizotumika. Walizunguka kwenye mji wakiuba vitu hivi siku nzima, katika juu kali. Baadhi yao, waliwabeba watoto wao wadogo kwenye migongo yao. Mwisho wa siku, baadhi yao walikuwa wamepata pesa kidogo katika mikono yao, lakini kulikuwa na wengine ambaa hawakupata kitu chochote. Jambo hili lilinifanya niwaze sana, na niligundua kwamba, hawa ni watu ambaa Mungu anataka kuwatoa katika shida zao. Nilamua kuwasaidia wanawake hawa kwa kuwapa mikopo midogo midogo, na kwa hiyo, nilianzisha kikundi kinachoitwa: “Mama Bahati foundation”.*

Neno ‘bahati’ linamaana ya mtu mwenye bahati nzuri, na hili lilikuwa jina la mwanamke wa kwanza, tuliye msaidia. Nilimpa mkopo mdogo wa shilingi 10,000 kutoka kwenye mfuko wangu. Kwa mkopo huo mdogo, aliweza kuanza biashara. Baada ya miaka michache, biashara yake ndogo ilikua, na ilisaidia kusomesha watoto wake, na baada ya muda, aliweza kujenga nyumba yake mwenyewe! Mkopo huu mdogo, ulimtoa kutoka hali ya chini kwenda juu! Hadi sasa, kikundi cha “Mama Bahati Foundation” kimetoa karibia mikopo 10,000”.

Na hii ni kwa sababu mmoja alipata changamoto, kutoka kwenye Biblia, kufanya kitu fulani kwa ajili ya maskini. Haimaanishi kwamba unapaswa kwenda kufungua kikundi cha kusaidia watu, na kuwapa watu mikopo, lakini inakupa mfano wa kiongozi mmoja, aliyepeata mzigo wa kuwa na huruma kwa maskini. Askofu Mtetemela pia anasema hivi: *“Ninaamini kwamba kiongozi anahitaji kuona kwamba Mungu anaemia, anapowaona maskini”*. Na hii ni changamoto kwetu siyo? Hapa Tanzania, tunaona umaskini umetuzunguka sote.

Watu wengi wanapambana kwa sababu ya umaskini. Watu wengi hawapati huduma za afya, au elimu. Watu wengi wanakwenda kitandani kila usiku wakiwa na njaa, kwa sababu hawawezi kumudu kununua chakula. Watu wengi hawana kazi. Na kuna furusa nyingi sana za sisi kuwasaidia watu. Wakati mwingine mahitaji yanazidi uwezo, na hatujui wapi pa kuanzia. Tunahitaji kuwa na hekima katika kujua wakati gani unafaa kusaidia. Lakini, kama viongozi wa kanisa, tunahitaji kuwa mfano mzuri kwa watu katika kanisa letu. Kama watu wataona kwamba sisi ni viongozi wenyewe huruma, pia watakuwa watu wenyewe huruma. Kama nilivosema mwanzo kwamba, kuna mistari mingi sana katika Biblia, inayohusu jambo hii, lakini ngoja ni nukuu mistari michache. Ninaposoma mistari hii, ninatumaini kwamba itakupa changamoto, na kukugiza kuwa kiongozi mwenye huruma kwa maskini.

Kumbukumbu La Sheria 15:11*. Kwa maneno mengine, uwe na moyo wa kutoa. Nabii Ezekiel ana maneno makali kwa watu, ambao hawakujali maskini. Anatuambia kwamba, sababu mojawapo ya kuharibiwa kwa Sodoma na Gomorah ni kwamba, walikuwa na mtazamo mbaya kwa maskini. **Ezekiel 19:49***. Katika Agano Jipy, tunakumbushwa na Yohana kwamba, kuwa na huruma kwa maskini ni alama ya upendo kwao. **Barua ya kwanza ya Yohana 3:17-18***. Hii ndiyo maana kamili ya huruma. Upendo wenye matendo, kwa watu ambao niwahitaji. Askofu Mtetemela alisema: *“kama tunafuata mfano wa Yesu, tunahitaji kuwa viongozi wenyewe huruma”*.

Lakini kwa sasa, nataka tuhame, na tuangalie sehemu ya pili ya somo letu: *“huruma kwa waliopotea”*. Kiongozi wa Kikristo, anapaswa kuwa na huruma kwa wale wasio mjua Kristo. Kila kiongozi wa kanisa, anapaswa kujihusisha katika umisheni. Wachungaji na Wainjilisti, wanapaswa kuwa na moyo wa kutangaza injili ya Yesu, kwa watu ambao hawajaisikia. Kwa kweli, siyo viongozi tu, lakini Wakristo wote, wanapaswa kujihusisha katika kuwafikia waliopotea. Biblia yote inahusu umisheni wa Mungu. Kutoka Mwananzo, hadi Ufunuo, inatuambia hadithi ya Mungu ya umisheni wa kumkomboa mwanadamu. Agano la Kale linautabiri wa Yesu Kristo, na kisha Agano Jipy, linatuambia kuhusu maisha yake, kifa chake, na kufufuka kwake. Hivi ndivyo Yesu alivyotimiza umisheni wa Mungu.

Na umisheni wa Mungu, ulikuwa ni nini? Barua ya kwanza ya **Yohana 4:9-10***. Mungu alimtuma Mwanaye ulimwenguni, kuleta uzima wa milele kwa mwanadamu. Na njia pekee ambayo mwanaume, au mwanamke, anaweza kuokoka daima, ni kumwamini Yesu. Katika Kitabu cha Matendo kuna mstari unao fafanua jambo hili. **Matendo 4:40***. Hakuna mtu mwingine anayeweza kutuokoa, lakini Yesu Kristo peke yake. Kuna watu wengi sana duniani leo, ambao hawakubaliani na kauli hii. Waislamu watakataa. Wahindu watakataa. Wabudha watakataa. Watu wengi watasema, hakuna njia moja ya kwenda kwa Mungu; kuna njia nyingi tunazoweza kutumia kumfikia Mungu.

Watakuambia kila mmoja yuko katika safari ya imani, ingawa tunatembea katika njia tofauti, hatimaye, njia zote zitatufikisha sehemu moja. Hiyo siyo kweli. Je, naweza kujua? Kwa sababu Biblia yangu inaniambia kwamba, kuna njia moja tu ya kwenda kwa Mungu – na njia hiyo ni kuititia Bwana Yesu Kristo. Hakika, kama hiyo ni kweli, kama viongozi wa kanisa, lazima tushiriki kuwaambia wengine kuhusu msalaba. Kwa kweli, hiyo ndiyo kazi tuliopewa kufanya. Ndiyo maana kanisa lipo. Kabla ya Yesu kupaa kwenda mbinguni, alikabidhi utume wake kwa wanafunzi wake. Katika **Yohana 20:21** aliwaambia: *“Kama Baba alivyonituma, hivyo hivyo nami nawatuma ninyi”*. Anawaita kuchukua kazi, lakini pia aliwaelekeza alichotaka wafanye. Je, unakumbuka alichosema katika **Mathayo 28?**

Wanafunzi kumi na moja walikutana pamoja na Yesu, katika mlima huko Galilaya - na hii ndiyo amri yake ya mwisho kabla ya kuwaacha. *“Nendeni basi, mkawa fanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu,*

mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na Roho Mtakatifu. Wafundisheni kushika maagizo yote niliyowapeni". Hiyo ni kazi aliyowapa mitume. Na katika kitabu cha Matendo, tunaona jinsi mitume walivyoanza kuifanya kazi hiyo.

Lakini mstari huu katika Mathayo, si kwa ajili ya mitume tu. Amri ya Yesu si kwa ajili ya wale watu kumi na moja tu. Ni kwa ajili ya sisi sote – na kanisa lote katika historia. Yesu alilambia kanisa kuchukua kazi ya kueneza injili, na kuwafikia waliopotea. Kama hiyo ndiyo kazi ya kanisa, ye yote aliyeitwa kuwa kiongozi katika kanisa, ameitwa kulisa idia kanisa, kufanya utume huu mkuu wa Bwana wetu Yesu. Tuna wajibu kwa Yesu Kristo. Tunapaswa kuwa viongozi wenye huruma kwa waliopotea. Tunapaswa kuwa viongozi wanaowaambia wengine habari njema.

Hadithi kuhusu Hudson Taylor:

Ni hadithi yenye nguvu sana. Je, unaona fundisho analo jaribu kufanya? Kama Wakristo, na kama viongozi katika kanisa, tunaamini kwamba msalaba wa Yesu ni habari njema, kwa waliopotea. Tunaamini kwamba kuna njia moja tu, ya mtu kuokoka. Tunajua kwamba kama watu wataamini injili, wataokoka kwenda jehanam. Tunajua kwamba hii ni kweli. Tunashikilia nyavu, na tunaweza kuzirusha kwao – lakini, je, tunazirusha nyavu, ili kuwaokoa watu wasizame? Je, tunawaambia watu habari njema ya injili, au tunakaa tu kwenye makanisa yetu; tukiimba nyimbo zetu; na kuangalia kwaya zetu zikicheza, na hatujisumbui kuwaambia wengine habari njema?! Yesu alitoa maelekezo kwa kanisa: "Nendeni mkafanye wanafunzi". Waambie watu ni jinsi gani wataokoka. Rusha nyavu ambazo zinaweza kuwaokoa, kutoka kwenye kifo cha kiroho. "Huruma kwa waliopotea".

Fungua nami katika kitabu cha **Mathayo 9:35-38***. Angalia kinachotokea katika mstari **36**, wakati Yesu anapowaona makutano ya watu. "Alikuwa na huruma kwao". Katika lugha ya Kigrika, neno lililotumika kuwakilisha 'huruma', ni neno sawa na 'tumbo'. Sasa, hii inaweza kuwa jambo la ajabu, lakini hebu fikiri kuhusu hili. Yesu anapowaona makutano, inamaana kwamba ameguswa ndani ya tumbo lake. Hii ilikuwa ni zaidi ya kujisikia huruma kwa ajili yao. Hii ni huruma, aliyojisikia ndani yake, yani hapa kwenye tumbo. Alicoona hakikugusa akili yake tu, ni kitu kilichomwacha katika maumivu ya mwili. Je, kinatokea nini unapopiga kwenye tumbo? Unaumia. Unalia. Kwa sababu pumzi imesukumwa nje. Na jinsi hiyo hiyo, Yesu alipowaona watu hawa, ni kama aligongwa kwenye tumbo lake.

Lakini, tambua kwamba, hii ni huruma, ambayo macho ya nyama hayawezi kuiona. Yesu haangalii katika hali yao ya kimwili, lakini, anaona hali yao ya kiroho. Anaangalia makutano, si kwa macho ya kimwili, lakini kwa macho ya kiroho. Tunajua kwamba Yesu, aliguswa kuhusu hali ya watu ya kimwili. Tayari katika sehemu ya kwanza ya semina hii, tumeona kwamba Yesu, alikuwa na huruma kwa maskini na wagonjwa. Na kama, unaangalia mstari **35**, utaona kwamba, Yesu: "alitembelea miji na vijiji akiponya magonjwa yote, na udhaifu". Aliwajali kimwili, na katika huruma yake kwao, aliwaponya baadhi yao. Lakini, tambua pia katika mstari **35**, kwamba Yesu, alihubiri habari njema, na alifundisha katika masinagogi. Alikuwa na huruma kwa waliokuwa maskini na wagonjwa, lakini pia aliguswa na hali yao ya kiroho. Je, Yesu anaona nini, anapowaangalia makutano?

Angalia mstari **36**. Watu wanaelezwa kama: "Wario hoi na wenge wasiwasi, kama kondoo wasio na mchungaji". Akiangalia kwa macho yake ya kiroho, Yesu aliona maelfu ya watu, ambao walikuwa wamepotea kiroho, na hawana msaada, na ambao hawakuwa na wachungaji wa kuwa linda, au kuwajali – na alisukuma kwa huruma. Ndani, anaumia kwa ajili yao. Kuna mstari mwingine kama huu katika Biblia. Ni mstari unao waelezea watu wa Israeli, katika namna hii hii. Miaka **850** iliyopita, kabla ya mstari huu wa kitabu cha Mathayo, kulikuwa na nabii, aliyeitwa Mikaya. Hatujui sana kuhusu nabii huyu, lakini tunajua kwamba, alikuwa nabii wakati ule ule wa Eliya na Elisha.

Katika **Wafalme wa Kwanza 22:17** Mikaya anasema hivi, kwa mfalme wa Israeli: "Niliwaona watu wa Israeli, wamesambaa katika kilima, kama kondoo wasio na mchungaji, na Bwana Mungu akasema, watu hawa hawana bwana". Je, anasema nini kwa mfalme? Mikaya anamkemea viongozi wa dini, kwa kwa sababu yakushindwa kuwaongoza watu wake. Anasema: "hakuna ye yote anaye waangalia watu wake kiroho. Hakuna anaye waongoza, au kuwalinda. Wamekuwa kama kondoo, katika milima wasio na mtu wa kuwaongoza". Miaka **850** baadaye, wakati wa Yesu Kristo, hali ilikuwa bado iko vile vile. Watu waliendelea kukosa msaada wa kiroho na kupotea. Mafarisiyo na walimu, walipaswa kuwa wachungaji wa watu, lakini hawakuwa wanaangalia maisha yao ya kiroho, hawakufanya chochote kuwaandaa watu, kwa ajili ya ujio wa Mesia. Katika Injili, hii ni moja ya sababu ya Yesu, kuwa kemea mafarisiyo mara kwa mara, kwa sababu walikuwa hawafanyi kazi vizuri kama viongozi.

Yesu anapoangalia katika kundi hili kubwa la watu, anawaonea huruma, kwa sababu katika upande wa kiroho, wamepotea, na hawana msaada, na hakuna yeoye anaye waandaa, kwa ajili ya ujio wa Mesia. Nina swali kwako. Kama mchungaji au mwingjilisti, je, una huruma kwa waliopotea kiroho? Je, unakumbuka ulipojisikia huruma kubwa ndani yako, kwa mara ya mwisho kwa ajili ya mtu fulani, kwa sababu hakumjua Yesu? Tunapowaona kupitia macho ya Yesu, tutagundua kwamba ni watu walioseka na hawana-msaada, na wanahitaji msaada wa kuokolewa. Na bado, mara kwa mara, ni vigumu sana, kuwa na huruma kwa kitu ambacho hatuwezi kukiona, siyo? Tunaweza kuona mateso ya kimwili. Tunaweza kuona umaskini. Tutaweza kuona mahitaji kwa macho yetu wenye – lakini inapokuja katika hali ya roho ya binadamu, ni vigumu kuona.

Bado kuna mamilioni ya watu, ambao wanakuwa, bila kumjua Yesu. Wengi wao hawajawahi kusikia, wamba Yesu alikuwa kwa ajili yao. Sikiliza takwimu hizi – na uziruhusu kuzama katika kichwa chako. Idadi ya watu, wasiofikiwa na injili ulimwenguni hadi sasa, ni kama ifuatavyo: Waislamu: milioni **865**. Wahindu: milioni **550**. Wabudha: milioni **275**. Makabila yenye imani za asili zaidi ya **2500**, ambao jumla yao, ni watu milioni **140**. Watu ambao hawaja wahi kusikia Injili. Je, tunajisikiaje kuhusu jambo hili? Baadhi ya watu hao, wanaishi katika jamii zetu. Je, tunaguswa kwamba watu hawa wanakwenda jahanamu? Je, tunahuruma kwa watu hawa, ambao wamepotea katika jamii zetu? Je, tunafanya nini kuhusu jambo hili, katika makanisa yetu? Kama kiongozi, je unajaribu kulisaidia kanisa lako kuwafikia waliopotea? Je, unatenda kwa huruma kwa wale wasiomjua Kristo?

Tambua anachosema katika mstari **37***. Watu wengi leo wanajaa ya kiroho. Wengi wao wanamtafuta Yesu, lakini hakuna watu wakutosha, ambao wanautayari wa kuwaonesha njia ya kwenda kwa Yesu. Ni mavuno mengi sana. Matunda yako tayari. Yanasubiri kuvunwa tu. Lakini, hakuna wakulima wakutosha kufanya kazi hii, na kwa hiyo, matunda yanaharibika, na kufa - bila ya kuvunwa. Na ndiyo maana Yesu anasema: “*Mwombeni Mungu ili alete watenda kazi zaidi*”. Mwombeni Mungu ili alete watu, ambao wanahuruma kwa watu walipotea. Na ninafikiri kwamba, hii ni sala ambayo tunahitaji kuomba zaidi na zaidi. Najua kwamba baadhi yenu, mnajihuisha katika kusaidia kuwafikia walipotea. Najua kwamba, baadhi ya makanisa hata hutuma wamisionari, lakini tunahitaji zaidi na zaidi watu, katika kanisa la Tanzania, wawe na huruma kwa walipotea. Kwa kweli, tunahitaji zaidi na zaidi watu, katika ulimwengu wazidi kuwa na huruma, kwa walipotea. Na jambo hili linaanza na kiongozi. Kama kiongozi hana huruma kwa walipotea; je, ni namna gani watu, katika kanisa, watajisumbua kwa jambo hili?

“*Alipowaona makutano, Yesu alikuwa na huruma juu yao, kwa sababu walikuwa wameteseka, na hawakuwa na msaada, kama kondoo wasio na mchungaji*”. Mungu aguse miyo yetu, na atufanye kuwa wachungaji na wainjilisti, wenye huruma kwa maskini, na walipotea pia. **Hii ni alama ya kiongozi mwadilifu.**

“NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU”. KIPINDI 11: “Majaribu ambayo humkibili kiongozi”

Kuna sura **7** tu katika kitabu hiki – lakini moja wapo ya sura hizo inazungumzia habari za majaribu kwa kiongozi. Kwa hiyo, ninafikiri tunaweza kusema kwamba, Askofu Mtetemela anahisi kwamba hili ni somo muhimu kujifunza. Kila mtu katika chumba hiki amewahi kujaribiwa kufanya jambo baya – na ninaweza kusema kwamba, kila mmoja katika chumba hiki, amewahi kuanguka kwenye majaribu, na kufanya jambo baya. Sisi sote ni binadamu, na kwa hiyo, sote tu wenye dhambi, ingawa tu Wakristo. Lakini tunapaswa pia kuelewa kwamba, viongozi wa Kikristo wako kwenye mtego wa Shetani. Anataka kuona wachungaji wakianguka. Anataka kuona wainjilisti wakianguka dhambini. Anataka kuona viongozi wa kanisa wakifanya makosa makubwa – ili kwamba huduma na makanisa yaanguke.

Tangu Shetani alipowajaribu **Adamu na Hawa**, katika Bustani ya Eden, amekuwa akifanya kazi ya kuwajaribu wanaume na wanawake; wachungaji na wainjilisti; maaskofu na viongozi; wanasiasa na marais. Hiyo ni kazi ya Shetani. Yeye huwajaribu watu kufanya ubaya, na kumwasi Mungu. Kwa kweli, mtume Petro anatuonya kuhusu mpango wa Shetani. Barua ya **1 Petro 5:8-9**: “*Muwe na kiasi na kukesha*”. Kwa nini? “*Adui yenu Shetani anazunguka zunguka akiunguruma kama simba, akitafuta mtu ammeze*”. Na ushauri wa Paulo ni huu “*Mpingeni Shetani, mkiwa thabiti katika imani*”.

Picha iliyopo hapa, ni ya simba aliye katika mawindo yake, na akitafuta kuua chakula chake. Kwa jinsi hiyo, Shetani anatafuta kukuangusha. Anataka uanguke. Anataka kuharibu huduma yako, na atajaribu

kufanya hivyo kwa kukujaribu ufanye kitu fulani kinyume na Neno la Mungu. Nina uhakika kwamba sote tumewahi kusikia kuhusu wachungaji, na maaskofu, ambao wameanguka katika majaribu, na matokea yake kila kitu kikaharibika. Katika kitabu chake, Askofu Mtetemela ameandika kama maeneo **6** ya majaribu, ambayo anafikiri kwamba, yanaweza kumkabili kiongozi, iwe katika siasa, biashara, au katika kanisa. Na kwa hiyo, zifuatazo ni mada ambazo tutaangalia: **1:** Jaribu linalokuja kwa sababu ya umaarufu. **2:** Jaribu la pesa na utajiri. **3:** Jaribu la uzinzi. **4:** Jaribu la kulipa kisasi kwa adui zako. **5:** Jaribu la ulevi. **6:** Jaribu ya uchawi na ushirikina.

1: Umaarufu na matumizi mabaya ya mamlaka. Ninafikiri kwamba, hili linawahuhusu sana watu walio katika siasa. Unapokuwa maarufu na kujulilkana sana, vyombo vyahabari huanza kukuzunguka. Watataku kuchukua picha yako. Watu wataanza kuzungumza kuhusu wewe. Utapata mialiko katika matukio mbali mbali, na kila mmoja atakuangalia. Wataanza hata kukuhudumia kama mtu maalum sana. Na watu wanapokuwa maarufu hupenda hadhi hiyo na kutaka iendelee. Mienendo ya maisha yao ni mizuri, na kila mtu atajaribu kufanya kitu fulani kwa ajili yao.

Baadhi ya viongozi hulewa umaarufu, kwa hiyo huwa hawataki kuachia nafasi zao. Na kwa hiyo, watafanya chochote ili kupanua nafasi zao za uongozi. Na mara kwa mara, katika nafasi ya mamlaka huja kiburi na majivuno. Kiongozi anaweza kuanza kufikiri kwamba, yeye ni mtu maalum sana, na kwamba yeye ni muhimu kuliko watu wanaomzunguka. Wanaanza kujisikia kwamba wanahaki ya kukaa katika meza kuu. Hii hutokeea katika ngazi zote za uongozi ulimwenguni. Lakini inasikitisha kwamba, hii inatoka pia katika kanisa. Katika kitabu chake, Askofu Mtetemela anasema hadithi ya muhubiri mmoja wa Kitanzania, ambaye alijulikana sana. Alikuwa amealikwa kuhubiri katika mukutano – lakini alipoona kwamba, angekuwa muhubiri wa pili, na siyo wa kwanza, alikataa kuhubiri! Kwa sababu alijulikana sana, na kwa sababu alifikiri kwamba, yeye alikuwa muhimu kuliko yule muhubiri mwengine, alifikiri kwamba ilikuwa haki yake kuwa muhubiri wa kwanza. Umaarufu na kiburi vilikuwa vimeingia katika kichwa chake!

Kwa muhubiri wa injili; kwa mchungaji, kwa Askofu - hii ilikuwa inatia aibu! Je, ushauri wa Paulo ulikuwa nini katika somo hili? **Warumi 12:3** “*Ninasema kwa kila mmoja wenu, msiwaze makuu kuliko iwapasavyo, lakini fikira zenu na ziwe na kiasi kadri ya kipimo cha imani*”.

Kujulikana sana, na kuwa maarufu, inaweza pia kumaanisha kwamba, kiongozi anaweza kujaribiwa kutumia vibaya mamlaka yake. Mfano wa jambo hili ni mfalme **Daudi**. Alitumia cheo chake cha mamlaka, na umaarufu wake, kumchukua **Bathsheba**. Alikuwa mke wa mmoja wa askari. Tunafahamu hadithi hii. Alimwona mwanamke huyu mzuri. Akaamuru watumishi wake kwenda kumchukua. Akalala naye, na kisha alipopata ujauzito, Daudi akafanya mpango wa kumuua mumewe **Uria**. Daudi alifanya hivyo kwa sababu alikuwa mfalme, watu walitii amri zake. Alijua kwamba, kama angewaambia watumishi wake kufanya jambo lolote, wanetii. Alitumia vibaya nafasi yake ya madaraka, ili kutimiza tamaa zake.

Swali la kujuliza sisi wenye, ni hili: Je, tumetumia mamlaka tuliyopewa na kanisa, kwa ajili ya kuwa tumikia wengine kwa uaminifu, au tumetumia nafasi zetu za uongozi kutimiza tamaa zetu? Katika **1 Petro 5:2-3**, mtume Petro alitoa ushauri huu kwa wazee, na wachungaji: “*Muwe wachungaji wa kundi mlilopewa na Bwana, mlitunze si kwa kulazimika, bali kwa hiari kama atakavyo Mungu. Fanyeni kazi hiyo si kwa tamaa ya fedha, bali kwa moyo wenu wote*”. Na kisha, hasa katika mstari **3** – sikiliza maneno haya : “*Msiwatawale kwa mabavu hao, waliowekwa chini ya ulinzi wenu - bali muwe mfano kwa hilo kundi*”. Kwa maneno mengine, msiwatawale kwa nguvu walio chini yenu. Msiwatumie kama fursa – lakini badala yake, watumikieni kwa hiari.

2: Jaribu la pili ambalo huwakabili viongozi ni hili: **Tamaa ya pesa na utajiri**. Labda hili ni jaribu kubwa sana, kwa viongozi wa kanisa leo. Je, ni mara ngapi tunasikia kwamba pesa zimetumiwa vibaya, kwa sababu watu walio katika madaraka, wamejaribiwa kuiba. Inatoka mara kwa mara. Ngoja tuweke wazi jambo hili – katika baadhi ya makanisa, hapa Tanzania, na ulimwenguni pote, wachungaji huwaibia watu wao. Baadhi yao hukusanya pesa nyingi kuitia sadaka. Wamechukua hizo pesa kwa ajili yao wenye, na kuwa matajiri sana. Baadhi yao wamejulikana, na kukamatwa, na kupelekwa mahakamani. Baadhi yao wako gerezani, na wengi wao wamepoteza ushuhuda wao, huduma zao, na ndoa zao.

Tatizo la pesa, linaweza kuteka moyo, na kwa hiyo watu huwa na kiu zaidi ya kupata pesa, katika maisha yao. Na hufikia hatua ambapo hufikiri kwamba, pesa na utajiri, ndiyo kila kitu katika maisha yao. Huwa wanaanza kwa kuiba kidogo kwanza, na kama hakuna mtu anayegundua, wanajaribu tena. Na baada ya muda mrefu, wanaiba kiasi kikubwa, hadi kufikia hatua ambapo hawawezi kuacha. Inakuwa kama ulevi kwao. Wanataka zaidi na zaidi. Katika **1 Timotheo 6:9-10** Paulo anatuonya kuhusu jambo hili*. Kama mchungaji, unapaswa kulinda moyo wako zidi ya jambo hili.

Kila mara huwa ninashangaa, ninaposoma katika Injili kuhusu **Yuda Iskarioti**. Alikuwa mtu ambaye alikaa na Yesu, pamoja na wanafunzi wengine kwa muda wa miaka 3. Alikuwa amesikia mafundisha ya Yesu. Alihusika katika huduma, lakini bado tunajifunza kwamba, mwanafunzi huyu alikuwa mwizi! Je, unaikumbuka hadithi hii katika injili ya **Yohana 12**? Siku chache tu kabla ya Yesu kwenda msalabani, Mariamu alikuwa amemimina pafyumu ya gharama kubwa, juu ya miguu ya Yesu. Lakini kulikuwa na mwanafunzi mmoja, ambaye hakuwa na furaha na jambo hilo - Yuda Iskarioti. Je, unakumbuka alisema nini? “*Kwa nini pafyumu hii haikuuzwa, na pesa wakapewa masikini. Ilikuwa na thamani ya ujira wa mwaka mzima!*” Pesa nyingi sana.

Katika injili ya **Yohana 12:6** tumeambiwa kwamba: *Yuda hakusema maneno hayo kwa sababu aliwajali masikini, lakini kwa sababu alikuwa mwizi. Kama mtunza mkoba wa fedha, alikuwa akiiba kutoka kwenye mkoba huo wa fedha*”. Hivi ndivyo Yohana anavyotuambia. Unaona, inaweza kutokea katika kanisa. Inaweza kutokea katika kundi la watu, hata wale ambao hutumia muda kuwa pamoja na Yesu! Yuda alipenda sana pesa, ndiyo maana alikwenda kwa viongozi wa Kiyahudi, na akakubali kupokea pesa ili amsaliti Yesu, na alipokea vipande thelathini nya fedha kwa ajili kumsaliti Yesu. Tamaa ya pesa inaweza kuwafanya watu watende mambo maovu.

Mwandishi wa barua kwa Waebrania, anasema hivi: “*Msiwe watu wakupenda fedha; toshekeni na vile vitu mlivyo navyo*” (**Waebrania 13:5**). Ni jukumu la kiongozi kuonesha mfano mzuri katika jambo hili, na tunapaswa kuwa makini na hatari hii. Ngoja niwape mfano wa kiongozi katika Biblia, ambaye alikuwa mwadilifu sana. Na kiongozi huyo ni **Nehemia**. Alikuwa kiongozi, ambaye hakutumia mamlaka yake kwa ajili ya kujitajirisha mwenyewe. Katika **Nehemia 5:14-15***. Huyu alikuwa kiongozi mwenye mamlaka makubwa sana, lakini hapakuwa na rushwa katika maisha yake. Hakuwa mtu aliyetaka kukusanya pesa nyingi kutoka kwa watu wake.

Je, wewe ni kiongozi wa aina gani, inapofika kwenye swala la fedha na utajiri? Je, uko kama **Nehemia** - au uko kama **Yuda Iskarioti**? Je, siku za nyuma, umewahi kujaribwa kuchukua fedha ambazo siyo zako? Je, hili ni jambo linalokusumba kwa sasa? Labda, ni swala gumu sana kwako, na labda unahitaji kuwa mwaminifu kuhusu jambo hili. Kama kiongozi katika kanisa, unapaswa kuonesha mfano mzuri kwa watu wako, na unapaswa kuepuka tuhuma katika eneo hili. Kama unatunza pesa katika kanisa, Je, huwa unakanuni ambazo hutumika kuhesabu pesa zote za kanisa? Je, ni mtu mmoja tu, hutunza fedha katika kanisa lako? Kama ni hivyo – hiyo ni hatari. Hakikisha kwamba unawajibika.

3: Jaribu la uzinzi: Hili ni jambo kubwa sana kwa viongozi, na ni jaribu jingine ambalo Shetani hulitumia katika vita yake zidi ya wachungaji. Na huwa tunasikia kuhusu wachungaji, ambao wameanguka katika aibu kwa sababu ya dhambi ya uzinzi. Uzinzi ni jambo ambalo hutokea katika angazi zote za jamii. Watu walio oa, au kuolewa, hudanganya kwa waume na wake zao, na huwa wanafanya mapenzi na watu wengine inje ya ndoa zao. Watu ambao hawajaoa, au kuolewa, hufanya uasherati na kucheza michezo ya hatari. Na kisha, kuna matumizi mabaya ya swala la kufanya mapenzi. Katika nchi nyingi za magharibi, vitendo vya ushoga sasa, vinachukuliwa kama tabia ya kawaidal! Watu wawili wa jinsia moja, sasa wanaruhusiwa kuoana! Shetani amekuwa akifanya kazi kwa bidii – na inasikitisha kuona tabia kama hizo zikipewa kibali.

Biblia inaweka wazi kwamba, mambo yote niliyoyataja ni batili, na hayapaswi kufanywa na watu wa familia ya Mungu. Katika **1 Wakorintho 6:18**, Paulo anatuambia hivi: “*Jiepusheni na uzinzi*”. Tunapaswa kuukimbia uzinzi haraka kadri tuwezavyo. Alipokuwa akiandika kwa kanisa la **Efeso**, Paulo alisema hivi: “*Kwa vile nyinyi ni watu wa Mungu, basi uasherati, uchafu wowote ule au choyo visitajwe kamwe mionganoni mwenu*”. **Waebrania 13:4***. Uzinzi ni mbaya sana. Unaona, hili siyo tatizo ambalo linatuathiri sisi tu leo. Lilituwa tatizo ambalo liliathiri kanisa katika Agano Jipyia pia – katika maeneo kama Roma na Korintho. Uzinzi lilikuwa tatizo katika Agano la Kale pia. Na vile vite katika kitabu cha **Kutoka**, na **Mambo ya Walawi**, Mungu ametoa sheria nyingi sana kuhusu jambo la uzinzi. Moja ya amri kumi za Mungu, inasema hivi: “*Usizini*”. Hakuna kitu ambacho hakieleweki hapa – iko wazi sana.

Ndoa ni muhimu sana kwa Mungu, na kwa hiyo, viapo vya ndoa vinapovunjwa, na watu wakaingia katika uzinzi, husababisha maumivu mengi sana mionganoni mwa wanafamilia. Na pia inamchukiza Mungu. Ni wazi kwamba, mtu anaposhindwa kuzuia jaribu hili, na kuanguka katika dhambi ya uzinzi, matokeo yake yanaweza kuwa mabaya sana katika familia. Maisha ya kiongozi huyo, aliyеanguka katika jaribu hili, hayatakuwa tena kama yale ya zamani. Mahusiano yataharibika. Huduma itaharibika, na makanisa yataharibika, na jina la Yesu Kristo, litachafuliwa.

Nini kilimpata mmoja wa viongozi wa Israeli – **Samsoni**. Kitabu cha **Waamuzi** kinatuambia kwamba, alikuwa amefanikiwa kwa mambo mengi kama kiongozi. Chini ya uongozi wake, Israeli waliweza kuwashinda Wafilsti. **Waamuzi 13:25**, inasema kwamba, kama kijana mdogo, “*Mungu alimbariki na Roho ya Bwana, akaendelea kukaa ndani yake*”. Alikuwa na nguvu sana kimwili. Hata tunasoma kwamba, aliweza kumpasua simba, kwa mikono yake! Katika tukio jingine, alikuwa akipigana na wanaume **30** wa Kifilsti, na akawatupa chini! Mtu mmoja - akipigana na watu **30** – na bado akawashinda! Pia katika tukio jingine aliwaua wanaume **1000!** Je, unajua alitumia kitu gani kama silaha yake? Mfupa wa punda!

Na kisha, katika siku za mwisho wa maisha yake, alipokuwa amekamatwa na Wafilsti, aliweza kubomoa jengo kubwa sana, kwa mikono yake tu. Alikuwa mtu mwenye nguvu sana, lakini pia, alikuwa na udhaifu mkubwa; wanawake. Inaonekana kuwa aliweza kujaribiwa na wanawake kwa urahisi. Alianguka, kwa sababu alimpenda mwanamke kahaba wa Kifilsti, aliyeitwa **Delila**, ambaye alimshawishi, na kisha akamsaliti. Na kwa hiyo, kwa kushindwa kupinga jaribu la uzinzi, alishindwa kutenda kama mtu mwenye hekima, na akapoteza nguvu zake za kimwili na kiroho.

Vipi kuhusu mfalme **Solomoni**? Kama kiongozi alianza vizuri sana. Alipokuwa mfalme wa Israeli, alimwomba Mungu ampe hekima, ili kwamba aweze kuwa kiongozi mzuri. Lakini baada ya muda – mambo yalianza kwenda isivyo. Kwa nini? **Uzinzi**. Ingawa Mungu alikuwa amemkataza kuoa wanawake wa mataifa, Solomi aliamua kutomtii Mungu. Katika **1 Wafalme 11**, tumeambiwa kwamba, Solomoni: “*alipenda wanawake wengi wa mataifa*”. Pia tumeambiwa kwamba, “*alikuwa na wake mia saba, na vimada mia tatu*”! Na matokeo yake ni nini? Ngoja ni some **1 Wafalme 11:4***. Dhambi hizi ziliharibu uadilifu wake, na hii ilikuwa na matokeo mabaya kwa taifa zima. Mungu hakupendezwa na alimwambia Solomoni: “*Kwa sababu haukutii sheria zangu, nitakuondolea ufalme wako*”. Na tunajua kwamba, baada ya Solomoni kufa, taifa la Israeli likagawanyika, na vita vya wao kwa wao vikaanza. Yote hayo ni kwa sababu ya mtu mmoja, ambaye alishindwa kuzuia jaribu la uzinzi.

Jaribu la uzinzi, ni jambo kubwa sana katika ulimwengu, na katika kanisa, hasa kwa vijana. Na bado, jambo hili halizungumziwi vya kutosha katika makanisa yetu. Je, hili ni somo, ambalo huwa unafundisha katika kanisa lako? Vipi kuhusu vijana katika kanisa lako? Je, huwa wanapata ushauri kutoka wapi? Je, huwa wanapata ushauri kutoka kwa watu wa dunia, au kutoka mitandao ya kijamii – au kutoka kanisani? Tafadhali, tuhakikishe kwamba, sisi ni viongozi amba ni mfano mzuri kwa watu wetu, na tuwaonye wengine kuhusu hatari ya uzinzi. Kumbuka, Shetani hutumia jaribu hili kama moja ya silaha zake kubwa dhidi ya viongozi.

4: Ushirikina na uchawi. Unajua vizuri kuliko mimi kuhusu jambo hili, kwamba katika Afrika, ushirikina, ibada za mababu, na uganga hufanya sana. Baadhi ya watu wanaweza kwenda kwa mganga wa jadi, kwa sababu wanataka ulinzi katika maisha yao. Wengine huenda kupata uponyaji wa magonjwa, na wengine huenda kupata nguvu katika maisha yao, ili kwamba waweze kufanikiwa zaidi. Kama utasoma magazeti, mara kwa mara uthaona taarifa za watu, amba hufanya hivyo. Katika ulimwengu wa wanasiwa wa Kiafrika, wakati mwingine, utasikia kuhusu Maraisi, amba huenda kwa waganga, kwa sababu wanafikiri kwamba watawasaidia kushinda uchaguzi.

Baadhi yenu mtakuwa mmeona **Kamusi ya Biblia ya Afrika** – ambayo imeandikwa na wasomi na wachungaji kutoka Afrika. Na ndani ya kamusi hiyo, kuna jarida kuhusu ushirikina. Mwandishi anasema hivi: “*Ni rahisi kuelewa ni namna gani Wakristo wa jina, wanaweza kuendelea kutegemea imani za kishirikina. Lakini, inasikitisha kuona kwamba, jambo hili lipo kwa kiasi kikubwa, hata miongoni mwa Wakristo walio komaa.*” Kwa baadhi ya Wakristo, na hata kwa baadhi ya wachungaji, jaribu la kurudi kwenye ushirikina kwa ajili ya kutapa msaada, wakati mwingine huwa ni jambo lenye nguvu sana.

Mchungaji Chiaka, alikuwa mchungaji wa kanisa moja huko Nigeria, lakini kanisa lake halikuwa likiendelea vizuri, kwa sababu kulikuwa na matatizo katika kanisa. Alikuwa na shauku kubwa ya kufanikiwa, kwa hiyo akaenda kwa mganga wa jadi, kutoa sadaka ya kuku na mbuzi, ili apate nguvu. Alisema hivi: ‘*wakati huduma yangu ilipokuwa ikianza tu, watu fulani walinitolea vitisho, kwa hiyo nilienda kumwona rafiki yangu, aliyekuwa mchungaji – na akanipeleka kwa mganga wa jadi. Nilimwomba mganga wajadi anitengenezee hirizi ya kunilinda, na ya kusaidia kanisa langu kukua. Alinipa vitu fulani vya kumeza, na akaniambia kwamba hakuna mtu angweza kuniua, na kwamba ningekuwa na nguvu za kufanya miujiza*’’. Badala ya kutafuta msaada kwa Mungu, alichagua kwenda kwa mganga wa jadi, kutafuta msaada. Matokeo yake, alijikuta yuko katika matatizo mengi zaidi, na miezi michache baadaye, alihitaji kufunguliwa kutoka nguvu za mapepo! Na hii ni kweli kwamba, Wakristo amba wameanguka katika hali kama hiyo, mara zote hujikuta katika mateso mengi sana.

Jambo hili huitwa '**kuchanganya imani**'. Na maneno haya yanamaana ya '**kuchanganya pamoja**'. Nikitendo cha kuchanganya pamoja imani za dini tofauti. Hii ni pale mtu anapochukua baadhi ya imani kutoka dini moja, na pia kuchukua baadhi ya imani kutoka dini nyingine, au utamaduni. Na kwa hiyo, tatizo linapotokea katika maisha yake, na kama ni Mkristo, anaweza kuomba kwa Mungu, lakini pia anaweza kwenda kutafuta msaada kwa mganga wa jadi. Jaribu la kurudi kwenye imani yake ya mwanzo, linaweza kuwa na nguvu sana. Basi, Biblia inasema nini kuhusu jambo hili? Kwa kweli, Biblia iko wazi sana. Ngoja niwakumbushe kuhusu mistari michache: **Mambo ya Walawi 19:31:** "*Msiwaendee waaguzi wa mizimu wala wachawi ili kuwaomba wawaagulie, na hivyo mkajitia najisi*". Haya maelekezo yako wazi sana – kwamba msiende kwa waganga.

Katika **Kumbukumbu la Torati 18:14**, Mungu anawaambia hivi Waisraeli*. Ninafikiri kwamba, kuna watu katika kanisa; hata baadhi ya wachungaji, ambao wanaweza kusimama mbele ya kanisa, na kusema kwamba, ni vibaya kwenda kumwona mganga wa jadi. Lakini matatizo yanapokuja katika maisha yao, wao wenywewe wanaweza kwenda kutafuta msaada kwa waganga wa jadi, na kufanya mambo ambayo yamekatazwa na Biblia. Hii huwa inatokea, na tunajua hivyo, lakini Biblia inaweka wazi sana kwamba, kwenda kwa waganga wa jadi, na kupata maelekezo kutoka kwao ni kosa.

Kiongozi wa Kikristo anapokutana na tatizo kubwa - je, huwa anaenda wapi kupata msaada? Je, wewe kama mchungaji au mwinjilisti, unapopata matatizo, katika maisha yako na huduma yako - je, huwa unamwendea nani kwa ajili ya msaada? Je, watu wanapokuja katika kanisa lako, na kukuomba ushauri, je huwa unawaambia waende wapi? Tunapaswa kutambua kwamba, ingawa waganga wa jadi wanaweza kuwa na nguvu kiasi, nguvu hizo hazitoki kwa Mungu. Na kama hazitoki kwa Mungu, basi zinatoka kwa Shetani, na hii inaweza kuleta shida tu. Tunapaswa kuzuia jaribu la kutafuta msaada kutoka nguvu nyingine, na kuelekeza macho yetu kwa Mungu tu, kwa sababu, ye ye pekee ndiye anaweza kutusaidia.

Kwa hiyo, tumeangalia majaribu makubwa **4**, ambayo kiongozi anaweza kukutana nayo katika maisha yake. Inaweza kuwa asubuhi hii ulikuwa umekaa ukisikiliza, na inaweza kuwa umegundua kwamba, baadhi ya majaribu haya ni halisi katika maisha yako. Baadhi yenu yaweza kuwa mmeanguka katika baadhi ya majaribu haya. Baadhi yenu inawezekana mnapambana na jaribu moja wapo au mawili, katika maisha yenu kwa sasa. Kama ni hivyo, unahitaji kutubu, na kuanza kazi yako na Mungu. Na labda, unahitaji mtu fulani aombe kwa ajili yako. Ninapenda kukutia moyo kwamba, ufanye hivyo kabla ya semina hii kuisha.

Lakini hapa kuna neno la onyo, na kwa kweli linatoka moja kwa moja kwenye kitabu cha **1 Wakorintho**. Inawezekana umekuwa umekaa hapa, ukifikiri kwamba hakuna jaribu hata moja kati ya majaribu haya, ambalo linakuhusu wewe. Kama hii ni kweli – je, Paulo anakwambia nini? **1 Wakorintho 10:12:** "*Kama unajidhania kwamba umesimama, angalia usianguke*". Unaweza kufikiri kwamba, majaribu haya hayawezi kuwa tatizo kwako. Kuwa makini sana kama unafikiri hivyo! Kwa sababu, Shetani atafanya kila njia ili akuangushe. Na Paulo anasema hivi, katika mstari **13:** "*Mungu ni mwaminifu, naye hata ruhusu mjaribiwe kupita nguvu zenu, ila pamoja na majaribu, ye ye atawapeni pia nguvu ya kustahimili, na njia ya kutoka humo salama*".

"NIONESHE KIONGOZI MWADILIFU". KIPINDI 12: "Jinsi Ya Kukabili Majaribu".

Ngoja tufungue **Luka 4:1-13**, na tutasoma kuhusu majaribu ya Yesu. Baada ya kuangalia baadhi ya majaribu, ambayo huwakabili viongozi leo, minataka pia tuangalie jinsi Yesu alivyuo kabili majaribu yake. **Luka 3** inatuambia kuhusu ubatizo wa Yesu. Maelfu ya watu waakisafiri kutoka Yerusalem, kwenda kumwona Yohana Mbatizaji, na kuna makundi makubwa ya watu, wamekusanyika katika Mto Yordani, karibu na **Yeriko**. Kuna msururu mrefu wa watu wanawataka kubatizwa – lakini ghafla, anatokea Yesu, na kusimama mbele ya Yohana. Na Yesu anaomba kubatizwa na Yohana. Tumeambiwa kwamba, Yesu alipotoka kwenye maji, mbingu zilifunguka, na Roho Mtakatifu akashuka juu yake katika umbo la njiwa. Mungu Baba anamwambia Yesu kwa sauti kubwa: "*Wewe ndiwe mwanangu mpandwa, nimependezwa nawe*". Na kisha, katika sura **4**, tunaona kwamba, Yesu anachukuliwa kutoka Mto Yordani, na kukaa jangwani kwa siku **40**.

Je, wewe ungependa kukaa jangwani kwa siku 40? Je, ungependa kukaa siku **40** bila chakula?! Nadhani kwamba, hakuna hata mmoja ambaye angependa kufanya kama alivyofanya Yesu. Hapa aliquwa katika jangwa la **Yudea** – siyo mbali sana kutoka Yerusalem. Nimewahi kuliona jangwa hili kwa macho yangu mwenywewe, na ninaweza kusema kwamba, mimi binafsi nisingetaka kukaa hata siku moja tu, nikitembea

katika jangwa hilo! Siyo jangwa la mchanga, lakini ni eneo kubwa la milima, na miamba, na miteremko mikali. Hakuna miti, na kipindi kirefu cha mwaka, huwa hakuna mvua. Wayahudi walifikiri kwamba, ilikuwa ni sehemu ya ukiwa; sehemu ambayo mapepo yaliishi, na sehemu ambayo wanyama wa porini waliishi. Wanyama kama mbwa mwitu, simba, na chui. Ilikuwa sehemu hatari sana, eneo la upweke, na sehemu ya ukatili. Na bado Yesu aliweza kuishi huko, kwa siku arobaini – huo ni muda wa majuma **6**!

Na kipindi hicho, Yesu alijaribiwa na Shetani. Lakini tambua kwamba, katika mstari **2**, hausemi kwamba, Yesu alijaribiwa mara tatu tu. Inasema kwamba: “*aliongozwa na Roho Mtakatifu kwenda jangwani, ambako alijaribiwa kwa siku arobaini*”. Kwa kweli, hiki ni kipindi kirefu cha majoribu – lakini tunachosikia ni kuhusu majoribu matatu tu. Na inaonekana kwamba, majoribu haya matatu yalikuja mwishoni mwa siku hizo **40**, wakati amba Yesu amekuwa dhaifu, na nguvu ya kuzuia majoribu imepungua. Tumeambiwa kwamba: “*hakula kitu chochote katika siku hizo arobaini, na mwishoni alikuwa na njaa sana*”. Hebu fikiri kuhusu kitendo hiki - cha kukaa bila chakula kwa siku arobaini, na kisha Shetani anakuja kwa Yesu, katika mstari **3**, akiwa na maneno haya: “*Kama wewe ni mwana wa Mungu, amuru mawe haya kuwa mkate*”.

Jambo la kwanza tunalopaswa kuona, kuhusu majoribu haya, ni kwamba yalikuwa majoribu halisi kabisa. Yaliupa changamoto utu wa Yesu. Wakati mwingine, tunaposoma aya hii, tunasahau kwamba, Yesu alikuwa mwanadamu kwa asilimia **100**. Kwa kweli, unapoangalia sura **3**, utaona kwamba, **Luka** amekuwa akitukumbusha kwamba, ingawa Yesu alikuwa Mungu, bado pia alikuwa mwanadamu. Hili ni jambo ambalo tunapata ugumu sana kulielewa – kwamba alikuwa mwanadamu kwa asilimia **100**, na pia alikuwa Mungu kwa asilimia **100**. Hili ni fumbo - lakini tunapaswa kuliadimi, kwa sababu Biblia inatuambia hivyo. Alikuja duniani katika umbo la binadamu – na katika kila namna alifanana na sisi – isipokuwa katika jambo moja: hakuwa na dhambi. Lakini kwa sababu alichukua umbo la binadamu, alikuwa na uwezo wa kufanya dhambi. Kama hapa kuwa na uwezekano wa yeche kufanya dhambi, basi majoribu hayo yasingekuwa na maana yeote. Tafadhalii tukumbuke kwamba, Yesu alimkabilii Shetani akiwa kama mwanadamu wa kawaada kama sisi.

Je, ni kwa muda gani mrefu zaidi ambaa ulikaa bila chakula? Labda wakati wa kufunga, au wakati wa kuugua - labda kwa siku chache tu. Labda siku **3**, au **4**, au hata wiki? Mwisho wa kipindi hicho – je, ulihisi njaa? Kwa kweli, lazima ulihisi njaa! Lakini fikiri jinsi gani utakuwa na njaa, kama hautakula chakula kwa muda wa wiki **6**! Yesu sasa alikuwa katika kipindi chake cha kuishiwa nguvu, na mwili wake, ulikuwa unatamani chakula. Lakini kuna kitu fulani, ambacho kililetu ugumu zaidi kwa Yesu, ambacho hatuwezi kukielewa. Kama Mwana wa Mungu, Yesu alijua kwamba alikuwa na nguvu ndani yake, nguvu za kuweza kubadili yale mawe kuwa mkate. Kama angetaka kufanya hivyo – angweza kufanya. Kwa hiyo, jaribu hili ni halisi sana na lazima ilikuwa vigumu sana kwa Yesu kulipinga.

Je, Yesu anasema nini? Anarejea kwenye Agano la Kale, na kunukuu maneno kutoka **Kumbukumbu la Torati 4:3**: “*Imeandikwa, mtu hata ishi kwa mkate tu*”. Kwa kweli, katika majoribu haya matatu, Yesu anaendelea kurejea kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Ananukuu mara **3** kutoka kitabu hiki. Labda, wakati wa kipindi hiki, Yesu alikumbuka kuhusu Waisraeli, ambaa walikaa katika jangwa kwa muda wa miaka **40**, na hii ilitokea kama umbali wa kilometra **300**, kusini kutoka pale alipokuwa Yesu. Anakumbushwa kilichotokea wakati wa Waisraeli, na kisha ananukuu kutoka **Kumbukumbu la Torati 8:3***.

Yesu anamwambia Shetani: “*Nguvu inayoniwezesha kuishi haitoki katika mkate tu – inatoka kwa Baba yangu. Kufanya mapenzi yake ni muhimu zaidi kuliko kuridhisha mahitaji yangu. Sitabadili mawe haya kuwa mkate, lakini nitamwamini Baba yangu na neno lake. Mimi siishi kwa mkate tu*”. Je, Yesu anasema nini hapa? Anasema kwamba, maisha ya mtu hayategemei katika kujaribu kurizisha njaa ya mwili tu, lakini pia kuna sehemu ya kiroho katika maisha ya mtu, ambayo ni muhimu zaidi. Je, hii inamaana gani kwetu kama viongozi? Kufanya mapenzi ya Mungu, linapaswa kuwa jambo la msingi zaidi kwetu, kuliko mahitaji yetu ya kimwili. Kumtii Mungu na kufanya mapenzi yake ni muhimu zaidi, kuliko kushibisha matumbo yetu! Kumtii Mungu na kufanya mapenzi yake, ni muhimu zaidi kuliko kutimiza matakwa yetu ya kimwili. Na hapa katika mstari **3** na **4**, Yesu amepitia jaribu lake la kwanza.

Katika mstari **5-7** Shetani anajaribu tena. Anampeleka Yesu juu ya mlima, kwa namna fulani, anafanikiwa kumwonesha Yesu, falme zote za ulimwengu. Na kisha, Shetani anamwambia kitu fulani cha kuchanganya: Mstari **6** na **7***. Je, ni kwa namna gani Shetani anaweza kusema maneno haya kwa Yesu? Kumbuka kwamba, Yesu kabla ya kuwa mwanadamu, alikuwa na Mungu Baba mbinguni, na waliumba ulimwengu, pamoa na Roho Mtakatifu. Sikiliza maneno haya kutoka **Wakolosai 1:15***. Sababu peke kwamba ulimwengu huu upo hapa leo, ni kwamba Yesu anaushikilia.

Shetani anasimama mbele ya Yesu – na kumwambia hivi: “*kila kitu unachokiona ni changu, na nina mamlaka ya kumpa yeyote nikipenda*”. Je, Yesu alijisikia vipi kuhusu jambo hili? Je, unadhani kwamba, alijaribiwa kunukuu mistari mingi kutoka Agano la Kale, ambayo inaonesha kwamba, Mungu ndiye aliyeumba ulimwengu? Labda alijaribiwa kufanya hivyo. Lakini, kuna kitu cha kusitusha, katika tukio hili, Shetani kwa sehemu fulani alikuwa anasema ukweli. Nina maana gani kusema hivi? Shetani alikuwa na uwezo wakumpa Yesu falme za dunia, kwa sababu kwa kweli yeye anamamlaka juu ya falme za dunia! Ngoja ni wasomee kutoka **1 Yohana 5**. Katika mstari **19**, inasema hivi: “*Tunajua kwamba sisi ni wake Mungu, ingawa ulimwengu wote unatawaliwa na Shetani*”.

Katika injili ya **Yohana**, Yesu anamsema Shetan, mara **3**, kama “*mfalme wa ulimwengu*”. Kwa nini? Je, unakumbuka nini kilitokea katika **Bustani ya Edeni**? Adamu na Hawa, waliamua kuwa sawa na Mungu, na Shetani aliwajaribu kuchukua tunda kutoka ule mti. Hili lilikuwa jaribu la kwanza kabisa kutokea – na walianguka katika jaribu hili. Tangu wakati huo, uhusiano kati ya Mungu na wanadamu ukavunjika, na ulimwengu wote ukawa chini ya utawala wa Shetani. Hata ulimwengu wa asili uliathirika, kwa sababu kifo cha kimwili kiliingia duniani, Adamu na Hawa walipotenda dhambi. Sasa, nahitaji kusema kwamba, utawala wake Shetani unakikomo, kwa sababu mmiliki halisi ni Mungu. Lakini kwa sasa, Shetani anafanya sehemu ndogo tu ya umiliki, hasa juu ya watu wasio milikiwa na Kristo.

Hapa ni Shetani – na anamwonesha Yesu mataifa, na watu wa ulimwengu. Na anamwambia Yesu, kama utanisujudia, na kuniabudu, utapata falme hizi. Je, jaribu hili linahusu nini hasa? Kwa kweli, lilimpa Yesu njia rahisi ya kuwa mfalme. Shetani anajaribu kumjaribu Yesu kwa kusema: hauhitaji kwenda msalabani. Hauhitaji kupitia maumivu. Niabudu mimi sasa hivi – na falme zote zitakuabudu wewe. Je, jibu la Yesu ni nini, katika mstari **8**? “*Imeandikwa mwabudu Bwana Mungu wako na kumtumikia yeye pekee*”. Yesu ananukuru tena kutoka kitabu cha **Kumbukumbu la Torati (6:13)**, ambapo Musa aliwaonya Waisraeli dhidi ya kuabudu sanam, na miungu ya mataifa. Na akitumia maneno haya machache, Yesu yuko wazi sana: “*Wewe Shetani, hakuna namna yoyote ambayo ninaweza kukuabudu wewe. Mimi ninamwabudu Mungu Baba pekee, na niko hapa kwa ajili ya kumtumikia yeye, na nitafanya mapenzi yake, kwa gharama yoyote*”.

Na hivi ndivyo ilivyo kwetu leo, kwa sababu Baba yetu wa mbinguni, anatuambia kumwabudu yeye pekee. Anatuambia kumtumikia yeye tu. Anatukataza kuabudu miungu mingine. Je, tunamwabudu na kumtumikia yeye tu - au tunatumia muda mwingi kuabudu miungu wengine, na Mwenyezi-Mungu tumemsahau? Ninajua kwamba, kimwili hatupigi magoti chini kuabudu miungu, lakini, kitu chochote ambacho kinachukua nafasi ya Mungu, katika maisha yetu, ni muungu. Yesu anasema hivi: “*Mwabudu Bwana Mungu wako, na kumtumikia yeye pekee*”. Yesu alijua kwamba, mpango wa Mungu ulikuwa kwamba yeye lazima aende msalabani. Pia alijua kwamba, kama angetimiza mpango kwa Baba yake, baadaye muda ungefika, ambapo ulimwengu wote ungemwabudu yeye. Na unaposoma kitabu cha **Ufunuo**, utaona kwamba hii itatokea siku zijazo. “*Kila goti litapigwa, na kila ulimi utakili kwamba Yesu Kristo ni Bwana*”. Itatokea wakati Yesu atakaporudi kwa mara ya pili.

Hatimaye, angalia mstari **9** hadi **12**, ili kuona jaribu **3**. Tunasoma kwamba, Shetani alimchukua Yesu kwenda Yerusalem, na wakasimama juu ya hekalu. Walipokuwa wamesimama juu ya paa, Shetani akamjaribu Yesu. Mstari **9**: “*Kama wewe ni Mwana wa Mungu, jitupe chin*”. Na kisha, inavutia kuona kwamba, Shetani alijaribu kutumia Neno la Mungu, ili amshinde Yesu. Ananukuru mstari kutoka Agano la Kale. Anatumia **Zaburi 91**: anasema hivi: “*Imeandikwa, Mungu atakuazigia malaika wakulinde, na tena watakuchukua mikononi mwao, usije ukajikwaa mguu kwenye jiwe*”.

Shetani anajaribu kumshawishi Yesu aruke. Anajua kwamba, Yesu anahitaji kutii neno la Baba yake, na kwa hiyo anajaribu kumjaribu kwa kutumia Biblia. Shetani alisema hivi: “*Yesu, unaniambia kwamba wewe umejitoa kutii neno la Baba yako – thibitisha jambo hili kwangu. Baba yako anasema kwamba ataamuru malaika wakuokoe, na kukulinda – thibitisha kwangu, ni kwa namna gani unamwamini Baba yako – hasa kama unasema wewe ni mtoto wake*”. Nafikiri kwamba hiki ndicho anachofikiri Shetani hapa. Tena, Yesu angeweza kufanya hivyo, na labda malaika wangkuja kutoka mbinguni kumuokoa – lakini alijua kwamba, Mungu hakuwa amemwamuru kufanya hivyo. Alijua kwamba, ingawa yeye ni Mwana wa Mungu, hawezি kwenda na kufanya jambo kwa nguvu zake mwenyewe, na halafu akategemea kwamba Mungu atamlinda.

Mara kwa mara, katika Agano Jipy, tunamsikia Yesu akisema: “*Mimi ninafanya yale ambayo Baba yangu ananiagiza kufanya*”. Yesu anajibu nini? Anarudi katika **Kumbukumbu la Torati 6**, na safari hii anarejea mstari **16**: “*Usimjaribu Bwana Mungu wako*”. Waisraeli walikuwa wameona miujiza mingi sana, walipokuwa wakitembea jangwani, na baada ya muda fulani, walianza kutarajia kwamba, Mungu angewafanyia miujiza mara tu watakapo-mwomba. Na Mungu anawaambia Waisraeli – **msinjaribu**.

Kwa jinsi hiyo hiyo, Yesu anamwambia Shetani: “*Sihitaji kuthibitisha uaminifu wa Mungu kwangu, na sitamjaribu Baba yangu kwa namna hii*”. Katika jangwa, Yesu alipitia majaribu matatu yenyeye nguvu sana – na inawezekana alipata majaribu mengine zaidi – lakini mara zote hakuanguka katika majaribu, na kushindwa kumpinga Shetani. Tumeambiwa katika mstari **13** kwamba: “*Shetani alipomaliza kumjaribu, alimwacha Yesu, hadi wakati mwingine*”. Je, unajua hii inamaana gani? Kulikuwa na matukio mengi sana, ambapo Shetani alijaribu kumjaribu Yesu – hili halikuwa tukio pekee. Kulikuwa na majaribu mengi zaidi kwa Yesu. Lakini safari hii katika injili ya **Luka**, tunaona kwamba, Shetani anamwacha Yesu. Je, Yesu alisikisikaje wakati Shetani alipokuwa ameondoka kwake? Alikuwa amechoka sana. Je, ninawezaje kujua? Fungua katika **Mathayo 4:11**. Inasema hivi: “*Shetani akamwacha Yesu, na malaika wakaja kumtumikia*”. Ninafikiri kwamba, Yesu amechoka sana hapa. Kumbuka kwamba, hajala kwa muda wa wiki **6**, na amekuwa katika vita na Shetani. Amepinga majaribu haya – lakini amemwacha akiwa dhaifu, na amechoka sana.

Ninafikiri kwamba, Baba anaangalia chini kutoka mbinguni, na anaona kwamba Mwanaye ameshinda vita, lakini pia anaona kwamba, Yesu amechoka sana, na kwa hiyo anatuma malaika wamsaidie. Huu ni upendo wa Mungu kwa Mwanaye. Tunahitaji kumshukuru Mungu kwamba, Yesu aliweza kumpinga Shetani. Kama asingempinga, basi pasingekuwa na wokovu kwetu. Pasingekuwa na msalaba. Pasingekuwa na kaburi wazi, na pasingekuwa na msamaha kwa dhambi zetu. Yesu alipinga majaribu, na akamaliza kazi aliyokuwa amepewa kufanya. Lakini, tunapohitimisha hapa – viperi kuhusu wewe na mimi? Kama viongozi katika kanisa – je, unakabili viperi majaribu yanayokujia? Je, unajua udhaifu wako ni nini? Kwa sababu Shetani anajua – na hayo ndiyo maeneo ambayo atalenga, ili kukujaribu na kukuangusha. Kwa hiyo, ni kwa namna gani unaweza kuwatayari, na je, huwa unayapingaje majaribu? Kwa ufupi sana, ngoja nitoe mapendekezo machache, ambayo yanaweza kukusaidia:

1. Majaribu kama hayo yanapokuja, tunahitaji kumwomba Mungu, na tunahitaji kumwita Yesu atusaidie. Kuna mstari wa ajabu sana katika **Waefeso 2:18**: “*Kwa kuwa Yesu mwenyewe alipitia mateso na majaribu, anaweza kutusaidia na sisi tunapajaribiwa*”. Tumeona jinsi majaribu yalivyo kuwa kwa Yesu. Anajua jinsi majaribu yalivyo, na kwa hiyo, anaweza kutusaidia tunapajaribiwa. Tunahitaji kumwomba atusaidie.

2. Tambua anasema nini katika **Luka 4:1**: “*Yesu alitoka mtoni Yordani, akiwa amejaa Roho Mtakatifu, akaongozwa na Roho mpaka jangwani*”. Hili ni somo ambalo tulifunza miaka miwili iliyopita; kujazwa na Roho Mtakatifu, na kuongozwa na Roho Mtakatifu. Kama Mkristo, na kama kiongozi – je, umejazwa Roho Mtakatifu? Katika huduma yako – je, unaongozwa na Roho Mtakatifu, au unajiongoza mwenyewe?

Katika **Waefeso 5:18**, Paulo anatusihi kwamba tujazwe na Roho Mtakatifu. Kadri tunavyojazwa na Roho Mtakatifu, ndivyo inakuwa vigumu zaidi kwetu kuanguka katika majaribu. Ingawa bado tutajaribiwa. Kumbuka, Yesu alikuwa amejazwa Roho Mtakatifu, lakini bado alijaribiwa. Lakini Roho Mtakatifu anapotujaza, Shetani hana mlango wa kuingilia, na tunatiwa nguvu za kumpinga. Kumbuka maneno ya Petro, katika **1 Petro 5:9**: “*Muwe imara katika imani, na kumpinga*”.

3. Unapopitia wakati wa majaribu, mshirikishe mwenzako mzigo ulionao. Mwambie mtu unayemwamini aombe pamoja nawe – na aombe kwa ajili yako.

4. Unaposoma hadithi hii katika **Luka 4**, utagundua kwamba, Yesu anakabili jaribu la tatu, kwa njia ile ile. Katika kila jibu, anarejea Biblia kwa kusema: “**imeandikwa**”. Anatumia mamlaka ya Neno la Mungu. Anamwambia Shetani, haya siyo maneno yangu, ni maneno ya Mwenyezi-Mungu, na kwa hiyo yana nguvu sana. Biblia ni silaha yenyeye nguvu sana dhidi ya Shetani. Kadri tunavyojua neno lake Mungu, ndivyo tutakavyoweza kulitumia zaidi, dhidi ya adui. Kwa hiyo, kama viongozi katika kanisa, Shetani anapokuja akigonga katika milango yetu, akijaribu kutujaribu – tunapaswa kwenda kwa Yesu kupata msaada; hebu tuwe viongozi walio jazwa Roho Mtakatifu; hebu tuwe viongozi wenye kuwaomba wengine waombe kwa ajili yetu; na hebu tuwe viongozi wanaojua Neno la Mungu, na wanaojua jinsi ya kulitumia dhidi ya adui Shetani.